ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID	-	SPIKA
1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais

9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13.Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais

19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
22. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
23. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
24. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
25. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
26. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
27. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
28. Mhe.Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
29. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe

30. Mhe. Ali Salum Haji - Jimbo la Kwahani
31. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) - Jimbo la Kijitoupele
32. Mhe. Ame Haji Ali - Jimbo la Nungwi
33. Mhe. Amina Iddi Mabrouk - Nafasi za Wanawake
34. Mhe. Asha Abdalla Mussa - Jimbo la Kiwengwa
35. Mhe. Bahati Khamis Kombo - Jimbo la Chambani
36. Mhe. Bihindi Hamad Khamis - Nafasi za Wanawake
37. Mhe. Hamad Abdalla Rashid - Jimbo la Wawi
38. Mhe. Hamida Abdalla Issa - Nafasi za Wanawake
39. Mhe. Hamza Hassan Juma - Jimbo la Shaurimoyo
40. Mhe. Hassan Khamis Hafidh - Jimbo la Welezo
41. Mhe. Hidaya Ali Makame - Nafasi za Wanawake
42. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa) - Jimbo la Mtoni
43. Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Jimbo la Paje
44. Mhe. Khadija Omar Kibano - Jimbo la Mtambwe
45. Mhe. Machano Othman Said - Jimbo la Mfenesini
46. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti - Jimbo la Mtopepo
47. Mhe. Makame Said Juma - Jimbo la Kojani
48. Mhe. Maryam Thani Juma - Jimbo la Gando
49 Mhe. Masoud Abrahman Masoud - Jimbo la Bububu
50. Mhe. Mihayo Juma N'hunga - Jimbo la Mwera
51. Mhe. Miraji Khamis Mussa - Jimbo la Chumbuni
52. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha - Jimbo la Mtambile
53. Mhe. Mohamed Said Mohamed - Jimbo la Mpendae
54. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini
55. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini
56. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake
57. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole
58. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani
59. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake
60. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake
61. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani
62. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy- Jimbo la Chaani
63. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni
64. Mhe. Omar Seif Abeid - Jimbo la Konde
65. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake

66. Mhe. Rashid Makame Shamsi	-	Jimbo la Magomeni
67. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa	-	Nafasi za Wanawake
68. Mhe. Said Omar Said	-	Jimbo la Wingwi
69. Mhe. Said Hassan Said	-	Mwanasheria Mkuu
70. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma	-	Nafasi za Wanawake
71. Mhe. Salma Mussa Bilal	-	Nafasi za Wanawake
72. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Nafasi za Wanawake
73. Mhe. Shaib Said Ali	-	Jimbo la Chonga
74. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Jimbo la Micheweni
75. Mhe. Simai Mohammed Said	-	Jimbo la Tunguu
76. Mhe. Suleiman Makame Ali	-	Jimbo la Ziwani
77. Mhe. Suleiman Sarahan Said	-	Jimbo la Chakechake
78. Mhe. Tatu Mohamed Ussi	-	Nafasi za Wanawake
79. Mhe. Ussi Yahya Haji	-	Jimbo la Mkwajuni
80. Mhe. Viwe Khamis Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
81. Mhe. Wanu Hafidh Ameir	-	Nafasi za Wanawake
82. Mhe. Yussuf Hassan Iddi	-	Jimbo la Fuoni
83. Mhe. Zaina Abdalla Salum	-	Nafasi za Wanawake
84. Mhe. Zulfa Mmaka Omar	-	Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem	-	Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Ishirini na Tano – Tarehe 22 Juni, 2016

(Kikao Kilianza saa 3:00 za asubuhi)

Dua

Mhe. Naibu Spika *(Mhe. Mgeni Hassan Juma)* Alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

UTARATIBU

Mhe. Mjumbe: Utaratibu Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Hata shughuli hatujaanza, tunaanza utaratibu.

Mhe. Mjumbe: Ndio, kwa sababu hatuna *mandate* ya kuendelea na Baraza wakati akidi haijatimia ndani ya Baraza hili. Tuko robo ya wajumbe hapa.

Mhe. Naibu Spika: Wanaingia sasa hivi. Hebu tulia.

Mhe. Mjumbe: Sio utaratibu. Unatakiwa taratibu kwanza...

Mhe. Naibu Spika: Wanakuja, wanaingia tulia, tulia.

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Biashara, Viwana na Masoko, kwa mwaka 2016/2017. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Shadya Mohamed Suleiman: (Kny: Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo): Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mwenyekiti, naomba kuweka hati mezani ya hotuba ya maoni ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo, kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko, kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 - Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu sasa likae kama Kamati ya Mapato na Matumizi kwa ajili ya kupokea, kuzingatia, kuchangia na hatimae kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa kazi za kawaida na maendeleo kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mhe. Naibu Spika, kwanza naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutuwezesha kufika katika ukumbi huu hii leo tukiwa wazima na afya njema. Aidha, naomba kuchukuwa fursa hii kukushukuru wewe binafsi pamoja na wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa mashirikiano makubwa, michango na ushauri mliotupatia kwa lengo la kufanikisha utekelezaji wa malengo ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2015/2016. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii pia kumpongeza kwa dhati Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kuchaguliwa tena kuiongoza Zanzibar kwa kipindi cha miaka mitano ijayo, kuanzia mwaka 2015/2020. Namuomba Mwenyezi Mungu ampe nguvu ya kuongoza nchi yetu kwa uadilifu, hekima na upendo ili tuweze kuishi kwa amani, utulivu na mshikamano. Aidha, nachukua fursa hii kukupongeza wewe binafsi kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika wa Baraza hili, nakutakia mafanikio katika kutekeleza shughuli zako katika kuhakikisha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inawatumikia wananchi kwa usawa bila ya ubaguzi au upendeleo. *(Makofi)*

Kadhalika, nachukua fursa hii kumpongeza Makamu wa Pili wa Rais, Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi kwa kuchaguliwa tena katika nafasi hiyo na namtakia kila la kheri katika utekelezaji wa majukumu yake ya kumsaidia Mheshimiwa Rais wa Zanzibar katika kuwatumikia wananchi wa Zanzibar. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, napenda vile vile kuchukua fursa hii kuwashukuru kwa dhati ya moyo wangu Katibu Mkuu Nd. Bakari Haji Bakari, Wakurugenzi na Viongozi wote wa taasisi na Mashirika yaliyo chini ya Wizara yangu, pamoja na wafanyakazi wote kwa juhudi zao kubwa za kuchapa kazi pamoja na mashirikiano makubwa wanayonipatia. Hakika bila ya msaada wao ingeniwia vigumu sana kutekeleza majukumu yangu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa hili ni Baraza la kwanza la Bajeti baada ya Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 2015, kwa unyenyekevu naomba nimshukuru Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt Ali Mohamed Shein kwa kuniteua kuwa mjumbe wa Baraza la Wawakilishi na kunipa dhamana ya kuiongoza Wizara hii. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, naomba kuliarifu Baraza lako kuwa Muundo wa Wizara hii ulifanyiwa mabadiliko ambapo majukumu ya usajili wa Biashara na mali ambayo yalikuwepo katika iliyokuwa Wizara ya katiba na Sheria yamehamishiwa katika Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko ambapo Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali itasimamiwa na wizara yangu. Aidha, katika mabadiliko hayo, Idara Kusimamia Ushindani halali wa Biashara pia imeongezeka katika muundo huo mpya wa Wizara.

Mhe. Naibu Spika, kabla ya mabadiliko hayo, Wizara yangu ilikuwa inasimamia Idara nne (4) ambazo ni Idara ya Mipango, Sera na Utafiti, Idara ya Utumishi na Uendeshaji, Idara ya Biashara na Masoko, na Idara ya Maendeleo ya Viwanda, pamoja na Ofisi Kuu ya Wizara Pemba. Aidha, Wizara pia inasimamia Shirika la Biashara la Taifa (*ZSTC*), Taasisi ya Viwango ya Zanzibar, Baraza la usimamizi wa Utoaji wa Leseni za Biashara, pamoja na Baraza la Taifa la Biashara.

Mabadiliko hayo Mhe. Naibu Spika, yatasababisha kufanyika kwa mapitio ya maudhui ya ala (*instruments*) kuu za kiutendaji kama vile, Dira ya Wizara, Dhamira na Malengo yake Makuu, Mpango Mkakati wa Viwanda ili kujielekeza katika utekelezaji wa majukumu mapya ya Wizara.

Mhe. Naibu Spika, matayarisho ya bajeti hii yamezingatia malengo ya Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2020, Ilani ya CCM ya mwaka 2015/2020, mambo mbali mbali yaliyoainishwa katika hotuba ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mh Dkt. Ali Mohamed Shein, wakati wa uzinduzi wa Baraza la Wawakilishi la tisa, Mpango wa Ukuzaji Uchumi na Kuondoa Umasikini Zanzibar (*MKUZA III)*, Maelekezo ya Serikali pamoja na ukomo wa bajeti. Kadhalika, mapendekezo haya yamezingatia muongozo wa utayarishaji bajeti uliotolewa na Wizara ya Fedha na Mipango ambao umesisitiza utayarishaji wa bajeti kwa kuzingatia changamoto zifuatazo:

i. Kushuka kwa mapato ya ndani;
ii. Kusita au kupungua kwa misaada ya kuendesha bajeti; na
iii. Kudhoofika kwa sarafu ya Tanzania.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na mazingatio ya hapo juu bajeti hii imezingatia malengo makuu ya mikakati ya kuendeleza viwanda ili viongeze kuchangia Pato la Taifa kuwapatia ajira wananchi wakiwemo vijana na wanawake. Pia kupunguza uagiziaji wa nje kwa bidhaa zinazoweza kuzalishwa nchini na kuongeza uzalishaji wa bidhaa na mazao ya kuuza nje ili kuongeza fedha za kigeni na pia kuongeza Pato la Taifa.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na mazingatio ya hapo juu, utayarishaji wa mapendekezo haya ulizingatia pia matukio mbali mbali yaliyojitokeza ulimwenguni ambayo yamekuwa na athari za moja kwa moja katika mwenendo wa biashara na uchumi duniani. Matukio hayo ni kama vile mwenendo wa uwekezaji duniani, biashara, maendeleo ya biashara na fedha na pia machafuko ya kisiasa katika baadhi ya maeneo duniani.

Mhe. Naibu Spika, kama kawaida, mapendekezo ya bajeti hii yamepitia katika ngazi mbali mbali za uzingatiaji wa awali, ikiwemo Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ya Baraza la Wawakilishi. Naomba kuchukua fursa hii kuishukuru sana Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ya Baraza la Wawakilishi inayoongozwa na;

Mhe. Yussuf Hassan Iddi Mwakilishi wa Jimbo la Fuoni, ambaye ni Mwenyekiti, pamoja na wajumbe wake:

Mhe. Hamida Abdalla Issa	Mjumbe
Mhe. Ussi Yahya Haji	Mjumbe
Mhe. Ali Salum Haji	Mjumbe
Mhe. Hamad Abdalla Rashid	Mjumbe
Mhe. Mohemmed Mgaza Jecha	Mjumbe
Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Mjumbe
Mhe. Shadya Mohammed Suleiman	Mjumbe
Ndg. Salum Khamis Rashid	Katibu
Ndg. Abubakar Mahmoud Iddi	Katibu

Nawashukuru wajumbe wote pamoja na Mwenyekiti, kwa kuchambua mapendekezo ya awali ya bajeti hii na hatimae kuridhia kuwasilishwa mbele ya Baraza lako tukufu kwa kujadiliwa na kuidhinishwa.

Mhe. Naibu Spika, katika hotuba yangu hii, nitaanza kwa kufanya mapitio ya jumla kuhusu mwenendo wa biashara duniani, mwenendo wa biashara Zanzibar, mapitio ya hali ya viwanda, utekelezaji wa malengo ya bajeti ya wizara kwa mwaka 2015/2016, hali ya mashirika na taasisi zinazosimamiwa na wizara, kubainisha changamoto zilizojitokeza katika kutekeleza bajeti ya

mwaka 2015/2016, na hatimae kubainisha Programu za Wizara kwa mwaka 2016/2017.

MWENENDO WA BIASHARA NA MASOKO

Hali ya Biashara Duniani

Mhe. Naibu Spika, hali ya ukuaji wa biashara duniani kwa kipindi cha mwaka 2015 haikuwa na mabadiliko makubwa na iliendelea kama ile ile ya mwaka 2014 ambayo ni asilimia 2.8. Hali hiyo imesababishwa na athari za kuzorota kwa uchumi wa China, athari za masoko ya kifedha iliyosababishwa na mtikisiko wa fedha nchi za Ulaya ya kusini, pamoja na madeni makubwa ya nchi zinazoendelea.

Hata hivyo, athari hizo zinategemewa kupungua ikiwa mabenki ya Ulaya yatasaidiwa kifedha kuweza kukuwa kwa haraka katika sarafu ya Euro. Kwa ujumla, kupungua kwa biashara ya dunia kumesababishwa na mabadiliko ya thamani ya fedha za kigeni, pamoja na kupungua kwa bei za bidhaa (*commodity price*). Thamani hiyo imepungua kwa asilimia 13 na kufikia USD 16.5 trilion kwa mwaka 2015 ikilinganishwa na USD 19 trilioni mwaka 2014.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka 2017, hali ya biashara duniani inatarajiwa kuendelea kukua kwa asilimia 3.6, ukuaji huo hata hivyo bado upo chini ikilinganishwa na ukuaji wa wastani wa asilimia 5 tokea miaka ya 1990.

Usafirishaji na Uagizaji wa Bidhaa Duniani

Mhe. Naibu Spika, taarifa ya biashara ya kimataifa ya mwaka 2015 inayotolewa na Shirika la Biashara la Dunia (*World Trade Organisation – WTO*), inaonesha kwamba usafirishaji wa bidhaa duniani kwa mwaka 2015 ulipungua na kufikia USD 15,985 bilioni kutoka usafirishaji wa USD 18,427 bilioni katika mwaka 2014. Katika usafirishaji huo, nchi za Ulaya ziliongoza kwa kusafirisha bidhaa zenye thamani ya USD 5,958 bilioni zikifuatiwa na nchi za Asia zilizosafirisha bidhaa zenye thamani ya USD 5,464 bilioni. Marekani ya Kaskazini imesafirisha bidhaa zenye thamani ya USD 2,294 bilioni, na nchi za Afrika zilisafirisha bidhaa zenye thamani ya USD 388 bilioni.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa uagiziaji bidhaa duniani, taarifa hiyo imeonesha kwamba uagiziaji wote ulifikia USD 16,340 bilioni kwa mwaka 2015 ikilinganishwa na uagiziaji wa bidhaa wenye thamani ya USD 18,574 bilioni zilizoagizwa kwa mwaka 2014. Nchi ambazo ziliongoza katika uagiziaji

huo ni Ulaya (USD 5,899 bilioni), nchi za Asia (USD 5,018 bilioni), na nchi za Marekani ya kaskazini (USD 3,151 bilioni). Katika uagiziaji huo wa bidhaa, nchi za Afrika ziliagiza bidhaa zenye thamani ya USD 559 bilioni kwa mwaka 2015. Mwenendo wa usafirishaji na uagiziaji huo ni kama unavyoonekana katika Jadweli Nam. 1 hapa chini.

Jadweli Nam. 1

Usafirishaji na Uagiziaji Bidhaa Duniani 2015 (USD bilioni)

Kanda	Usafirishaji	Asilimia	Uagiziaji	Asilimia
Ulaya	5,958	37.3	5,899	36.1
Asia	5,464	34.2	5,018	30.7
Marekani/ kaskazini	2,294	14.4	3,151	19.3
Mashariki ya Kati	841	5.3	747	4.6
Jumuiya ya Madola	500	3.1	345	2.1
Marekani/Kusini	540	3.4	622	3.8
Afrika	388	2.4	559	3.4
Jumla	**15,985**	**100**	**16,341**	**100**

Chanzo: *World Trade Organization* (WTO)

Hali ya Biashara Zanzibar

Usafirishaji na Uagiziaji wa Bidhaa

Mhe. Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2015, hali ya usafirishaji bidhaa kwa upande wa Zanzibar ilishuka kwa asilimia 68.3 kutoka usafirishaji wa bidhaa wenye thamani ya TZS 133,591.7 milioni mwaka 2014 hadi kufikia TZS 42,407.0 milioni mwaka 2015.

Mhe. Naibu Spika, nchi ambazo Zanzibar ilifanya nazo biashara kwa mwaka 2015 ni pamoja na India, Comoro, Singapore, China, Vietnam, UAE, na Nchi za Umoja wa Ulaya. Nchi ya India imenunua bidhaa zenye thamani ya TZS 21,115.9 milioni sawa na asilimia 50 ya usafirishaji wote kwa mwaka 2015, ingawaje usafirishaji huo wa bidhaa kwenda India ulipungua kutoka TZS

63,539.7 milioni mwaka 2014 na kufikia kiwango cha TZS 21,115.9 milioni mwaka 2015.

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyoeleza hapo awali sababu ambazo zilipelekea usafirishaji wa bidhaa dunia kupungua, athari hizo hizo pia zimeikumba Zanzibar, kwa vile nayo inashiriki katika utekelezaji wa Sera za kibiashara za Kimataifa.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa Uagiziaji kwa kipindi cha mwaka 2015, Zanzibar iliagiza bidhaa zenye thamani ya TZS 156,941.1 milioni ikilinganishwa na uagiziaji wa TZS. 279,552.8 milioni mwaka 2014.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na hali hiyo ya mwenendo wa biashara ya usafirishaji na uagiziaji kutokuwa mzuri kwa kipindi cha mwaka 2015, urari wa biashara (Trade balance) ulipungua kutoka TZS 145,965.0 milioni kwa mwaka 2014 hadi kufikia TZS 114, 534.1 milioni mwaka 2015. Jadweli Nam 2 linafafanua zaidi hali ya usafirishaji na uagiziaji wa bidhaa kwa kipindi cha miaka mitano (2011 - 2015)

Jadweli Nam 2
Usafirishaji na Uagiziaji wa Bidhaa 2011 – 2015
(TZS Mil)

	2011	**2012**	**2013**	**2014**	**2015**
Uingizaji wa Bidhaa	164,187.10	271,273.10	208,051.90	279,552.80	156,941.10
Usafirishaji wa bidhaa	61,261.40	67,390.50	87,799.60	133,587.70	42,407.00
Kiasi cha Biashara (*Volume of Trade*)	**225,448.50**	**338,663.60**	**295,851.50**	**413,140.50**	**199,348.10**
Urari (*Trade* Balance)	**-102,925.70**	**-203,882.60**	**-120,252.30**	**-145,965.10**	**-114,534.10**

Chanzo: Mtakwimu Mkuu wa Serikali

Biashara Baina ya Zanzibar na Tanzania Bara

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa usafirishaji bidhaa kwenda Tanzania Bara, Zanzibar imesafirisha bidhaa zenye thamani ya TZS. 401,219.4 milioni mwaka 2015 ikilinganishwa na bidhaa zenye thamani ya TZS. 366,354.2 milioni mwaka 2014. Usafirishaji huo ulikuwa ni ongezeko la asilimia 8.69. Aidha, kwa upande wa Uagiziaji bidhaa kutoka Tanzania Bara, Zanzibar iliagiza bidhaa zenye thamani ya TZS. 95,397.3 milioni kwa mwaka 2015

ikilinganishwa na uagiziaji wa bidhaa zenye thamani ya TZS 69,794 milioni kwa mwaka 2014.

Kutokana na mwenendo huo, Mhe. Naibu Spika, urari wa biashara kati ya Zanzibar na Tanzania Bara uliendelea kuwa mzuri kutoka nakisi ya TZS 296,560.2 milioni ya mwaka 2014 hadi ziada ya TZS 305,822.1 milioni mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 3.02 kama inavyoonekana katika **Jadweli Nam 3**.

Mhe. Naibu Spika, Biashara baina ya Zanzibar na Tanzania Bara inahusisha bidhaa zinazozalishwa Zanzibar na kuuzwa katika soko la Tanzania Bara na bidhaa zinazoagizwa kutoka nje na kuhaulishwa kwenda Tanzania bara, kwa upande mmoja na bidhaa zinazotoka Tanzania bara kuja katika soko la Zanzibar kwa upande wa pili.

Jadweli Nam. 3

Usafirishaji kwenda na kutoka Tanzania Bara
TZS. (Mil)

Mwaka	**2011**	**2012**	**2013**	**2014**	**2015**
Kuja Zanzibar	114,435.90	98,871.60	82,906.20	69,794	95,397.3
Kwenda T.Bara	71,396.80	224,400.50	501,204.20	366,354.20	401,219.40
Urari wa Biashara	**-43,039.10**	**125,528.90**	**418,298.00**	**296,560.20**	**305,822.10**

Chanzo: Mtakwimu Mkuu wa Serikali ya Mainduzi, Zanzibar

Mwenendo wa Bei za Chakula Duniani

Mhe. Naibu Spika, mwenendo wa bei za chakula katika masoko ya dunia kwa mwaka 2014 ulikuwa wa utulivu ukilinganisha na mwaka 2015. Wastani wa bei ya sukari katika masoko ya dunia ulishuka kwa wastani wa asilimia 3.9 kwa mwaka huo wa 2015 kama inavyoonekana katika **Jadweli Nam 4** hapa chini.

Jadweli Nam. 4

Wastani wa Bei za chakula muhimu katika Soko la Dunia 2015
(USD/MT)

Bidhaa	2014	2015	Mabadiliko (%)
Mchele	404	455	12.6
Sukari	562	540	-3.9
Unga Ngano	253	445	75

Chanzo: www.indexmundi.com

Mwenendo wa Uagiziaji na Bei za Chakula katika Soko la Ndani

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa uagiziaji wa chakula hapa Zanzibar, hali ya uwepo wa chakula ilikuwa ya kuridhisha. kwa takwimu tulizonazo zinaonesha kuwa Jumla ya Tani 72,535 za mchele, tani 16,322.2 za sukari, na tani 29,472.2 za unga wa ngano zilizokuwepo kwa ajili ya matumizi ya soko la ndani hadi kufikia mwezi Machi, 2016. **Jadweli Nam. 5** linachambua hali ya uagiziaji chakula katika kipindi cha mwaka 2015/2016 .

Jadweli Nam 5

Wastani wa Uingizaji wa Chakula Muhimu
katika Soko la Zanzibar 2015/2016

	Mchele	Sukari	Unga wa Ngano	Jumla
Mahitaji ya Chakula	72,535	16,322.2	29,472.2	118,329
Matumizi	63,108	12,645	19,368	95,121
Bakaa	9,425	3,677.9	10,104.2	23,207

Chanzo: Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko,

Hata hivyo, Mhe. Naibu Spika, bei za chakula muhimu katika soko la Zanzibar ziliendelea kuwa na utulivu katika kipindi cha mwaka 2015/2016 kama inavyoonekana katika **Jadweli Nam 6**.

Jadweli Nam 6
Wastani wa Bei za Reja Reja za Chakula Muhimu
katika Soko la Zanzibar

(TZS/Kilo)

Bidhaa	Julai - Sept	Okt – Dis	Jan - Machi
Mchele	1,100 – 1,300	1200 – 1300	1200 – 1300
Sukari	1,300 – 1,400	1300 – 1400	1400 – 1500
Unga Ngano	1,200 – 1,300	1200 – 1300	1200 – 1300

Chanzo: Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko

Mwenendo wa Bei ya Karafuu na Mwani

Mhe. Naibu Spika, Wizara yangu imeendelea kufuatilia mwenendo wa bei za mazao ya mwani na karafuu ambayo huzalishwa na kusafirishwa na Zanzibar. Katika kipindi cha mwaka 2015, bei ya karafuu katika soko la dunia ilikuwa kati ya *USD* 7,000 hadi *USD* 8,200 kwa tani. Kwa upande wa soko la ndani, Serikali bado inaendelea kutoa asilimia 80 ya bei ya kuuzia karafuu nje kwa wakulima wa zao hilo. Kwa upande wa zao la mwani, bei katika soko la dunia imekuwa kati ya *USD* 0.45 hadi *USD* 0.75 kwa kilo moja. Aidha, bei ya zao hilo katika soko la ndani imekuwa ikiuzwa kati ya TZS 300 na TZS 1,000. Wizara inatafuta njia ya kudumu ya kushajiisha zao la mwani ili kuongeza kipato kwa wakulima wa mwani.

MAENDELEO YA VIWANDA

Mhe. Naibu Spika, Moja ya malengo makubwa ya Serikali katika kuanzisha viwanda hapa nchini ni kupunguza uagiziaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi, kuongeza usafirishaji wa bidhaa, kutumia malighafi za hapa nchini, kuongeza ajira pamoja na kuongeza mapato ya Serikali na hivyo kupunguza nakisi katika urari wa biashara.

Mhe. Naibu Spika, Hali ya uwepo wa viwanda unahitaji hatua za haraka kubadilisha mfumo uliopo wa kuwepo viwanda vingi vidogo vidogo kwa Zaidi ya asilimia 90 ya viwanda viliopo idadi ya 2050.vingi vyao vikiwemo kwenye mfumo usio rasmi hivyo vinakosa misaada mikubwa ikiwemo utaalam na mitaaji.

Mhe. Naibu Spika, Thamani ya uzalishaji viwandani kwa mwaka 2015/2016 kwa ujumla imeimarika ikilinganishwa na mwaka wa 2014/2015. Hali hiyo imetokana na kuimarika uzalishaji katika viwanda vitatu vikubwa vya Zanzibar ambavyo ni kiwanda cha maziwa cha *Azam Dairy Ltd* kilichopo Fumba, Kiwanda cha *Zanzibar Milling Corporation* kilichopo Mtoni na kiwanda cha Sukari Mahonda. Kiwanda cha maziwa cha Azam Dairy Ltd kimezalisha bidhaa za maziwa ujazo wa lita 3.6 milioni katika mwaka huu ukilinganisha na lita 0.36 milioni zilizozalishwa katika mwaka wa 2014/2015.

Kwa upande wa kiwanda cha *Zanzibar Milling Corporation* kimezalisha bidhaa zinazofikia uzito wa Tani 42,154 zenye thamani ya TZS. 33,000 milioni ikilinganishwa bidhaa zenye uzito wa tani 34,975 zenye thamani ya TZS 23,800 milioni katika mwaka 2014/15. Aidha, kiwanda cha Sukari Mahonda kimeanza uzalishaji wa majaribio tarehe 5 Machi 2016, ambapo kufikia mwisho wa mwezi huo kiwanda kilikwishazalisha tani 350 za sukari. Kiwanda hiki kinauwezo baada ya kufanyiwa ukarabati mkubwa kuzalishaji hadi tani 3.1 na kuongeza uhakika wa upatikanaji wa sukari ndani ya nchi.

Mhe. Naibu Spika, Aidha uzalishaji wa viwanda vidogo vidogo ulikuwa wa kuridhisha hasa kwa kuzingatia kuwa mwaka huo ulikuwa na pirika za uchaguzi. Viwanda vipya kumi vya kupigia matofali vilianzishwa katika sehemu mbalimbali za Zanzibar, na kiwanda cha kuchanganya majani ya chai *tea blending* kilianzishwa katika eneo la Mfenesi mazizi. Kadhalika, mchango wa sekta ya viwanda katika Pato la Taifa katika mwaka wa 2015 umefikia asilimia 19.8 kutoka asilimia 16.8 ya mwaka 2014. Mchango wa sekta ndogo ya uzalishaji *manufacturing* umefikia asilimia 8.0 kwa mwaka 2015 kutoka asilimia 6.4 ya mwaka 2014. Ifikapo mwaka 2020 mchango wa sekta ya viwanda unatarajia ufikie asilimia 12 na kuongeza ajira kwa asilimia 20.5.

UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA 2015 – 2016

Mhe. Naibu Spika, baada ya kutoa maelezo hayo ya utangulizi pamoja na mapitio ya hali ya biashara na viwanda, naomba sasa kufanya mapitio ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka 2015/2016.

Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016

Mhe. Naibu Spika, Kwa upande wa matumizi, Wizara ilitengewa jumla ya TZS 6,608.30 milioni kwa ajili ya kutekeleza programu zake kwa mwaka 2015 - 2016 . Kati ya fedha hizo TZS 2,360.60 milioni zilitengwa kwa Programu ya Utawala na Uendeshaji wa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko, TZS 891.37 milioni Programu ya Maendeleo ya Viwanda na Ujasiriamali, TZS

1,256.33 milioni Programu ya Maendeleo na Ukuzaji wa Biasharana TZS 2,100 milioni kwa Programu ya Viwango na Uthibiti Ubora wa bidhaa.

Mhe. Naibu Spika, Hadi kufikia Machi, 2016, Wizara iliingiziwa Jumla ya TZS 2,101.5 milioni, ambazo zilikuwa ni sawa na asilimia 37 ya fedha zilizopangwa kutumika kwa kipindi hicho ambacho ni sawa na asilimia 31.8 ya bajeti ya mwaka. Mchanganuo wa matumizi hayo kwa kila programu ulikuwa kama unavyoonekana katika **Jadweli Nam 7:**

Jedwali Nam 7 Maombi ya Fedha (TZS Mil)

Geresho (Code)	Programu	Makisio ya mwaka 2015/16	Makisio ya Miezi tisa (Julai - Machi)	Fedha zilizoingizwa miezi tisa (Julai - Machi)
211	**Utawala na Uendeshaji wa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko**			
21101	Utawala	1,562.90	1,261.50	1,093.40
21102	Mipango, Sera na Utafiti	442.57	378.3	109.2
21103	Ofisi Kuu Pemba	355.17	276.2	242.5
Jumla ndogo		**2,360.60**	**1,916.00**	**1,445.10**
212	**Maendeleo ya Viwanda na Ujasiriamali**			
21201	Ukuzaji wa Viwanda	191.02	142.9	4.1
21202	Maendeleo ya Ujasiriamali	700.35	604.2	
Jumla ndogo		**891.37**	**747.1**	**4.1**
213	**Maendeleo na Ukuzaji wa Biashara**			
21301	Ukuzaji wa Masoko na Usafirishaji bidhaa nje	423.93	306.5	41.7
21302	Ushindani wa kibiashara na Kumlinda Mtumiaji	142.36	122.4	11.4
21303	Biashara za ndani na Urahisishaji biashara	690.04	566	248.3
Jumla ndogo		**1,256.33**	**994.9**	311.4
214	**Viwango na Uthibiti Ubora wa bidhaa**			
21401	Uthibiti Viwango	2,100.00	1,953.20	340.9
Jumla ndogo		**2,100.00**	**1,953.20**	**340.9**
JUMLA KUU		**6,608.30**	**5,611.20**	**2,101.50**

Ukusanyaji wa Mapato

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2015/2016 Wizara yangu ilipangiwa lengo la kukusanya mapato ya TZS 139.28 milioni kutoka katika vianzio vyake mbali mbali. Hadi kufikia mwezi wa Machi, 2016 jumla ya TZS 41.87 milioni zilikusanywa na kuingizwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Kiasi hicho cha makusanyo ni sawa na asilimia 30.0 ya makadirio.

Mhe. Naibu Spika, Sababu zilizopelekea kutokufikiwa kwa kiwango ambacho kilipangwa kukusanywa ni pamoja na malipo ya kodi yaliyotangulizwa (Advance) katika kipindi cha mwaka 2015/2016 ya jumla ya TZS 36.96 milioni. Aidha, Wizara ilijipangia kukusanya jumla ya TZS 40.0 kutokana na Tamasha la Biashara ambalo hufanyika kila Januari. Tamasha hilo halikuweza kufanyika kutokana na hali ya kisiasa iliyokuwepo kwa kipindi hicho.

Utekelezaji wa Malengo ya Bajeti

Mhe. Naibu Spika, Kwa mwaka 2015/2016 Wizara ilijipangia kutekeleza Programu kuu nne (4), zilizogawika katika programu ndogo tisa (9). kama ifuatavyo:

1. Programu ya Utawala na Uendeshaji
2. Programu ya Maendeleo ya Viwanda na Ujasiriamali
3. Programu ya Ukuzaji na Uendelezaji Biashara
4. Programu ya Viwango na Uthibiti Ubora

Programu kuu ya Utawala na Uendeshaji wa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko

Mhe. Naibu Spika, Programu kuu ya Utawala na Uendeshaji wa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko inajumuisha Programu ndogo tatu ambazo ni Utawala na Uendeshaji wa Wizara; Programu ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti; na Programu ndogo ya Ofisi kuu Pemba. Utekelezaji wa kazi zilizopangwa katika kila program ndogo nilizozitaja ni kama ifuatavyo:

Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji wa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko

Mhe. Naibu Spika, Programu hii ndogo ya Utawala na Uendeshaji inasimamiwa na Idara ya Uendeshaji na Utumishi pamoja na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti. Kwa mwaka wa fedha 2015/2016 programu ndogo ya Utawala

na Uendeshaji wa Wizara ilikuwa na jukumu la kutoa huduma ya uimarishaji wa mazingira mazuri ya kufanyia kazi, utoaji wa huduma kwa Idara zote za Wizara, na Uratibu wa mikutano ya majadiliano. Program ndogo ya Utawala na Uendeshaji ilitekelezwa kama ifuatavyo:-

Uimarishaji wa Mazingira Mazuri ya Kufanyia Kazi

Mhe. Naibu Spika, Kwa madhumuni ya kuweka mazingira mazuri ya kufanya kazi wizara iliendelea kuwalipa wafanyakazi wake wote mishahara yao kama inavyostahiki, aidha Wizara iliwapatia wafanyakazi wake likizo zao na stahiki za likizo hizo, ambapo jumla ya wafanyakazi 29 walipatiwa likizo za kawaida, wafanyakazi 2 likizo bila malipo, wafanyakazi 13 likizo za dharura na wafanyakazi 2 likizo la uzazi. Aidha, Wizara imefanya ukarabati mkubwa wa jengo lake la zamani la Shirika la Magari liliopo Malindi kwa ajili ya matumizi ya ofisi ya Baraza la Usimamizi wa Utoaji wa Leseni. Hata hivyo, Wizara imeshindwa kuanza ujenzi wa jengo la ofisi kuu Pemba, na kufanya ukarabati wa majengo yake mengine, kutokana na uhaba wa fedha uliojitokeza.

Utoaji wa Huduma kwa Idara

Mhe.Naibu Spika, Katika kuitekeleza huduma hii, Wizara ilifanya tathmini ya mahitaji ya wafanyakazi kwa lengo la kuwa na idadi ya kutosha ya kuendesha shughuli za Wizara kwa ufanisi na tija. Kwa mwaka wa fedha 2015 - 2016 Wizara ilipanga kufanya Uajiri wa wafanyakazi wapya 17 katika fani za mizani na vipimo, sheria, uchumi, biashara na ujasiriamali. Napenda kuliarifu Baraza lako tukufu kwamba uajiri huo haukuweza kufanyika, na utafanyika katika mwaka huu wa fedha wa 2016/2017.

Mhe. Naibu Spika, kwa lengo la kuimarisha ufanisi katika utendaji kazi kwa kuwajengea uwezo wafanyakazi, Wizara iliendelea kutekeleza mpango wake wa mafunzo, ambapo jumla ya wafanyakazi 4 wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu katika fani za Sheria, Uongozi wa Biashara na Uchumi na wafanyakazi 8 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi katika masuala ya biashara na ujasiriamali katika nchi za India na China.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa manunuzi, Wizara kupitia mpango wake wa manunuzi (annual procurement plan) kwa madhumuni ya kusimamia vyema matumizi ya fedha za umma kwa mujibu wa sheria ya manunuzi, ilitangaza tenda saba (7) kwa manunuzi ya vifaa vya kuandikia, mafuta, kompyuta, samani na vifaa vya usafi, na matengenezo ya jengo la zamani la Shirika la magari kwa ajili ya matumizi ya ofisi mpya ya Baraza la usimamiaji wa Utoaji wa Leseni.

Uratibu wa mikutano ya majadiliano ya kibiashara.

Mhe. Naibu Spika, Katika kuendeleza ushiriki wa Viongozi wa Wizara katika Mikutano ya sekta ya Biashara na Viwanda kinchi, Kikanda na Kimataifa, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la mapinduzi iliweza kuratibu ushiriki wetu wa mikutano ya kisekta, iliyohusu majadiliano ya Utekelezaji wa Itifaki ya Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Programu Ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti

Mhe. Naibu Spika, Programu ndogo hii ya Mipango, Sera na Utafiti ilikuwa na jukumu la kutayarisha, kuchambua na kutathmini utekelezaji wa mipango na malengo maalum ya Wizara. Huduma ambazo zimesimamiwa na kutekelezwa na Programu hii ndogo ni Mapitio na Uandaaji wa sera za biashara na Viwanda; Utambuzi wa vikwazo katika kuongeza usafirishaji wa bidhaa nje; Uimarishaji wa mfumo wa ufuatiliaji na tathmini; Utayarishaji wa ripoti za utekelezaji wa bajeti; Uimarishaji wa uwezo wa wafanyakazi katika ukusanyaji taarifa na utumiaji wa teknolojia ya habari namawasiliano; Uimarishaji wa Mkakati wa mawasiliano; Ukondoeshaji wa masuala Mtambuka; na Uimarishaji wa Mazingira Bora ya Biashara.

Mhe. Naibu Spika, katika utekelezaji wa programu ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti, huduma ambazo nimezitaja hapo juu zilitekelezwa kama ifuatazo:-

Mapitio na Uandaaji wa Sera za Biashara na Viwanda

Mhe. Naibu Spika, katika kutekeleza huduma hii wizara yangu imeongezewa jukumu la Idara mpya ya Ushindani Halali wa Biashara *Fair Trade Department*, hivyo inaendelea na matayarisho ya kuandaa Sera ya Kumlinda Mtumiaji *Consumer Protection Policy* kwa lengo la kuweka mfumo ulioimara wa kumlinda mtumiaji kutokana na bidhaa zisizo na ubora.

Mhe. Naibu Spika, Shughuli nyengine ambayo imetekelezwa ndani ya huduma hii ni kufanya mapitio ya Sera ya Wafanyabiashara Wadogo wadogo na Kati ya mwaka 2006. Napenda kuliarifu Baraza lako tukufu kuwa Wizara yangu kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo ya Viwanda *NIDO* imekamilisha kufanya mapitio ya Sera hiyo na rasimu yake iko katika hatua za mwisho. Baada ya kukamilika kwa mapitio hayo, Wizara itaandika Sera mpya ya *SME* pamoja na Sheria yake ili kuweka misingi muhimu ya kuweza kuwasaidia na kuwakuza wajasiriamali pamoja na *SME* (viwanda vidogo vidogo na kati).

Utambuzi wa Vikwazo katika Kuongeza Usafirishaji wa Bidhaa Nje

Mhe. Naibu Spika, wizara ilifanya utafiti wa majaribio *Pilot study* wa kubaini vikwazo vya kibiashara visivyo vya ushuru *NTBs* vinavyowakabili wafanyabiashara kati ya Zanzibar na Tanzania Bara.Katika utafiti huo Ilibainika kuwa miongoni mwa vikwazo ni vya kitaalamu(*Technical Barriers*) vikiwemo ubora na viwango vya bidhaa, uwekaji wa alama (*Labelling and Packaging)*, uchunguzi na uthibiti wa bidhaa *Testing and Cerification* pamoja na taratibu za kiforodha ambazo zinapelekea kupoteza muda mwingi na kuongeza gharama za ufanyaji biashara. Napenda kuliarifu baraza lako tukufu kuwa wizara itaendelea na kufanya utafiti wa kina kuhusiana na masuala hayo kwa ajili ya kuchukua hatua za kutatua vikwazo hivyo na kuweza kuongeza uuzaji wa bidhaa zetu bara.

Uimarishaji wa Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini

Mhe. Naibu Spika, katika kutekeleza huduma hii, Wizara ilifanya shughuli ya kuandaa taarifa za utekelezaji za miradi ambayo inasimamiwa na Wizara. miradi ambayo ilifanyiwa ufuatiliaji ni pamoja na mradi wa Mkakati wa maendeleo ya karafuu na ule wa ujenzi wa maabara pamoja na ofisi za Taasisi ya Viwango ya Zanzibar *ZBS*.

Utayarishaji wa Ripoti za Utekelezaji wa Bajeti

Mhe. Naibu Spika, Kazi ya kuandaa taarifa za utekelezaji pamoja na bajeti ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa kipindi cha mwaka 2016/2017 imefanyika.

Uimarishaji wa Uwezo wa Wafanyakazi katika Ukusanyaji Taarifa na Utumiaji wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano

Mhe. Naibu Spika, Wizara imempatia mfanyakazi mmoja mafunzo ya muda mfupi nchini china yanayohusiana na ukusanyaji, uchambuzi na uhifadhi wa takwimu ambayo yatasaidia katika kuimarisha sekta ya biashara nchini.

Uimarishaji wa Mkakati wa Mawasiliano.

Mhe. Naibu Spika, Wizara ina jukumu la kutoa taarifa zinazohusiana na sekta ya biashara kwa wadau ambazo zitapelekea kuchambua mwenendo wa biashara nchini. Aidha, Wizara inaendelea na juhudi za kumalizia uandaaji wa tovuti ili

kutoa taarifa hizo muhimu kwa wananchi ikiwemo kutoa taarifa za hali ya uwepo wa vyakula nchini na bei.

Ukondoeshaji wa Masuala Mtambuka

Mhe. Naibu Spika, shughuli iliyotekelezwa katika huduma hii ni kushiriki katika semina ya kujenga uwelewa juu ya maambukizi ya ukimwi kwa vijana iliyo endeshwa na Tume ya *UKIMWI* ya Zanziabr. Lengo la semina hiyo ilikuwa ni kutathmini hali ya maambukizi ya *UKIMWI* kwa vijana pamoja na kupendekeza hatua za kuchukuliwa ili kukabiliana na hali hiyo.

Programu Ndogo ya Ofisi Kuu Pemba

Mhe. Naibu Spika, Programu ndogo ya Ofisi Kuu Pemba ina jukumu la kutekeleza na kusimamia shughuli zote za Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa upande wa kisiwa cha Pemba. Huduma zilizopangwa kutolewa na Programu hii ndogo ni utoaji wa huduma na ununuzi wa vifaa; Uimarishaji wa mazingira ya kazi; Ukondoeshaji masuala mtambuka; Ukuzaji wa maendeleo ya wajasiriamali; na Uhakiki na Ukaguzi wa vifaa vya mezani na vipimo, maduka, mabekari,maghala na "*supermarket*".

Mhe. Naibu Spika, Utekelezaji wa program ndogo ya ofisi kuu Pemba ulikuwa kama ifuatavyo:-

Utowaji wa Huduma na Ununuzi wa Vifaa

Mhe. Naibu Spika, Katika kutekeleza huduma hii, Wizara kupitia Afisi Kuu Pemba ilifanya ununuzi wa vifaa vya kufanyia kazi, Ununuzi wa huduma za umeme, maji na mawasiliano, matengenezo ya magari, ununuzi wa mafuta na kutoa huduma ya usafiri kwa maafisa wa wizara kwa ajili ya ufuatiliaji wa kazi mbali mbali za wizara.

Uimarishaji wa Mazingira ya Kazi

Mhe. Naibu Spika, shughuli ambazo zilifanyika katika huduma hii ni kuwapatia wafanyakazi wawili (2) mafunzo ya muda mfupi na mfanyakazi mmoja (1) mafunzo ya muda mrefu katika ngazi ya shahada ya pili yanayohusiana na masuala ya uchumi, biashara na ujasiriamali. Aidha, Wizara kupitia Ofisi kuu Pemba iliwapatia likizo wafanyakazi kumi na tano (15) pamoja na kuwapatia wafanyakazi malipo ya posho ya baada ya saa za kazi kwa shughuli zilizofanyika baada ya muda wa kazi.

Ukondoeshaji wa Masuala Mtambuka

Mhe. Naibu Spika, katika kutekeleza huduma hii, Wizara ilitoa mafunzo kwa njia ya semina kwa wafanyakazi wote kuhusu Sera ya Taifa ya Jinsia.

Ukuzaji wa Maendeleo ya Wajasiriamali

Mhe. Naibu Spika, Kwa lengo la kuwaendeleza wajasiriamali wadogo wadogo na wa kati *SMES*, Wizara ilifanya ukaguzi wa vikundi 80 vya wajasiriamali katika Wilaya zote za Pemba. Ukaguzi huo uliendana na shughuli ya kutoa ushauri wa njia bora za kuimarisha miradi hiyo ya wajasiriamali. Miradi iliyotembelewa ni pamoja na miradi ya chumvi, Vikundi vya Ufugaji nyuki, Watengenezaji sabuni, pamoja na Vikundi vya Wajasiriamali wanao tengeneza kazi za mikono na pia watengenezaji wa mazao ya viungo na matunda yaliyosindikwa au kukaushwa.

Uhakiki na Ukaguzi wa Vifaa vya Mezani na Vipimo, Maduka, mabekari, maghala na *Supermarket* na Vituo vya *petrol*

Mhe. Naibu Spika**,** kwa lengo la kuhakikisha haki za mtumiaji zinalindwa, Wizara ilifanya ukaguzi wa mizani na vipimo kwa mujibu wa Sheria ya Mezani na Vipimo Nam 1 ya mwaka 2004. Katika ukaguzi huo, jumla ya mizani 1,075, mita ndogo za mafuta 36, mita 3 kubwa za kutolea mafuta katika bandari ya Wesha, magari 8 ya kubebea mafuta zimekaguliwa katika shehia mbali mbali za wilaya zote za Pemba.

Aidha, Wizara ilifanya ukaguzi wa maduka, maghala na mabekari kwa mujibu wa Sheria ya Ushindani halali wa kibiashara na kumlinda Mtumiaji Nam 2 ya mwaka 1995. Katika ukaguzi huo jumla ya maduka 1,500, maghala 18 na bekari 25 zimekaguliwa. Kadhalika, tani 72.2 za bidhaa mbali mbali zenye thamani ya TZS 112,344 milioni ziligundulika kutofaa kutumiwa na binaadam na hivyo ziliangamizwa kwa mujibu wa Sheria iliopo.

Programu Kuu ya Maendeleo ya Viwanda na Ujasiriamali

Mhe. Naibu Spika**,** katika Mkakati wa Mkuza III na Dira ya 2020, Ilani ya Uchaguzi ya CCM kwa mwaka 2015, maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika hotuba yake elekezi aliyoitoa alipofungua Baraza la Wawakilishi la tisa, suala la uendelezaji wa viwanda na hususan ujasiriamali umetiliwa mkazo ili wananchi wetu hasa wanawake na vijana wawezeshwe kiuchumi. Wengi wa wajasiriamali wa Zanzibar wamo kwenye mfumo usio rasmi katika sekta mbali mbali.

Mhe. Naibu Spika, maendeleo ya viwanda ndio msingi mkuu wa maendeleo ya nchi. Mikakati ya uchumi na mpango wa maendeleo wa mwaka 2016/2017 imeipa kipaumbele program ya kutayarisha sera na mkakati wa kuendeleza viwanda. Fedha zimetengwa kwa ajili ya kuanza kutayarisha mpango mkakati na Sheria ya Maendeleo ya Viwanda itakayoelezea sekta zitakazopewa kipaumbele pamoja na kuweka muda wa utekelezaji na kutoa vivutio maalum kwa wawekezaji katika sekta hizo. Pia kuangalia uwezekano ufufuaji wa viwanda vilivyo binafsishwa na kuvifufua kwa misingi ya kutoa ajira na kuchangia Pato la Taifa.Wizara yangu itashirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Viwanda *(United Nation Industrial Development Organization – UNIDO)* kwa kutengeneza sera mpya ya viwanda.

Mhe. Naibu Spika**,** Taarifa za tafiti mbali mbali zilizotayarishwa awali zikiwemo Mkakati wa Uuzaji bidhaa Nje wa mwaka 2009 *(National Export Strategy 2009),* Mkakati wa Maendeleo ya Maeneo Tengefu ya Kiuchumi *(Special Economic Zones),* Sera ya viwanda vidogo vidogo ya mwaka 2006 zitafanyiwa mapitio ili tuweze kuweka mkakati mpya utakaoangalia hali halisi na uwezo wa ndani na mashirikiano na sekta binafsi kwa kuziunganisha sera ziliopo kama vile maeneo huru na mikakati maalum ya kitaifa.

Mhe. Naibu Spika**,** kwa mwaka wa fedha 2015/2016, program kuu ya Maendeleo ya Viwanda na Ujasiriamali ambayo utekelezaji wake inasimamiwa na idara ya viwanda na maendeleo ya ujasiriamali pamoja na idara ya mipango, sera na utafiti inajumuisha Programu ndogo mbili zifuatazo:-

Programu ndogo ya Ukuzaji Viwanda

Mhe. Naibu Spika**,** Programu ndogo ya Ukuzaji Viwanda ina jukumu la kutoa huduma za Uimarishaji wa teknolojia ya uzalishaji kwa wazalishaji wadogo wadogo, Ukuzaji wa Sekta ya Viwanda, Uimarishaji Mazingira mazuri kwa ukuaji wa Sekta ya Viwanda na kuongeza thamani na Mradi wa Kuimarisha Mazingira Bora ya Biashara. Utekelezaji wa program ndogo ya Ukuzaji Viwanda ulikuwa kama ufuatavyo:-

Uimarishaji wa Teknolojia ya Uzalishaji kwa Wazalishaji Wadogo Wadogo

Mhe. Naibu Spika, Moja ya changamoto zilizopo kwa wazalishaji wadogo wadogo ni tatizo la utumiaji wa tekhnolojia za kisasa ya kuongeza ubora wa bidhaa, urahisi wa masoko na vile vile bei. Katika utafiti uliofanywa na Wizara katika changamoto ya kutoweza kutumia teknolojia mfano ni wa sekta ya

uzalishaji wa chumvi ndio unaotupa changamoto kubwa inayohitaji hatua za haraka. Utafiti umeonyesha kuwepo kwa soko la uhakika la chumvi katika nchi za Afrika ya Mashariki ikiwemo Rwanda pindipo ikiwezekana kutumia teknolojia ya kisasa katika uzalishaji wake, kuifanya iwe ya unga na kuitia maadini joto ya *iodine* ili iandane na matakwa ya Shirika la Afya la Kimataifa *(World Health Organization – WHO).*

Katika kutekeleza huduma hii, Wizara ilifanya Maandalizi ya mikutano ya wadau wa chumvi kupitia Jumuiya ya wazalishaji Chumvi. Lengo la mikutano hiyo ni kuwafahamisha wanaushirika wa *AZASPO (Association of Zanzibar Salt Processing Organisation)* juu ya matokeo ya utafiti na haja ya kubadilisha mfumo wa Jumuiya hiyo ili iweze kujiendesha kibiashara. Kwa bahati mbaya kazi hiyo haikufanyika kutokana na ukosefu wa fedha, na imepangwa kufanyika katika bajeti ya mwaka 2016/2017.

Ukuzaji wa Sekta ya Viwanda

Mhe. Naibu Spika, Hatua zilizofikiwa kwa sasa ni kutayarisha Dhana ya awali (*Concept note)* ya kazi ya utayarishaji wa Mkakati wa Maendeleo ya Viwanda. Aidha wizara inaendelea na ukusanyaji wa takwimu za uchumi na za kisekta ikiangalia uzalishaji wa malighafi, soko na masuala mengine muhimu kwa ajili ya kukamilisha kazi ya kuandaa Mkakati wa Maendeleo ya Viwanda.

Programu ndogo ya Maendeleo ya Ujasiriamali

Mhe. Naibu Spika**,** Programu ndogo ya Maendeleo ya Ujasiriamali ina jukumu la kutoa huduma za ukuzaji wa Ujasiriamali na Ushindani, usaidizi wa kuanzisha biashara kwa Wajasiriamali, Kurasimisha biashara na mali za wafanyabiashara wadogo wadogo, mradi wa Kuimarisha Mazingira Bora ya Biashara pamoja na Uimarishaji wa Maendeleo ya Sekta Binafsi. Utekelezaji wa program ndogo ya Maendeleo ya Ujasiriamali ilikuwa kama ifuatavyo:-

Ukuzaji wa Ujasiriamali na Ushindani

Mhe. Naibu Spika, katika kukuza ujasirimali na kukabili ushindani Wizara imetoa usaidizi na ushauri wa kitaalamu wa kutambua teknolojia mwafaka kwa mradi wa kusarifu ndimu wa Chwaka. Aidha katika kipindi hicho jumla ya vikundi 40 vya wajasiriamali wazalishaji vilitembelewa. Kadhalika, katika hatua za kuandaa muongozo wa mafunzo kwa wajasiriamali, Wizara imekamilisha ukusanyaji wa mitaala ya mafunzo ya ujasiriammali kutoka taasisi tano pamoja na kuunda kikosi kazi cha kuchambua na kuianisha mitaala

hiyo. Hatua inayofuata sasa nikusubiri ripoti ya kikosi kazi hicho ambayo itatoa mapendekezo makhsusi katika uandaaji wa muongozo huo pamoja na kuangalia uwezekano wa kuanzisha chombo cha kuwaendeleza wajasiriamali na viwanda vidogo vidogo na kati.

Mhe. Naibu Spika, baada ya taarifa nilizozieleza hali isiyoridhisha ya wajasiriamali, Wizara yangu kwa kushirikiana na *UNIDO* imefanya mapitio ya Sera ya Viwanda vidogo vidogo ya mwaka 2006 kwa lengo la kuweka mikakati ya kuimarisha sekta ndogo ya ujasiriamali. Taarifa ya awali itapatikana karibuni na itawezesha kupeleka serikalini sera mpya ya viwanda vidogo vidogo, na vyakati ikiwemo na chombo cha kusimamia na kushajiisha ujasiriamali. Aidha, Wizara ilipanga kufanya sensa ya wajasiriamali wachanga, wadogo na wakati na tayari imekamilisha kuandaa madodoso kwa hatua ya awali ambayo inasambazwa kwa wajasiriamali kwa ajili ya kukusanya takwimu.

Aidha, kwa upande wa kuratibu wafanyabiashara wadogo na wakati, Wizara ilipanga kufanya mikutano ya Kamati ya Mashauriano ya SME kila robo mwaka. Hata hivyo, kutokana na kukosekana kwa fedha, mikutano hiyo haikuweza kufanyika.

Usaidizi wa Kuanzisha Biashara kwa Wajasiriamali

Mhe. Naibu Spika, Kwa upande wa kutoa usaidizi wa kuanzisha biashara kwa wajasiriamali, Wizara inajukumu la kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Kurasimisha Biashara na Rasilimali za wanyonge Tanzania kwa upande wa Zanzibar. Kwa mwaka wa fedha 2015/2016, Wizara ilifanya ufuatiliaji wa wafanyabiashara 50 kwa upande wa Unguja na 50 Pemba ambao walipatiwa mafunzo ya namna ya kurasimisha biashara zao, na ufanyaji wa biashara. Aidha Jumla ya wafanyabiashara 80 wameweza kurasimisha biashara zao.

Mhe. Naibu Spika, Wizara katika kipindi cha 2015/2016 kwa kushirikiana na Jumuiya ya Wafanyabiashara, wenye Viwanda na Wakulima (*ZNCCIA*) imeendelea kuhamasisha wafanyabiashara kuhusu umuhimu wa matumizi ya alama za mistari (*Barcodes*) ili waweze kuingiza biashara zao katika masoko ya ndani na nje. Uhamasishwaji huo ulifanyika kwa njia za mikutano, kuwahamasisha wafanyabiashara ambao wanahitaji kushiriki katika maonesho ya biashara ambapo *barcodes* 419 zimeetolewa kwa makampuni 35 kwa kipindi hiki na kuwapa uwezo Zanzibar *National Chamber of Commerce Industry and Agriculture*. Yaani Jumuiya ya Wafanyabishara wenye viwanda na wakulima wa Zanzibar.

Programu Kuu ya Ukuzaji na Uendelezaji wa Biashara

Mhe. Naibu Spika, Programu kuu ya Ukuzaji na Uendelezaji wa Biashara inajumuisha Programu ndogo tatu ambazo ni Ukuzaji wa Masoko na Usafirishaji; Ushindani wa Kibiashara na kumlinda Mtumiaji; pamoja na Urahisishaji wa Biashara na Ukuzaji biashara za ndani. Utekelezaji wa kazi zilizopangwa katika kila program ndogo nilizozitaja ni kama ifuatavyo:

Programu ndogo ya Ukuzaji wa Masoko na Usafirishaji

Mhe. Naibu Spika, Programu ndogo Ukuzaji wa Masoko na Usafirishaji inasimamiwa na Idara ya Biashara na Masoko pamoja na Mipango Sera na Utafiti. Huduma ambazo zimesimamiwa na kutekelezwa na Programu hii ndogo ni Fursa za Masoko na Urahisishaji biashara; Mradi wa Kujenga uwezo wa Kukondoesha Biashara; Uratibu wa Mkakati wa Usafirishaji bidhaa nje; na Mradi wa Mkakati wa Maendeleo ya Karafuu.

Mhe. Naibu Spika, huduma hizo nilizozitaja hapo juu zilitekelezwa kama ifuatazo:-

Fursa za Masoko na Urahisishaji Biashara

Mhe. Naibu Spika, Wizara itafanya mapitio ya hali ya masoko kwa bidhaa zetu na kuangalia changamoto zilizopo.shughuli mbali mbali za kupanuwa masoko ya bidhaa za Zanzibar na fursa ziliopo zitachunguzwa ilituweze kuingia katika masoko ya kanda za Afrika za kiuchumi ikiwemo Afrika ya Mashariki SADC na nchi za nje zikiwemo nchi za Asia ya mbali nchi za Ghuba ikiwemo UAE, Oman, Kuwait, Iran, nk.

Mhe. Naibu Spika, Wizara iliratibu ushiriki wa Zanzibar katika maonesho ya saba saba ya 39 ya kimataifa ya biashara yaliyofanyika huko Dar e s salaam mwezi wa Julai, 2015 katika juhudi ya kukuza soko za bidhaa za Zanzibar.Wajasiriamali 27 na taasisi 2 za Kiserikali ziliweza kushiriki katika maonesho hayo ambao wamefanikiwa kuuza bidhaa zao na kupata masoko endelevu ya bidhaa zao. Wafanyabiashara walioshiriki katika maonesho hayo ni pamoja na watengezaji wa bidhaa za viungo (*spices*), sabuni za viungo (*spices*), kazi za mikono, dawa za asili, samani, bidhaa za vyakula vya kusindika kama achari, na majani ya chai na kadhalika.

Mhe. Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TANTRADE) iliratibu ushiriki wa maonesho ya *Expo Milan* yaliofanyika nchini Italia Mwezi Mei hadi Oktoba 2015 na jumla ya

wajasiriamali wawili wa kazi za mikono na uchoraji na wauzaji wa mazao ya viungo (*spices*) kutoka Zanzibar na Shirika la Biashara la Taifa (*ZSTC*) waliweza kushiriki katika maonesho hayo.

Aidha, wajasiriamali walipata fursa ya kushiriki katika mashauriano ya kibiashara (B2B) ambayo yalipelekea fursa ya kupata kushiriki katika maonesho mengine madogo hapo nchini Italia na pia kuwafungulia fursa ya kushiriki katika maonesho mengine ambayo yanatarajiwa kufanyika nchini Uturuki mwezi Mei hadi Oktoba, 2016.

Zaidi ya hayo, maonesho ya *Expo* yalitayarishiwa siku maalum ya Tanzania ambayo ilihudhuriwa na ujumbe kutoka Tanzania ambao uliongozwa na Makamo wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar kwa niaba ya Makamo wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa Tamasha la Biashara la Zanzibar linalofanyika kila mwanzo wa mwezi wa Januari kama sehemu ya kuadhimisha Sherehe za Mapinduzi, napenda kuliarifu Baraza lako kuwa Tamasha hilo halikuweza kufanyika kutokana na hali ya kisiasa iliyokuwepo katika kipindi hicho. Aidha, katika hatua za kulifanya Tamasha hilo liwe endelevu kwa lengo la kuwasaidia wajasiriamali wetu, Wizara yangu imetenga fedha kwa ajili ya kununua magazebo kwa maonesho yatakayo andaliwa kwa mwaka 2016/2017.

Uratibu wa Mkakati wa Usafirishaji bidhaa Nje

Mhe. Naibu Spika, Kwa lengo la kuongeza usafirishaji bidhaa nje Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji ya Tanzania Bara wanaendelea na kazi ya kufanyia mapitio Mkakati wa Usafirishaji bidhaa Nje (*NES*). Mapitio hayo yanafanyika kwa ufadhili wa Benki ya Dunia.

Mradi wa Mkakati wa Maendeleo ya Karafuu

Mhe. Naibu Spika, Karafuu ni zao muhimu sana kwa maendeleo ya Zanzibar. Wizara inaendelea kuifanyia kazi karafuu ya Zanzibar kwa kuisajili na kuweza kuipatia hati miliki. Wizara yangu kwa kushirikiana na Wataalamu kutoka Shirika la umoja wa Mataifa la Hati Miliki Duniani *(World Intellectual Property Organisation – WIPO)* iliandaa makala maalum ya karafuu za Zanzibar kwa ajili ya kuingiza katika shughuli ya utambuzi wa karafuu ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, itakumbukwa kuwa Baraza lako lilipitisha Sheria ya Maendeleo ya Karafuu Nam 2 ya mwaka 2014 ambayo ilianzisha Mfuko wa Maendeleo ya Karafuu. Napenda kuliarifu Baraza lako kuwa Mfuko huo umezinduliwa rasmi na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi mwezi wa Agosti 2015, huko kisiwani Pemba. Shughuli za mfuko zinaendelea vizuri na unachangia katika kuwasaidia wakulima wa karafuu.

Mradi wa Kujenga Uwezo wa Kukondoesha Biashara

Mhe. Naibu Spika, katika kutekeleza huduma hii Wizara yangu ilitafuta Mshauri Muelekezi kwa lengo la kuwapatia mafunzo wajasiriamali 50 juu ya kuzitambua fursa za biashara ziliopo.

Programu Ndogo ya Ushindani wa Kibiashara na kumlinda Mtumiaji

Mhe. Naibu Spika, Programu ndogo ya Ushindani wa Kibiashara na kumlinda Mtumiaji ina jukumu la kutoa huduma za ukaguzi na uhakiki wa vifaa; mizani na vipimo; ukaguzi wa Maduka ya Sonara; ukaguzi wa biashara na maghala; ushajihishaji na utoaji wa elimu kwa watumiaji; na uimarishaji wa mazingira ya kazi. Huduma hizo zilitekelezwa kama ifuatazo:-

Ukaguzi na Uhakiki wa Vifaa, Mizani na Vipimo

Mhe. Naibu Spika, Wizara ina jukumu la kufanya ukaguzi wa mizani, vipimo, vituo vya mafuta, magari ya mafuta, matangi ya mafuta, pampu za kuuzia mafuta na mita kubwa za mafuta (Depo). Kwa mwaka wa fedha 2015/2016 wizara ilifanya ukaguzi kama inavyoonekana katika Jedwali Nam 8 la hapo chini.

Jadweli Nam 8

Huduma ya Ukaguzi

a ukaguzi	**Lengo 2015 - 2016**			**Utekelezaji**			
	Unguja	**Pemba**	**Jumla**	**Unguja**	**Pemba**	**Jumla**	**Asilimi**
i	2,500	1,500	**4,000**	1,937	1,075	3,012	**75**
vya mafuta	56	12	**68**	56	12	68	**100**
za kuuzia mafuta	169	36	**205**	216	36	252	**123**
gi ya kuuzia mafuta	56	-	**56**	21	-	21	**38**
i ya kusambaza mafuta	12	8	**20**	12	8	20	**100**
a mafuta(Depo)	9	3	**12**	9	3	12	**100**

Chanzo: Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko

Aidha, Wizara imekamilisha kufanya mapitio ya kanuni za Sheria ya mizani na vipimo ya mwaka 2004 ambazo zilionekana kuwa zina mapungufu na kukwaza utekelezaji sahihi wa sheria hiyo. Kanuni hizo tayari zimeshawasilishwa kwa ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuweza kupitishwa na kutumika rasmi.

Ukaguzi wa Maduka ya Sonara

Mhe. Naibu Spika, katika kutekeleza lengo la kumlinda mtumiaji na kuweka ushindani halali wa kibiashara, wizara ilifanya utafiti mdogo kwa lengo la kutambua maduka ya vito vya thamani nchini. Aidha, jumla ya maduka ya sonara 21 yametambuliwa kwa upande wa unguja**.**

Ukaguzi wa Biashara na Maghala

Mhe. Naibu Spika, kwa madhumuni ya kusimamia mwenendo wa biashara na kumlinda mtumiaji wizara imefanya ukaguzi wa maduka, maghala, bekari na supermarket ili kubaini ubora wake pamoja na bei za bidhaa hizo kama inavyoonekana katika Jadweli Nam **9** hapo chini.

Jadweli Nam 9
Huduma za Ukaguzi

Eneo la ukaguzi	Lengo 2015 - 2016			Utekelezaji			
	Unguja	**Pemba**	**Jumla**	**Unguja**	**Pemba**	**Jumla**	**Asilimia**
Maduka	3000	1300	**4300**	2680	1500	**4,180**	**97.2**
Maghala	150	18	**168**	161	15	**176**	**104.8**
Bekari	20	25	**45**	20	25	**45**	**100**
Supermarket	6	-	**6**	6	-	**6**	**100**

Chanzo: Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko

Mhe. Naibu Spika, Katika ukaguzi huo, uliofanyika bidhaa mbali mbali zenye thamani ya TZS 16.5 milioni zilipatikana zikiwa zimepitwa na muda wake wa matumizi na zilikamatwa na kuondolewa madukani na zikaangamizwa. Bidhaa zilizokamatwa ni pamoja na vyakula vya makopo, taulo za watoto na watu wazima, magodoro, nguo za ndani, juice, dawa za kuulia mbu na bidhaa nyengine za matumizi ya majumbani.

Programu ndogo ya Urahisishaji wa Biashara na Ukuzaji Biashara za Ndani

Mhe. Naibu Spika, Kwa mwaka wa fedha 2015/2016 Baraza la kusimamia mfumo wa Utoaji Leseni, Baraza la Taifa la Biashara na Idara ya Biashara na

Ukuzaji masoko zilipangiwa kutekeleza huduma katika program ndogo ya uendeshaji biashara na ukuzaji biashara za ndani *(Trade Development and Promotion).*

Mhe. Naibu Spika, Programu ndogo ya Urahisishaji wa Biashara na Ukuzaji biashara za ndani ina jukumu la kutoa huduma za Uwekaji wa taratibu za utoaji na Udhibiti wa Leseni; Utoaji wa Huduma za Utawala na Uendeshaji wa Baraza la Leseni; Ushauri na Uhamasishaji kwa Wadau; Uimarishaji wa mazingira ya kazi; Utekelezaji wa Sheria ya Biashara ya Zanzibar Na.11 ya mwaka 2013; Majadiliano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi; Kusimamia Utawala na uendeshaji wa Baraza la Taifa la Biashara; na Mradi wa Kuimarisha Mazingira Bora ya Biashara.

Mhe. Naibu Spika, huduma hizo nilizozitaja hapo juu zilitekelezwa kama ifuatazo:-

Uwekaji wa Taratibu za Utoaji na Udhibiti wa Leseni

Mhe. Naibu Spika, katika kutekeleza huduma hii, Baraza limeandaa Kanuni (*regulations*) kwa ajili ya utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa utoaji wa leseni ya mwaka 2013. Aidha, mambo mengine yaliyotekelezwa ni pamoja na kuorodhesha Mamlaka za Utoaji Leseni, vibali au ruhusa za kuendesha biashara na kutayarisha vigezo na kuweka misingi, utaratibu pamoja na mfumo wa aina moja kwa ajli ya utoaji wa leseni, vibali au ruhusa nyingine za kuendesha biashara nia ikiwa kuingia katika utaratibu wa kielektroniki ili kurahisisha upataji wa leseni na kuzuia ukwepaji wa kodi na tozo zinazohusika.

Utoaji wa Huduma za Utawala na Uendeshaji wa Baraza la Leseni

Mhe. Naibu Spika, katika kutekeleza huduma hii Baraza limeandaa mapendekezo ya muundo wa Baraza pamoja na kuanisha majukumu ya kazi kwa kila Idara na Sehemu za Idara za Baraza hilo. Aidha, Sambamba na hilo, Baraza limeshaandaa mapendekezo ya awali ya wafanyakazi wake. Vilevile Baraza limeandaa rasimu ya Mpango Mkakati wa Baraza wa miaka mitano.

a. Ushauri na Uhamasishaji kwa Wadau

Mhe. Naibu Spika, katika kutekeleza huduma hii Baraza limetoa mafunzo kwa mamlaka zinazotoa leseni pamoja na wadau wengine wanaohusika juu ya matakwa ya sheria mpya ya kusimamia mfumo wa utoaji leseni.

b. Uimarishaji wa Mazingira ya Kazi

Mhe. Naibu Spika, katika kutekeleza huduma hii Baraza limeweza kufanya matengenezo makubwa ya jengo la ofisi yake katikia eneo la Malindi. Aidha, wafanyakazi wote walilipwa mishahara yao kwa wakati.

c. Utekelezaji wa Sheria ya Biashara ya Zanzibar Nam.11 ya mwaka 2013

Mhe. Naibu Spika, wizara imetayarisha mpango kazi wa kutoa elimu kwa jamii kuhusu masuala ya sheria za biashara. Mpango huo ulihusisha kutoa elimu kwa wajasiriamali ambao hupewa mafunzo ya biashara. Elimu hiyo ilitolewa kwa wafanyabiashara wa makontena yaliopo Darajani ili kuweza kutoa uelewa zaidi wa sheria hii. Aidha, wizara ilipanga kufanya vikao vya Kamati ya ushauri ambayo imeanzishwa katika Sheria ya Biashara, vikao hivyo bado havijafanyika kwa vile kamati hiyo ya ushauri haijaundwa.

d. Majadiliano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi

Mhe. Naibu Spika, serikali imekuwa na kawaida ya kufanya majadiliano baina ya sekta ya umma na sekta binafsi kwa madhumuni ya kuelewa matatizo yanayoikabili sekta hiyo na kuyatafutia ufumbuzi. Hata hivyo, mkutano wa majadiliano baina ya serikali na sekta binafsi kwa mwaka wa fedha 2015/2016 haukuweza kufanyika kutokana na hali ya kisiasa.

e. Kusimamia Utawala na Uendeshaji wa Baraza la Taifa la Biashara

Mhe. Naibu Spika, Baraza la Taifa la Biashara ni chombo muhimu katika kukuza biashara. Wizara imeendelea kusimamia shughuli mbali mbali za uendeshaji wa Baraza la Taifa la Biashara pamoja na kutoa huduma muhimu za kuendeshea Ofisi ya Baraza hilo.

f. Mradi wa Kuimarisha Mazingira Bora ya Biashara

Mhe. Naibu Spika, katika kutekeleza mradi huu katika *program* ndogo, wizara ilipanga kutekeleza sheria ya usimamizi wa mfumo wa utoaji wa leseni, kwa mwaka wa fedha 2015/2016, wizara imefanya matengenezo makubwa jengo lake lililokuwa Ofisi ya Shirika la Magari pamoja na kununua samani za ofisi.

A. Programu kuu ya Viwango na Tathmini ya Ubora

Mhe. Naibu Spika, programu kuu ya viwango na tathmini ya ubora inajumuisha programu moja ambayo ni viwango na udhibiti wa ubora. Utekelezaji wa huduma zilizopangwa katika programu ndogo niliyoitaja ni kama ifuatavyo:-

Programu Ndogo ya Viwango na Udhibiti wa Ubora

Mhe. Naibu Spika, Programu ndogo ya Viwango na Udhibiti wa Ubora inasimamiwa na Taasisi ya Viwango ya Zanzibar (*ZBS*) na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti. Kwa mwaka wa fedha 2015/2016 programu ndogo ya Viwango na Udhibiti wa Ubora ilikuwa na jukumu la kutoa huduma ya Uandaaji na Ukuzaji wa Viwango, Huduma ya Tathmini ya Ubora wa Bidhaa, Utoaji wa huduma za Utawala na Uendeshaji wa Taasisi na Mradi wa Kuimarisha Taasisi ya Viwango Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, utekelezaji wa Programu Ndogo ya Viwango na Udhibiti wa Ubora ulikuwa kama ifuatavyo:-

a. Uandaaji na Ukuzaji wa Viwango

Mhe. Naibu Spika, hatua za uwekaji wa viwango kwa bidhaa mbalimbali zinaendelea kupitia Kamati za Kitaalamu na Divisheni. Hadi sasa Taasisi kupitia kamati za Kitaalamu zimeshazingatia na kupitisha jumla ya Viwango vya Zanzibar Sabiini na nane (78) vikiwemo vya baadhi ya vyakula, vinywaji, mafuta ya nishati, vifaa vya umeme, ujenzi na mazingira.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa utoaji taaluma juu ya viwango na bidhaa zenye ubora kwa wazalishaji wakiwemo wajasiriamali, wafanyabiashara na watumiaji, Taasisi ya Viwango Viwango (*ZBS*) imeendelea na utoaji wa taaluma kupitia semina, vyombo vya habari, vipeperushi pamoja na kuwatembelea baadhi ya wajasiriamali.

b. Huduma ya Tathmini ya Ubora wa Bidhaa

Mhe. Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2015/2016 taasisi imeweza kupokea maombi kumi na mbili (12) ya uthibiti ubora wa bidhaa kwa ajili ya kutumia alama ya ubora ya *ZBS*. Bidhaa tatu (3) kati ya hizo zimefanikiwa kupatiwa leseni ya uthibiti ubora baada ya taratibu kukamilika. Aidha, taasisi imefanikiwa kufanya ukaguzi katika maeneo ya uzalishaji na masoko ya Unguja na Pemba.

Mhe. Naibu Spika, katika ukaguzi huo kwa upande wa viwandani *ZBS* imebaini kuwa viwanda vingi havina maabara za ndani, jambo linalokwaza kufikiwa kwa viwango na ubora unaotakiwa. *ZBS* imeweza kutoa ushauri kwa wazalishaji viwandani juu ya namna ya kuzalisha bidhaa kwa kuzingatia viwango na ubora.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa maeneo ya masoko bidhaa za aina mbili zikiwemo unga wa uji na viungo vimezuiliwa kuendelea kuwepo katika soko baada ya kubainika kutokufaa kwa matumizi ya binadamu. Katika kipindi cha mwaka 2015/2016 jumla ya sampuli kumi na tano (15) zikijumuisha bidhaa za vyakula na sabuni zimefanyiwa uchunguzi wa kimaabara.

Mhe. Naibu Spika, *ZBS* imo katika hatua za mwisho za kuanza kutekeleza, mfumo wa uthibiti na ukaguzi wa bidhaa nje ya nchi (*PVoC*). Mfumo huu unatarajiwa kuanza utekelezaji wake katika mwaka mpya wa fedha 2016/2017 baada ya taratibu kukamilika.

c. Utoaji wa Huduma za Utawala na Uendeshaji wa Taasisi

Mhe. Naibu Spika, katika kujenga uwezo wa kitaalamu kwa watendaji wake, *ZBS* imewapatia wafanyakazi 13 mafunzo ya nadharia na vitendo ndani na nje ya nchi. Mafunzo hayo yalihusu uandaaji wa viwango, ukaguzi, upimaji wa sampuli katika maabara, mfumo wa uthibiti ubora, mfumo wa mawasiliano na habari, taratibu za utumishi na utawala pamoja na masuala ya sheria. Aidha, watendaji wawili wameshiriki katika mikutano mitatu (3) ya kimataifa ambayo ni Mkutano wa Shirika la Kimataifa la Viwango vinavyohusiana na Chakula (*CODEX*) uliofanyika nchini India uliojadili kiwango cha karafuu na Mkutano Mkuu na Baraza la Shirika la Viwango la Afrika (*ARSO*) uliofanyika nchini Ethiopia na Afrika ya Kusini.

d. Mradi wa Kuimarisha Taasisi ya Viwango Zanzibar

Mhe. Naibu Spika, katika kipindi hichi *ZBS* imekamilisha matengenezo ya jengo katika ofisi zake zilizopo Amani katika eneo la Viwanda Vidogo Vidogo. Ujenzi huo ulihusisha vyumba viwili ambapo vitatumika kwa ajili ya Maabara ya Chakula na Vimelea pamoja na maabara ya Kemikali. Aidha, kwa upande wa ujenzi wa eneo la Maruhubi taasisi imefikia hatua ya kuitisha zabuni ya kutafuta mjenzi ambapo jumla ya makampuni matano yamewasilisha zabuni zao. Zabuni zimefikia katika hatua ya uchambuzi.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa ununuzi wa vifaa vya maabara, *ZBS* inaendelea na hatua za ununuzi wa vifaa vya upimaji wa mafuta ya nishati pamoja na umeme na elecktroniki. Katika hatua hii ya awali, Jumla ya TZS 927.13 milioni zinahitajika kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya upimaji wa nishati ya mafuta. Aidha, jumla ya TZS 300 milioni zinahitajika kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kupimia bidhaa za umeme na elektroniki na TZS 893.43 milioni ikiwa ni gharama za hatua ya awali ya ununuzi wa vifaa vya Maabara ya Chakula na Vimelea. Hivyo, TZS. 2,120.56 milioni zinahitajika kwa awamu ya kwanza ya ununuzi wa vifaa vya maabara za *ZBS*.

MASHIRIKA YA WIZARA

Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko inasimamia Shirika la Biashara la Taifa (*ZSTC*), Taasisi ya Viwango ya Zanzibar, Baraza la Usimamizi wa Utoaji wa Leseni za Biashara, Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali, pamoja na Baraza la Biashara. Kutokana na mfumo mpya wa utekelezaji wa Bajeti ya Serikali ambao ni kutumia programu, baadhi ya taasisi hizo ambazo zinapokea ruzuku kutoka serikalini utekelezaji wake umeelezewa katika programu hizo nilizozieleza hapo awali. Aidha, ni Shirika la Biashara la Taifa – *ZSTC* ndio ambalo halikuingizwa katika programu hizo kwa vile linajitegemea kiutendaji.

Shirika la Biashara la Taifa – *ZSTC*

Mhe. Naibu Spika, Shirika la Biashara la Taifa (*ZSTC*) limepewa jukumu la kutafuta masoko, kununua, kuuza na kusafirisha bidhaa mbali mbali za kilimo na bahari. Hata hivyo, kwa sasa shirika hilo linashughulikia zao la karafuu peke yake na kusindika bidhaa zinazotokana na zao hilo na baadhi ya mazao mengine ya viungo.

Ununuzi na Usafirishaji Karafuu

Mhe. Naibu Spika, katika msimu mwaka 2015/2016 shirika lilijipangia kununua tani 5,500 za karafuu zenye thamani ya TZS 77,000 milioni. Hadi kufikia tarehe 28/04/2016 shirika lilikwisha nunua jumla ya tani 5,709.3 za karafuu zenye thamani ya 80,000 milioni kutoka kwa wakulima, ambazo ni sawa na asilimia 103.80 ya matarajio kwa msimu wa mwaka 2015/2016. Karafuu hizo zimenunuliwa kwa viwango vya bei vifuatavyo:-

a. Daraja la 1 - TZS 14,000 kwa kilo
b. Daraja la 2 - TZS 12,000 kwa kilo
c. Daraja la 3 - TZS 10,000 kwa kilo

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka 2015/2016, shirika lilikadiria kuuza nje tani 2,945 za karafuu kwa thamani ya USD 41.8 milioni sawa na TZS 89.8 bilioni. Hadi kufikia mwezi wa April, 2016 jumla ya tani 5,602 za karafuu zenye thamani ya USD 45.11 milioni sawa na TZS 97,000 milioni ziliuzwa nje. Aidha, shirika lilifanya mauzo ya karafuu katika ujazo mdogo ya tani 22 zenye thamani ya TZS 435.7 milioni sawa na USD 201,300.

Mhe. Naibu Spika, kwa msimu wa mwaka 2016/2017, shirika linatarajia kununua tani 3,685 za karafuu zenye thamani ya TZS 55,200 milioni, kwa bei ifuatayo:-

i. TZS 15,000 kwa kilo ya karafuu ya daraja la kwanza;
ii. TZS 13,000 kwa kilo ya karafuu ya daraja la pili; na
iii. TZS 11,000 kwa kilo ya karafuu ya daraja la tatu.

Bei hiyo imezingatia Sera ya Serikali ya kununua karafuu kutoka kwa mkulima ya kwa asilimia themanini (80%) ya bei ya kuuzia karafuu nje ambayo inakisiwa kufikia baina ya USD 8,500 na USD 8,750.

Mikopo kwa Wakulima wa Karafuu

Mhe. Naibu Spika, katika kuendeleza zao la karafuu shirika limechukua jitihada za kuwasaidia wakulima katika huduma za uchumaji wa zao hilo. Juhudi hizo ni pamoja na kuwapatia mikopo wakulima ambao wametimiza vigezo ambavyo vimewekwa na shirika. Kwa mwaka 2015 – 2016, shirika lilitoa mikopo yenye thamani ya TZS 342.3 milioni kwa wakulima 126 Unguja na Pemba. Hadi kufikia mwezi wa Machi, 2016 jumla ya TZS 95.6 milioni sawa na asilimia 27 zimerejeshwa na wakulima.

Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyoeleza hapo awali kuhusiana na mabadiliko ya muundo wa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko, Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali Zanzibar (*Zanzibar Business and Property Registration Agency – BPRA*) ambayo imeanzishwa kwa Sheria mpya Nam. 13 ya mwaka 2012 ya Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali Zanzibar imehamishiwa katika wizara yangu ikitokea iliyokuwa Wizara ya Katiba na Sheria. Taasisi hii ina jukumu la kusimamia masuala ya usajili na utunzaji wa taarifa na nyaraka zilizosajiliwa zinazohusu taasisi za biashara, hati za mali za ubunifu, pamoja na usajili wa nyaraka mbalimbali kama vile za urithi, nyaraka za wakfu, kodi,

viapo na mikataba ya uhaulishaji wa vyombo vya moto ambazo zinazowahusu wananchi na wageni wanaofanya shughuli zao katika visiwa vya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa utekelezaji, Wakala ya Usajili wa Biashara na Mali ilipangiwa kutumia jumla ya TZS 1,308.2 milioni kwa mwaka 2015/2016. Kati ya fedha hizo, TZS 308.2 millioni kwa kazi za kawaida na TZS1,000 milioni kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa usajili wa biashara kwa njia ya mtandao.

Mhe. Naibu Spika, hadi kufikia mwezi wa Machi, 2016, Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali imeingiziwa jumla ya TZS 168.76 millioni sawa na asilimia 13 ya bajeti yote. Aidha, Taasisi hii imeweza kusajili Kampuni 170, Majina ya Biashara 234, Alama za Biashara 930, Jumuiya za kiraia 58 na Nyaraka 657.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa ukusanyaji mapato Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali ilipangiwa kukusanya jumla ya TZS 128.7 millioni kutoka katika vyanzo vyake vya mapato. Hadi kufikia mwezi wa Machi 2016, Wakala imekusanya jumla ya TZS 96.8 millioni sawa na asilimia 75.2 na kuziingiza katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

PROGRAMU ZA WIZARA KWA MWAKA 2016/17

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2016/2017, wizara imeweka umbele wa mgawanyo wa rasilimali katika maeneo ya msingi ya majukumu yake ya ukuzaji biashara, uendelezaji wa viwanda, uwekaji wa mazingira ya kuhamasisha biashara, usarifu wa bidhaa, wajasiriamali na wawekezaji wadogo wadogo. Kadhalika kwa upande wa ukusanyaji mapato wizara itapanua wigo wa vianzio vya mapato yake kwa kukagua bidhaa zilizofungashwa (*pre – packed goods*) na zinazoingizwa nchini pamoja na viwandani.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko itatekeleza *program* kuu nne (4) kama zifuatavyo:-

i. Programu ya Utawala na Uendeshaji;
ii. Programu ya Maendeleo ya Viwanda na Ujasiriamali;
iii. Programu ya Ukuzaji na Uendelezaji Biashara; na
iv. Programu ya Viwango na Uthibiti Ubora

A. Programu ya Utawala na Uendeshaji

Mhe. Naibu Spika, programu hii itakuwa na program ndogo zifuatazo:-

i. Uendeshaji wa Shughuli za Biashara, Viwanda na Masoko;
ii. Mipango, Sera na Utafiti; na
iii. Ofisi Kuu – Pemba

Mhe. Naibu Spika, Programu Ndogo ya Uendeshaji wa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko ambayo inatekelezwa na Idara ya Uendeshaji na Utumishi itakuwa na jukumu la kutoa huduma kwa idara zote, uimarishaji wa mazingira ya kazi pamoja na kuratibu mikutano ya majadiliano ya kibiashara ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa. Ili kutekeleza majukumu yake, programu hii ndogo imepangiwa matumizi ya TZS 1,370.58 milioni kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa Programu ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti ambayo utekelezaji wake utasimamiwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti itakuwa na jukumu la kutoa huduma za Mapitio na uandaaji wa Sera za Biashara na Viwanda, Utambuzi wa Vikwazo katika kuongeza usafirishaji wa bidhaa nje, Uimarishaji wa Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini, Utaarishaji wa ripoti za utekelezaji wa Bajeti, Uimarishaji wa Mkakati wa Mawasiliano pamoja na Ukondishwaji wa masuala ya mtambuka. Katika kutekeleza huduma hizo programu ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti imepangiwa matumizi ya TZS 313.06 milioni kwa mwaka wa fedha wa 2016/2017.

Mhe. Naibu Spika, kadhalika, program ndogo ya Ofisi Kuu Pemba ambayo itasimamia uendeshaji wa shughuli za Biashara, Viwanda na Masoko kwa upande wa Pemba imepangiwa matumizi ya TZS 341.67 milioni kwa mwaka wa fedha wa 2016/2017.

Mhe. Naibu Spika, ili kuweza kutekeleza Programu ya Utawala na Uendeshaji wa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa mwaka 2016/2017, programu hii imetengewa jumla ya TZS 2,025.31 milioni.

B. Programu ya Maendeleo ya Viwanda na Ujasiriamali

Mhe. Naibu Spika, Programu ya Maendeleo ya Viwanda na Ujasiriamali itakuwa na majukumu ya kuandaa na kutekeleza sera na mikakati ya maendeleo ya viwanda na ukuzaji ujasiriamali. Utekelezaji wa majukumu ya programu hii umegawika katika programu ndogo mbili ambazo ni:-

i. Ukuzaji Viwanda; na
ii. Maendeleo ya Ujasiriamali.

Mhe. Naibu Spika, Programu Ndogo ya Ukuzaji wa Viwanda itakuwa na jukumu la kutoa huduma za Uimarishaji wa teknolojia ya Uzalishaji kwa wazalishaji wadogo wadogo pamoja na Uimarishaji wa Sekta ya Maendeleo ya Viwanda, ambazo utekelezaji wake utasimamiwa na Idara ya Maendeleo ya Viwanda na Idara ya Mipano sera na Utafiti. Ili kutekeleza huduma hizo, programu hii ndogo imepangiwa matumizi ya TZS 297.61 milioni kwa mwaka 2016/2017.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa programu ndogo ya Ukuzaji Ujasiriamali, ambayo itakuwa na jukumu la kutoa huduma za kutoa msaada wa vifaa kwa wajasiriamali pamoja na usaidizi wa kuanzisha biashara kwa wajasiriamali, ambapo utekelezaji wake utasimamiwa na Idara ya Maendeleo ya Viwanda pamoja na Idara ya Biashara na Masoko. Ili kutekeleza huduma hizo, programu hii ndogo imetengewa TZS 56.82 milioni kwa mwaka 2016/2017.

Mhe. Naibu Spika, iIli kutekeleza majukumu ya Program ya Maendeleo ya Viwanda na Ukuzaji Ujasiriamali kwa mwaka 2016/2017 jumla ya TZS 354.43 milioni zimetengwa kwa ajili hiyo.

C. Programu ya Ukuzaji na Uendelezaji Biashara

Mhe. Naibu Spika, programu ya tatu itakayotekelezwa na wizara kwa mwaka 2016/2017 ni Ukuzaji na Uendelezaji Biashara. Kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa malengo yake, programu hii imegawanywa katika program ndogo ndogo tatu kama ifuatavyo:-

i. Ukuzaji Masoko na Usafirishaji;
ii. Ushindani Halali wa Biashara na Kumlinda Mtumiaji na;
iii. Urahisishaji Biashara na Ukuzaji Biashara za ndani.

Mhe. Naibu Spika, Programu Ndogo ya Ukuzaji Masoko na Usafirishaji itakuwa na jukumu la kutoa huduma za Uratibu wa Mkakati wa Usafirishaji Bidhaa Nje, Uimarishaji wa Soko na Uzalishaji wa Zao la Karafuu, Kuongeza Fursa za Masoko na Urahisishaji biashara pamoja Uimarishaji wa Mazingira Mazuri ya Biashara, ambapo utekelezaji wake utasimamiwa Idara ya ya Biashara na Masoko pamoja na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti. Ili kutekeleza huduma hizo programu ndogo ya Ukuzaji wa Masoko na Usafirishaji kwa mwaka 2016/2017 imetengewa jumla ya TZS 834.50 milioni.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa programu ndogo ya Ushindani Halali wa Kibiashara na Kumlinda Mtumiaji ambayo itakuwa na jukumu la kutoa huduma za Ukaguzi na Uhakiki wa Vifaa vya Mizani Vipimo, Ukaguzi wa Maduka ya Sonara, Ukaguzi wa Biashara na Maghala pamoja na Ushahijishaji na Utoaji wa Elimu kwa Watumiaji, ambapo utekelezaji wake utasimamiwa na Idara ya Biashara na Masoko na Idara ya Ushindani Halali wa Biashara. Ili kutekeleza huduma hizo programu ndogo ya Ushindani Halali wa Kibiashara na Kumlinda Mtumiaji imetengewa jumla ya TZS 116.64 milioni kwa mwaka 2016/2017.

Mhe. Naibu Spika**,** Programu ndogo nyengine chini ya Programu ya Ukuzaji na Uendelezaji Biashara ni Urahisishaji Biashara na Ukuzaji Biashara za Ndani. Programu hii ndogo itakuwa na jukumu la kutoa huduma za Kusimamia Utawala na Uendeshaji wa Baraza la Taifa la Biashara, Utoaji wa Huduma za Utawala na Uendeshajia wa Baraza la Usimamizi wa Utoaji Leseni, Ushauri na Uhamasishaji kwa wadau, Utekelezaji wa Sheria ya Biashara ya Zanzibar No. 11 ya mwaka 2013, Majadiliano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi, Uimarishaji wa Mazingira ya Biashara pamoja na Usimamizi wa Usajili wa Biashara na Mali, Utekelezaji wake utasimamiwa na Idara ya Biashara na Masoko, Baraza la Taifa la Biashara, Baraza la Usimamizi wa Utoaji wa Leseni za Biashara na Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali. Ili kutekeleza huduma hizo programu ndogo ya Urahisishaji Biashara na Ukuzaji Biashara za Ndani imetengewa jumla ya TZS 2,024.53 milioni.

Mhe. Naibu Spika, Ili kutekeleza majukumu ya Programu ya Ukuzaji na Uendelezaji Biashara kwa mwaka 2016/2017 jumla ya TZS 2,975.67 milioni zimepangwa kwa ajili hiyo.

Programu ya Viwango na Tathmini ya Ubora

Mhe. Naibu Spika, Programu ya nne itakayotekelezwa na Wizara kwa mwaka 2016/2017 ni Viwango na Tathmini ya Ubora wa Bidhaa. Kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa malengo yake, programu hii imepangiwa kuwa na programu ndogo moja ya Uthibiti wa ubora ambayo itakuwa na huduma za Uandaaji na Ukuzaji wa Viwango, Tathmini ya Ubora wa Bidhaa, Utawala na Uendeshaji wa Taasisi pamoja na Uthibiti wa ubora wa bidhaa. Utekelezaji wake utasimamiwa na Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS) pamoja na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti, Jumla ya TZS 1,529.00 milioni zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa programu hii ndogo.

Mhe. Naibu Spika, Taarifa kamili ya Wizara hii imeelezwa kuanzia ukurasa wa R-1 hadi ukurasa wa R – 23 wa kitabu cha Mkadirio ya Mapato na Matumizi ya

Fedha kwa Bajeti inayotumia Programu (PBB) kwa mwaka wa fedha 2016/2017 – 2018/2019.

SHUKRANI

Mhe. Naibu Spika, Mafanikio ya Wizara niliyoyaeleza katika hotuba yangu ni matokeo ya mashirikiano makubwa niliyoyapata kutoka kwa Wajumbe wa Baraza hili chini ya uongozi wako mahiri. Ninakushukuru wewe binafsi, Wenyeviti wa Kamati za kudumu za Baraza na Wajumbe wote kwa ushauri na michango yao mliyotupa katika kipindi cha utekelezaji wa bajeti.

Mhe. Naibu Spika, sina budi kukiri vile vile kuwa mafanikio ya kiutendaji yaliyojitokeza katika kipindi cha mwaka 2014/2015 ni matokeo ya ushirikiano mkubwa ambao Wizara yangu iliupata kutoka kwa wadau mbali mbali wa ndani na nje ya nchi yetu. Kwa madhumuni ya kutambua mchango mkubwa wa Wadau hao kwa Wizara, naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa nchi na taasisi za ndani na nje hususan zifuatazo:-

(i) Jamhuri ya Watu wa China;
(ii) India;
(iii) Serikali ya Marekani;
(iv) Shirika la Kimataifa la Kusimamia Malibunifu (World Intellectual Property Organisation – *WIPO*);
(v) Kituo cha Biashara cha Kimataifa (*International Trade* Center – *ITC*);
(vi) Mpango wa Maendeleo wa Umoja wa Mataifa (*UNDP*);
(vii) Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Viwanda (*UNIDO*);
(viii) Benki ya Dunia (*World Bank*);
(ix) Shirika la Biashara Duniani (*WTO*);
(x) Shirika la Misaada la Japan (*JICA*);
(xi) Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara za Nje Tanzania - TanTrade;
(xii) Jumuiya za Wafanyabiashara, Wenye Viwanda na Wakulima za Zanzibar na Tanzania Bara; (*ZCCA*), *TCCA;*
(xiii) Baraza la Biashara la Tanzania (*TNBC*); na
(xiv) Wafanyabiashara wote wakubwa na wadogo na Wawekezaji wa Viwanda.

Mhe. Naibu Spika, Napenda nichukue fursa hii kwa mara nyengine tena kuwapongeza kwa dhati wafanyakazi wote wa Wizara ya Biashara, Viwanda na

Masoko kwa kazi kubwa yenye ufanisi mzuri wanayoifanya kila siku licha ya kukabiliwa na changamoto mbali mbali. Ni matarajio yangu kwamba wataongeza juhudi zao ili kuzidisha ufanisi kwa kuwahudumia wananchi na kutekeleza majukumu yao ipasavyo. Kadhalika, napenda kuwapongeza wafanyakazi wote walioshiriki katika maandalizi ya Hotuba hii kwa kazi nzuri waliyoifanya. Aidha, nawaombea dua njema katika kazi zao.

Mhe. Naibu Spika, Naomba kutumia nafasi hii pia kuwashukuru wafanyabiashara wote wakubwa, wakati, wadogo, Juakali na wengine kwa juhudi zao kubwa za kuwahudumia wananchi kwa kuwapatia bidhaa mbali mbali muhimu kama vile nguo, chakula, vyombo vya moto na vifaa vya ujenzi. Nawaomba waendelee kushirikiana na Wizara yangu kwa kufanya kazi pamoja kwa lengo la kuimarisha biashara na kutoa huduma bora kwa wananchi.

Nawaomba wafanyabiashara wote kuwahurumia wananchi kwa kuwawekea bei nafuu za bidhaa ili waweze kumudu maisha yao hasa katika kipindi hichi cha Mwezi Mtukufu wa Ramadhani. Kadhalika, kwa kutambua mchango mkubwa kwa wawekezaji wa viwanda, naomba pia Mheshimiwa Spika, kuchukua nafasi hii kutoa pongezi za dhati kwa baadhi ya wadau wetu wenye viwanda na wafanyabiashara wote, wakiwemo:

a. Bakhressa Group of Companies;
b. Kiwanda cha Sukari Mahonda;
c. Zainab Bottlers;
d. Drop of Zanzibar
e. Super Pure
f. Zan Bottling
g. ZATEPA
h. Zenji Sky Cola.
i. Alawys Supplies;
j. Wajasiriamali wote

Mhe. Naibu Spika, Juhudi zao za kuimarisha viwanda nchini zinaweka njia kwa wafanyabiashara wengine kuwekeza katika viwanda.

II. MAOMBI YA FEDHA KWA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

Mapato ya Serikali:

Mhe. Naibu Spika, Kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara imepanga kukusanya TZS 371.23 milioni. Mapato hayo yatakusanywa kutoka vianzio vifuatavyo kama inavyoonekana katika **Jadweli Nam 10**:-

Jadweli Nam 10

Vyanzo vya Mapato kwa mwaka 2016/2017

KIFUNGU	MAELEZO	MAKADIRIO (mil)
R 0104	**Idara ya Biashara na Ukuzaji Masoko**	**160.00**
1422014	Ukaguzi wa mezani na vipimo	100.00
1422077	Malipo ya kazi za biashara	60.00
R0106	**Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali**	**211.23**
1146002	Ada ya Mali maiti	0.4
1422030	Alama za Biashara	90.5
1422031	Uandikishaji wa Makampuni	56.33
1422032	Uandikishaji wa majina ya biashara	43.5
1422034	Ujira wa kutengeneza nyaraka	20.5
Jumla Kuu		**371.23**

Matumizi

Mhe. Naibu Spika, Kwa upande wa matumizi na ili Wizara yangu iweze kutekeleza programu zake ilizojiwekea kwa mwaka wa fedha 2016/2017, naliomba Baraza lako Tukufu sasa liidhinishe matumizi ya jumla ya TZS 6,884.40milioni kwa programu nne (4) kama inavyoonekana katika **Jadweli Nam 11**:

Jadweli Nam 11

Maombi ya Fedha (TZS Mil)

Geresho (Code)	Programu Kuu /Programu ndogo	Makadirio 2016/2017 (mil)
R0101	**Utawala na Uendeshaji wa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko**	**2,025.31**
R010101	Uendeshaji wa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko.	1,370.58
R010102	Mipango, Sera na Utafiti	313.06
R010103	Ofisi Kuu Pemba	341.67

R0102	**Maendeleo ya Viwanda na Ujasiriamali**	**354.42**
R010201	Ukuzaji wa Viwanda	297.60
R010202	Maendeleo ya Ujasiriamali	56.82
R0103	**Ukuzaji na Uendelezaji wa Biashara**	**2,994.57**
R010301	Ukuzaji wa Masoko na Usafirishaji	834.50
R010302	Ushindani Halali wa kibiashara na Kumlinda Mtumiaji	116.64
R010303	Urahisishaji biashara na Ukuzaji Biashara za ndani	2,024.53
R0104	**Viwango na Tathmini yaUbora wa bidhaa**	**1,529.00**
R010401	Viwango naUthibiti Ubora	1,529.00
JUMLA KUU		**6,884.4**

III. HITIMISHO

Mhe. Naibu Spika, naomba kwa mara nyengine tena kukushukuru wewe binafsi pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu wote na wananchi wa Zanzibar kwa ujumla kwa ustahamilivu wao na pia kwa kunisikiliza..

Mheshimiwa Spika**,** naomba kutoa hoja.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko. Waheshimiwa Wajumbe nimekuwa napokea vikaratasi muhimu sana watu wanaomba ruhusa kutaka kwenda kufanya shughuli nyengine, lakini tujuwe kwamba na hii ni shughuli yetu kubwa, hii tuliyonayo hapa. Kwa hiyo ningeomba sana idadi ya humu ndani ni ndogo sasa hivi, ningekuombeni sana Waheshimiwa Wajumbe mbakie mvute stahamala na baadaye nadhani wajumbe wengine watakuja lakini hatuwezi kuwacha ukumbi huu wazi kiasi hiki. Kwa hiyo, ningewaomba sana wajumbe wale ambao wana dharura wazisogeze mbele dharura zao. Nawashukuru, tuendelee Mwenyekiti.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi (**Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo):** Mhe. Naibu Spika, natanguliza shukrani zangu za dhati kwa

Mwenyezi Mungu mtukufu kwa kunijaalia afya njema na uzima wa kuweza kusimama mbele ya Baraza lako tukufu katika kutekeleza majukumu ya kulijenga taifa letu. Aidha napenda pia kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii muhimu ya kutoa maoni ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mhe. Naibu Spika**,** nitakua sijatenda haki nikiwa sijamshukuru Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Mheshimiwa Balozi Amina Salum Ali pamoja na watendaji wa Wizara hii wote kwa mashirikiano yao ya dhati walioyotupatia wakati Kamati yetu ilipokua ikichambua mapendekezo ya Serikali kuhusiana na Wizara hii kama ilivyoelezwa katika Kanuni ya 110 (e) ya Kanuni ya Baraza la Wawakilishi Toleo la 2012. Aidha, napenda kumpongeza tena Mheshimiwa Waziri kwa kuteuliwa kwake kuwa Waziri wa Wizara hii, tunaamini kwamba uzowefu na jitihada zake zitasaidia ufanisi wa Wizara hii ngumu, aliyokabidhiwa.

Mhe. Naibu Spika, niruhusu pia nitoe shukrani za aina ya pekee kwa umoja wa wanawake Mkoa wa kusini Pemba kwa kuniamini na kunichagua tena kuwawakilisha katika Baraza lako tukufu la kutunga sheria. Namuomba mwenyezimungu anifanyie wepesi katika kutekeleza majukumu yangu.

Mhe. Naibu Spika, kwa moyo thabiti kabisa napenda pia kuchukua fursa hii kuwashukuru wajumbe wote wa Kamati hii kwa mashirikiano yao wanayonipatia katika kuhakikisha kwamba Kamati yetu inaweza kukamilisha na kutekeleza kazi zake za kuliwakilisha Baraza katika kusimamia na kufuatilia shughuli mbali mbali za Wizara inazozisimamia.

Mhe. Naibu Spika**,** ili kuongeza msisitizo wa Shukurani zangu naomba uniruhusu niwatambue wajumbe wa waliounda Kamati hii kwa majina.

1.	Mhe. Yussuf Hassan Iddi	Mwenyekiti
2.	Mhe. Hamida Abdalla Issa	Makamo Mwenyekiti
3.	Mhe. Ussi Yahya Haji	Mjumbe
4.	Mhe. Ali Salum Haji	Mjumbe
5.	Mhe. Hamad Abdalla Rashid	Mjumbe
6.	Mhe. Moh'd Mgaza Jecha	Mjumbe
7.	Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Mjumbe
8.	Mhe.Shadia Mohamed Suleiman	Mjumbe
8.	Ndg. Salum Khamis Rashid	Katibu
9.	Ndg. Abubakar Mahmoud Iddi	Katibu

Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko ni miongoni mwa Wizara muhimu sana kwa maendeleo na mustakabali wa nchi na wananchi kwa ujumla, hii ni kutokana na ukweli kwamba Wizara hii imebeba sekta muhimu sana kwa uchumi wa nchi yetu pamoja na maisha ya wananchi wa Zanzibar, miongoni mwa sekta hizo ni pamoja na Sekta ya Viwanda, Biashara na Masoko.

Mhe. Naibu Spika, Umuhimu wa sekta hizi umepelekea kuwepo kwa changamoto nyingi katika Wizara hii na kupelekea kuwepo kwa malalamiko mengi kutoka kwa wananchi kuhusiana na uendeshaji wa taasisi zinazohusika na sekta hizo katika kuwahudumia wananchi. Hivyo ni wajibu wa watendaji wa Wizara kufanya kazi kwa uadilifu na umakini mkubwa katika kutekeleza majukumu yao ya kuwatumikia wananchi pamoja na taifa kwa ujumla.

Mhe. Naibu Spika, Aidha kwa upande wa Serikali ni vyema ikahakikisha kwamba inazijengea mazingira mazuri taasisi zilizomo katika wizara hii, ikiwemo suala zima la kuwajengea uwezo watendaji wake, pamoja na kufanya tathmini ya mara kwa mara ili waweze kuona kasoro na changamoto ili kuchukua hatua zinazofaa katika kurekebisha kasoro zinazojitokeza katika utekelezaji wa shughuli za kawaida za Wizara hii.

UWAJIBIKAJI WA WAFANYAKAZI

Mhe. Naibu Spika, kufanya kazi kwa kujituma na kwa ubunifu ni suala muhimu sana katika kufikia malengo ya taasisi yoyote ile, kwa muda mrefu tumekuwa tukishuhudia wafanya kazi wengi wa taasisi za umma wakifanya kazi kwa mazoea bila ya kujali ni kwa kiasi gani wanaweza kufikia malengo ya kazi zao kwa mujibu wa muongozo na mwelekeo wa taasisi hizo.

Mhe. Naibu Spika, hali hii inajitokeza kutokana na ukweli kwamba wafanyakazi wengi wa taasisi za umma hufanya kazi katika hali ya utaratibu wa kawaida tu yaani '*daily rootine'* bila ya kuwa wabunifu na kuzingatia mipango na miongozo maalum ya kazi kama vile mipango kazi (*action plans)*, sera (*policies*), na dira *(vision*) za taasisi za Wizara wanazozifanyia kazi, hali hii hupelekea kutokuwepo kwa ufanisi wa kazi hizo. Aidha, wafanyakazi hushindwa kujitathmini wao wenyewe namna wanavyozisaidia taasisi zao ili ziweze kufikia malengo yaliyokusudiwa ya taasisi hizo.

Mhe. Naibu Spika, Kamati yetu inazidi kusisitiza kuwa wakati wa siasa umekwisha hivyo kila mmoja atimize wajibu wake kulingana na nafasi yake na kutekeleza kwa vitendo falsafa ya hapa kazi tu. Kwavile Chama kilichopata

ridhaa ya kuongoza nchi ni Chama cha Mapinduzi hivyo ilani inayotumika kwa kipindi chote cha miaka mitano 2016-2020 ni ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi na sio ilani nyengine yeyote.

Mhe. Naibu Spika**,** Ni wajibu wa kila mtumishi wa umma kutekeleza majukumu kwa mujibu wa kanuni za utumishi Serikali na kuunga mkono juhudi za Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuwataka watumishi wa umma wabadilike na waache kufanya kazi kwa mazowea ili kuleta mabadiliko na ufanisi katika sekta zote na wananchi waweze kunufaika na huduma za taasisi hizo.

SHIRIKA LA BIASHARA LA TAIFA (*ZSTC*)

Mhe. Naibu Spika, Kamati inapongeza mafanikio makubwa yaliyofikiwa na Shirika hili katika biashara ya karafuu na kuliendeleza zao lenyewe la karafuu, bado kuna changamoto kadhaa zinazoendelea kuikabili biashara hii ikiwemo magendo ya karafuu pamoja na kujitokeza kwa baadhi ya watu wasioitakia mema nchi yetu, kuikata mikarafaa na kufanya tanuri za mkaa.

Mhe. Naibu Spika, Pamoja na jitihada mbali mbali zinazofanywa na Wizara pamoja na taasisi husika katika kudhibiti magendo ya karafuu, magendo hayo ya karafuu yanaonekana kuwa bado ni changamoto na yanaathiri upatikanaji wa mapato ya Serikali. Hivyo, Kamati inaisisitiza Wizara na taasisi husika kuzidisha mashirikiano na wananchi ili kuweza kubaini mbinu mbali mbali mpya zinazotumiwa na wananchi wanaofanya vitendo hivyo haramu vya magendo ya karafuu.

Mhe. Naibu Spika, Kamati inaishauri Serikali kuwachukulia hatua kali wale wote wanaofanya vitendo hivi vya kihalifu vya kuuhujumu uchumi kwani tukiendelea kuwafumbia macho tutaendelea kuwa masikini.

Mhe. Naibu Spika, **t**aarifa zinaonesha kuwa kuna baadhi ya wakulima wanachanganya karafuu na makonyo au vitu visivyostahiki kuwemo katika karafuu, jambo ambalo linaweza kusababisha kuharibu sifa na ubora wa karafuu za Zanzibar. Uchanganyaji huo unaweza kuleta athari kubwa hasa kwa kuwa Serikali hivi sasa imo katika mipango mizuri ya kuilinda karafuu ya Zanzibar ikiwa pamoja na kuiweka katika utambulisho maalum (*Branding*). Hivyo, Kamati inaitaka Wizara pamoja na Shirika la Biashara la Taifa (*ZSTC*) kuengeza bidii katika kutoa elimu kwa wakulima na kukemea tabia hii, kwani licha ya kupelekea kushusha hadhi na soko la Karafuu ya Zanzibar lakini pia

itachafua mipango mizuri iliyowekwa ya kuimarisha biashara ya karafuu hapa nchini.

Mhe. Naibu Spika, Kamati imesikitishwa sana na kitendo cha baadhi ya wakulima waliokopeshwa fedha na Shirika kwa ajili ya kuwasaidia katika shughuli za karafuu na hatimaye wakulima hao kushindwa kuzilipa fedha hizo. La kusikitisha zaidi kuwa wakulima hao wameuza karafuu zao lakini wameshindwa kulipa deni hilo. Taarifa zinaonesha kuwa jumla ya Tsh 64 miliioni zilikopeshwa kwa wakulima wa karafuu kwa upande wa Pemba na jumla ya Tsh 25 miliioni kwa wakulima wa Unguja. Aidha kwa mujibu wa utaratibu, deni hilo lilitakiwa kulipwa katika kipindi cha miezi mitatu. Hivyo, Kamati inalitaka Shirika kujizatiti kikweli katika kutoa taaluma kwa wananchi juu ya taratibu za Shirika hilo pamoja kuwasisitiza wakulima ambao hawajalipa deni hilo kurejesha fedha hizo.

PROGRAMU YA UTAWALA NA UENDESHAJI WA WIZARA YA BIASHARA,VIWANDA NA MASOKO

Mhe. Naibu Spika, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti ina majukumu makubwa ya kufanya utafiti katika bidhaa mbali mbali zikiwemo zile zinazoweza kusafirishwa nje ya nchi na ndani ya nchi pamoja na kufanya utafiti wa masoko ili kuweza kufikia malengo makuu ya Wizara. Ni wazi kwamba utekelezaji mzuri wa majukumu ya Wizara takribani asilimia 100% unategemea utafiti ulio bora na umakini katika utekelezaji wa kazi zake.

Mhe. Naibu Spika, Pamoja na jitihada mbali mbali zinazochukuliwa na Wizara katika kufanya tafiti za uzalishaji na kuongeza thamani kwa bidhaa mbali mbali zinazozalishwa hapa nchini ikiwemo karafuu, Kamati inaona kuwa kuna haja kubwa kwa Wizara kuongeza nguvu zaidi katika nyanja hiyo ya utafiti juu ya uzalishaji wa bidhaa na kuongeza thamani kwa bidhaa mbali mbali zinazozalishwa hapa nchini hususan katika mazao ya mwani, mdalasini, pilipili manga, pilipili hoho na hiliki ili kuinua zaidi kipato cha wazalishaji wetu wa ndani.

PROGRAMU YA UKUZAJI NA UENDELEZAJI BIASHARA

Mhe. Naibu Spika, katika risala ya kuukaribisha mwezi mtukufu wa Ramadhani iliyosomwa siku ya tarehe 5, June 2016 na Muheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi imeonesha ni jinsi gani Raisi wetu amesikitishwa kuona kuwa, licha ya uislamu kuwa unahimiza kuoneana huruma, lakini wapo baadhi ya wafanya biashara ambao huchukua fursa ya

kupandisha bei bidhaa zao bila ya utaratibu katika mwezi huu Mtukufu wa Ramadhan, hasa zile bidhaa za Sukari, mchele na unga pamoja na zile zinazotoka Tanzania bara kama vile mbatata, kunde, vitunguu, njugu mawe na tungule ambazo Serikali hupunguza ushuru ili kuwapa afueni wananchi wananchi wake.

Mhe. Naibu Spika, hili ni jambo baya na la aibu kwa wafanya biashara na hasa ukizingatia hivi sasa kumejitokeza mgomo baridi kwa baadhi ya wafanya biashara kwa makusudi kutolipa kodi pamoja na kutoa huduma kwa ubaguzi hasa katika kisiwa cha Pemba.

Mhe. Naibu Spika, kamati yangu inataka kujua, je, serikali imejipanga vipi katika kuhakikisha inatatua kero hizi zinazoendelea kuwaumiza wananchi wetu na kuendelea kupanda mbegu mbaya ya uchochezi na kuhatarisha amani ya nchi.

Mhe. Naibu Spika, kamati pia inaishauri serikali kuongeza juhudi za kuwafatilia wafanya biashara wenye tabia hiyo ya kupandisha bei za bidhaa muhimu bila ya sababu za msingi, jambo ambalo linaathiri hatua ya Serikali ya Mapinduzi ya kutoa unafuu wa ushuru wa bidhaa muhimu kwa wafanya biashara, ili waziuze bidhaa hizo kwa wananchi kwa bei nafuu. Kadhalika, upandishaji wa bei usio na msingi unakwenda kinyume na malengo yetu ya kuanzishwa kwa biashara huru yenye ushindani.

Mhe. Naibu Spika, kamati inaipongeza sana wizara kwa kujiwekea lengo la uzalishaji wa zao la karafuu pamoja na uimarishaji wa mazingira mazuri ya biashara. Hata hivyo, kamati inaishauri Wizara ya Biashara ijenge uhusiano wa karibu zaidi hasa katika suala hili ya upandishaji wa mikarafuu, kwani imejitokeza tabia kwa serikali kupoteza nguvu nyingi katika kuzalisha na kupandisha mikarafuu lakini haionekani athari yake kwa jamii. Kamati pia inaishauri wizara kuhakikisha miche inayopandwa inasimamiwa mpaka inastawi kwani kwa kufanya hivyo ndio tutaweza kuliokoa zao hili na kuliimarisha zaidi.

PROGRAMU NDOGO YA VIWANGO NA UDHIBITI WA UBORA

Mhe. Naibu Spika, ilivyoelezwa kuwa programu hii ina programu ndogo moja ya Viwango na Udhibiti wa Ubora. Programu hii inatarajiwa kutoa huduma za kutayarisha na kukuza viwango pamoja na kushajihisha matumizi ya viwango, ni wazi kuwa utekelezaji wa programu hii inasimamiwa chini ya Taasisi ya Viwango, Zanzibar (*ZBS*).

Mhe. Naibu Spika, kamati inaishauri taasisi hii kuzidisha bidii katika kufanya ugaguzi na kutoa taarifa juu ya ukaguzi wao kila itakapoona inafaa. Madhumuni ya ukaguzi huo ni kuona dosari za wafanya biashara na wale wanaohusika na vitendo vyote vya ubadhirifu, wizi na hujuma katika vyakula vinavyouzwa na wafanya biashara wetu.

Mhe. Naibu Spika, kamati imebaini suala la viwango na ubora wa bidhaa bado limegubikwa na udanganyifu hasa kwa wafanya biashara wa vyakula. Kwa niaba ya kamati naiomba serikali iipatie Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko fedha kwa wakati ili taasisi hii iweze kufanya kazi zake kwa ufanisi.

PROGRAMU NDOGO YA MAENDELEO YA WAJASIRIAMALI

Mhe. Naibu Spika, kama ilivyoelezwa kuwa kwa mwaka wa fedha 2016/2017, programu hii inakusudia pamoja na mambo mengine kutoa misaada ya vifaa kwa wajasiriamali pamoja na usaidizi wa kuanzisha biashara kwa wajasariamali ambapo jumla ya Shilingi Tshs. 798,704,000 zimetengwa kwa ajili ya programu hiyo. Hata hivyo, kamati ina wasi wasi juu ya utekelezaji bora wa shughuli mbali mbali zilizopangwa ndani ya programu hii kwani kiwango cha fedha kilichotengwa ni kidogo na hakitoweza kukidhi matakwa ya wizara kama ilivyojitengea.

Mhe. Naibu Spika, kamati inaiomba serikali kuongeza fedha katika programu hii kwani azma ya serikali ni kukuza viwanda kwa lengo la kuimarisha uchumi na kwa fedha zilizotengwa hazitoweza kufikia malengo hayo.

Mhe. Naibu Spika, natumia fursa hii kuipongeza Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa kuonesha kuwa inawajali wakulima wake kwa kuwalipa stahiki zao wale wote waliopata ajali wakati wakikamilisha zoezi la kuchuma karafuu. Mwenyezi Mungu awajaalie wale wote waliopata ajali wakati wakifanya shughuli ya kuokoa uchumi wa nchi wapone haraka ili warudi katika kazi zao za kujenga taifa.

Mhe. Naibu Spika, Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo imejadili na kuyakubali mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa mwaka wa fedha 2016/2017, na inawaomba Waheshimiwa Wajumbe wako wote waijadili, watoe mapendekezo yao na hatimae kuipitisha bajeti hii. Napenda kuwashukuru na kuwapongeza viongozi na watendaji wa wizara hii kwa juhudi wanazochukua katika kutekeleza kazi zao pamoja na ushirikiano wao kwa kamati hii. Aidha, nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa kunisikiliza

kwa makini na utulivu wa hali ya juu wakati wote nilipokuwa nikiwasilisha hotuba hii.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Tunakushukuru sana Mhe. Shadya Mohamed Suleiman, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo. Waheshimiwa Wajumbe, sasa tunaanza michango, kwa hiyo, mchangiaji wetu wa mwanzo atakuwa ni Mhe. Suleiman Sarahan Said na baadae atafuata Mhe. Shamata Shaame Khamis.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana na mimi awali ya yote niungane na wenzangu tumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema mwenye kurehemu, tumtakie kheri Mtume wetu Muhamad *(S.A.W)*, tuwatakie kheri ndugu zetu, wazee wetu waliotangulia mbele ya haki, Mwenyezi Mungu awalaze mahala pema peponi. *Amin.*

Mhe. Naibu Spika, pia, nimpongeze sana Rais wetu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dokta Ali Mohamed Shein pamoja na Makamu wa Pili wa Rais Balozi Seif Ali Iddi kwa jitihada zao za makusudi za kuwaendeleza kimaendeleo wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, niende moja kwa moja katika hotuba yetu ya kuchangia Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko. Mimi kwanza kuna neno ambalo kila siku tunalianza kwa kusema tunafanya kazi kwa mazoea. Mimi nilikuwa namuomba sana Mhe. Waziri, kwa sababu ni mzoefu wa mambo ya ndani na nje, neno la biashara kwa sababu ameshakuwa Waziri wa Fedha, biashara na fedha ni kitu kimoja.Watendaji wengi hawajafahamu neno la 'biashara', hawajafahamu neno la 'serikali'.

Mhe. Naibu Spika, watendaji wetu wengi wakiambiwa neno la 'serikali' hawaliingizi kama ni neno la 'biashara', wao wanajua kwamba ni serikali, ni matumizi bila ya kutafuta. Ningeshauri sana sasa hivi hakuna serikali tena ya kutumia, iko serikali ya kutafuta, mambo yote sasa hivi ni lazima utafute halafu ndio utumie, mambo ya kuletewa kwa kupeleka msaada wowote wa kutumia hili jambo limeshapitwa na wakati. Kwa hivyo, ningemuomba sana Mhe. Waziri, kwa suala moja au jengine yeye ni mzoefu sana kwa masuala mengi lakini na biashara pamoja na mapato ya fedha ni mzoefu. Biashara ni kitu chochote ambacho mwenyewe umekipangia katika mazingira ya kupata faida, hasara inakuwemo, utafiti katika kuangalia hilo, lakini hakuna kitu chochote kinachoweza kwenda katika dunia hii bila ya biashara. Hata ukizaa watoto

wako basi wanakuwa ni jumla ya biashara unategemea baadae waje wakusaidie, tunasema tunawekeza.

Kwa hivyo, ningeshauri serikali sasa hivi hasa watendaji wakaondoka katika misingi ile ambayo tuna hakika ya kusema tu kwamba aa, hili ni jambo la serikali lakini tukalitengeneza kibiashara kwa niaba ya mapato. Hilo Mheshimiwa, nimesema kwa kuchangia kwa sababu muda wenyewe ni mdogo, niseme watalifafanua zaidi ili tuliweke vizuri.

Mhe. Naibu Spika, ningesema zaidi kuhusu habari ya biashara zetu za ndani. Biashara za ndani mimi najua kwamba kila wizara ina mapato yake, ina sehemu zake za kutafutia mapato, lakini neno 'biashara' tumelileta kwake moja kwa moja. Linataka ushauri katika wizara nyingi kwa sababu hii ni serikali moja, tunajenga kitu kimoja, asione tabu Mhe. Waziri, kuingilia wizara yoyote kama anaona kuna mtaji wa kupata mapato na biashara maalum akaifuatilia ili kuweza kuangalia wapi ambapo patasaidia serikali hii mapato.

Mhe. Naibu Spika, anaweza akaenda kwenye miundombinu akaangalia pale, miundombinu tunajua ni bandari, *airport*, nchi kavu hizi na wenyewe wana wizara yao, lakini yeye ni Wizara ya Biashara, tunataka tulete maboti ya kusafiria watu, wao ndio wanapitisha lakini yeye ndiye mtafutaji, hayo masuala lazima awe anakwenda nje akitafuta biashara, zote ni biashara zake, tusiondoke kwenye biashara ya serikali kwamba uti wa mgongo ni zao la karafuu, inakuwa karafuu ni moja tu mtu yeyote anaitizama karafuu, si biashara. Wizara hiyo hiyo moja ikatizama neno la karafuu itakuwa wizara haipo, lazima tuangalie tutoke tulikotoka tutizame mazao gani yanaweza yakatusafirishia, yanaweza yakatusaidia, tusikamate karafuu tu.

Mhe. Naibu Spika, tuna mkarafuu, tuna mchaichai, tuna mikaratusi, tuna mambo mengi ambayo yapo. Lakini Mhe. Waziri, yeye wizara yake ndio nilisema tunaunga wizara zote, ukikamata kilimo yeye ni Wizara ya Kilimo, akikamata fedha yeye ni Wizara ya Fedha. Kwa hivyo, ni lazima tuangalie biasahara ambayo ni wizara yake, nini biashara za ndani, nini biashara za kwetu hapa mpaka Tanzania Bara na hapa katikati na nini biashara za nje ili ziweze kutusaidia.

Mhe. Naibu Spika, biashara za ndani tunazo ameshazungumza hapa, kuna viwanda vyetu vidogo vidogo vya Said Salum Bakhressa vya maziwa tunaviangalia, yanatutosha mawiza yale, tunaweza tukauza nje na sisi au inakuwaje. Sasa isiwe tunazalisha na tunakunywa sisi tu, kwa nini tusiuze nje tukapata hizi *foreign currency*. Kwa hivyo, ningeshauri sana tukaangalia suala

la ndani. Hilo najua Mhe. Waziri ni mtaalamu mimi nagusia tu kama kukumbusha.

Mhe. Naibu Spika, suala la pili ambalo nalichukulia liko ndani ya Tanzania Bara. Mheshimiwa, ninalozungumza nimeshawahi kumuuliza maswali yangu ingawa yalikuwa mengine hayajafika, bado sisi asilimia 80 tunalishwa na vitu vingi vinavyotoka Bara. Lazima tukubali kwamba tuna vyakula ambavyo Bara inatusaidia sana.

Jengine nataka niseme bado vyakula vinavyotoka Bara, tunatumia sarafu moja ya pesa au ya shilingi, ni hiyo hiyo wala haina *changing* ya aina yoyote. Lakini bado gharama za kuja kula mlaji wa Zanzibar ni kubwa na zina changamoto nyigi.

Mhe. Naibu Spika, jambo la kwanza ni suala la usafiri. Suala la usafiri bado ni tatizo inakuwa ni majahazi mara nyengine watu wanazama, suala la meli zinakuwa na mashaka. Sisi tulikuwa na meli zetu kama MV. Jitihada, lakini zile meli hazijakuwa na mpangilio wa kuwa zina-*supply* kisiwa cha Pemba na ina-*supply* kwa hapa Zanzibar. Nilizungumza hata masuala ya nyama ya ng'ombe nikawa nazumgumza kwamba nyama Bara bado kilo shilingi 5,000, lakini leo Unguja na Pemba kilo shilingi 10,000. Mheshimiwa, bado tuangalie ili tukitaka kujua kwamba tunajijenga kibiashara, kwanza sisi wenyewe tule tushibe halafu ndio zitafutwe na nguvu za kusaidia mambo mengine, huwezi kuwa huwezi kula ukalima. Tunasema wenzetu wa Bara wana uwezo wa kulima kwa sababu wanashiba, huku kwetu sisi mtu hawezi kukamata jembe wala hilo trekta lenyewe, huwezi kufanya kazi hizo, shibe ndogo, bila ya kula wewe unaposikia pale kuleni chakula bora; sijui mboga, maziwa na nyama, hakuna, tatizo ni hilo.

Tukija kwenye upande wa samaki hatuna meli za kuvulia, bado samaki ni ghali, unamkuta mtu kila siku anakula dagaa au samaki wa shilingi 2,000, visamaki vitatu, bado ni tatizo la biashara halijakuwa safi. Leo itakuwaje Mhe. Waziri, anambie kwamba eti samaki anatoka China aje auzwe hapa rahisi kuliko samaki wetu na wataumu zaidi haiwezekani, bado hatujajipanga. Ningeshauri sana suala hilo.

Mhe. Nabu Spika, lakini ningeshauri tena bado bandari zetu *border* za Dar-es-Salaam na hapa usumbufu wa chakula bado upo, haukidhi haja kwa sababu gunia moja ile gharama nitatolewa mimi kiasi fulani, gharama ile ile atatolewa mwengine kiasi fulani, inakuwa ni tabu, hakuna kidhibiti cha kusema gunia moja ya mbatata ni shilingi 1,000 kodi yake, inakuwa na tabu tunakuwa

tunapitisha misingi ile ile ya rushwa, maana yake nina gunia 10 unasema tano, mbili ulipe, tatu usilipe inakuwa bado ni tatizo. Mbatata inafika wakati inauzwa shilingi 400 inakuwaje ifike shilingi 2,500. Keshokutwa Sikukuu nyama itauzwa kilo shilingi 20,000 au 15,000.

Mwezi wa Aprili hapa tunapandisha misharaha, Rais anasema anapandisha shilingi 300,000 kima cha chini, kilo ya nyama itakuwa shilingi 20,000 bado hatujakidhi haja ya chakula kwetu. Mhe. Naibu Spika, ingawa wizara nazichanganya lakini hii ni yake, lazima tukubaliane. Kwa sababu yeye ndiye anayekwenda kuzungumza na mambo ya biashara ya ndani.

Sasa nizungumze kumueleza vizuri Mhe. Waziri, hiki ni kisiwa au visiwa, biashara ya visiwa kila siku ina shida zake, tatizo la usafiri linakuwepo, tatizo la *border* linakuwepo, na gharama nyengine za hasara zinakuwepo, lazima tuliangalie kwa kina suala la vitu kama hivyo.

Halafu tuangalie ni biashara gani na zipi ambazo tunazipatia mapato, ni biashara aina tatu, kuna biashara tunazozalisha sisi wenyewe tunauza sawa, tuna biashara tuna-*import* kuleta halafu tunajiuzia tunapata faida, lakini kuna biashara ambazo kwa kweli ni kama za mpito lakini zote tuziangalie kwa kina, ni biashara gani inaweza ikatusaidia mapato. Lengo letu la biashara ni mapato, hakuna biashara nyengine zaidi ya mapato tunayoyatafuta, yeye amewekwa hapa kwa ajili ya mapato angetusaidia sana Mhe. Waziri, kwa sababu tunajua ana upeo mkubwa lakini lazima tukumbushane kwenye mbinu hizi.

Mhe. Naibu Spika, utakuta masuala kama ya magari, kwa nini tunakuwa wazito wa kuweka wazi, inakuja gari yangu *Land Cruise, Prado* namba fulani au *VX*, bei inakuwaje iwe hii ina namba moja. Bei nyengine hata kama ni mwaka unaitia katika *gender* unaijua tu kwamba gari yoyote inayoteremka hapa ni kiasi fulani, *agent* hana tatizo, *agent* kazi yake ni mtumwa anajua tu kwamba mimi ninafanya kazi hizi za kutoa gari lakini gari inajulikana, lakini *agent* huyo atatoa kwa shilingi 10,000; huyu atatoa kwa shilingi 20,000, huyu atatoa kwa 30,000, hakuna sababu hizo na kila kitu kinaonekana pale.

Mhe. Naibu Spika, pia, sijafahamu hasa huyu *agent* sababu yake, kwa nini mwenyewe mtu kama anataka kwenda kulipa asiweze kwenda kulipa. Wakati mwengine tunafanya makosa tunapata pesa *cash* tunaziacha kwa sababu tunasubiri *agent*, pesa *cash* zipo, kwa nini tusichukue.

Nilikuwa nasema mambo haya hata kwa watu wa mapato na wao wana mashaka yao, unamwendea *agent* mtu yeyote mwenye biashara unamwambia

nakudai shilingi milioni kumi, nina shilingi milioni mbili hizi hapa anakwambia utaleta 10 hutaki nakufungulia mashtaka, chukua mbili, subiri nane dai. Sasa unakuta mtu anakwenda pale anadaiwa shilingi milioni kumi anamwambia mtu ah, mimi sichukui kama hujaja kulipa nikakuandikia risiti, wewe chukua mbili, nane zinakuja huyu atalipa deni lipo. Sasa tunatupa mapato Mheshimiwa hilo lilikuwa ni suala ambalo naliangalia sana.

Halafu kuna suala bado tuna uti wa mgongo wa karafuu, tuna mashamba ya serikali, tuna mambo mengine mbiu ya mgambo imelia.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa, una dakika nne.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Hee! Haya Mheshimiwa. Tuna mashamba hayo. Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi inaungana humo, mashamba yako matupu mengine yanajengwa nyumba, kwa nini uti wa mgongo ni karafuu yasizalishwe karafuu yakalimwa yale mashamba, leo tunategeme matatizo ni kama hayo. Sasa mashamba yapo tele yaliyohodhiwa na serikali hayana mti hata mmoja, tunashindwa kumwagilia maji. Rais anapiga kelele kuhusu mikarafuu, kilimo wao ndio wanaotoa mikarafuu wanashindwa kuipanda, halafu tunasema uti wa mgongo sijui Thailand wanazalisha tani ngapi, sisi kwa nini hatuzalishi. Halafu sasa hivi lazima tukubaliane, pamoja na kwamba sio wizara yake Wizara ya Kilimo ikatafute mbegu za kuzaa karafuu kwa mwaka, keshokutwa miaka mitatu inazaa karafuu, karafuu yetu miaka 20 haijazaa. Kwa hiyo, lazima tukatafute karafuu za haraka haraka ambazo nazo zina tija.

Hapa tuna maembe yanapigwa mpira, watoto wanachezea mpira kule Ole, hatuna viwanda vya *juice* wala hatuna utaratibu wa kuyasafirisha, maembe huzaliana mwisho sasa hivi watu wanakata mbao miembe haina kazi. Mhe. Naibu Spika, na hili nalisemea lazima tuliangalia kwa kina.

Mhe. Naibu Spika, nataka nizungumze suala la kukatwa kwa mikarafuu, ni zao tunaloliheshimu, tunalitegemea, leo utakuta miaka ya 1990 na 2000 ilikuwa karafuu tulitoa sababu haina bei. Mheshimiwa, tuliikata mikarafuu mpaka shamba zima unaukuta mkarafuu mmoja, tumeipanda mikarafuu imekua sasa hivi tumekuja na suala jengine eti kuna siasa, mimi sijaamini kama ni siasa, tunaikata tena mikarafuu. Huu ni uchoyo na hii ni mipango maalum tu lakini sio siasa.

Kwa hivyo, ningeshauri sana Mhe. Naibu Spika, mkarafuu ukiukata mmoja huwezi kuupanda tena ukaanza zaidi ya miaka 10 au 15. Tunaikata mikarafuu

na tunafanya kama mchezo. Mhe. Naibu Spika, kuna lugha moja ya Kiswahili na mimi natowa wazo sana Waswahili wanasema; "tusihadaliwe na kiza" mengine mtaongeza nyie.

Tunahadaliwa na kiza, kesho kutwa hapa tukikaa vizuri tukizungumza mikarafuu tushaikata tutajuta kabisa kabisa. Mtu ambaye anamahaki na jambo lake anajitia ndani mwenyewe anafanya mambo yake peke yake, sio anakata mkarafuu...

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa, muda wako umekwisha.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mheshimiwa, naomba kidogo basi zile za ziada mbili.

Mhe. Naibu Spika: Nakupa dakika moja tu.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Haya Mheshimiwa.

Mhe. Naibu Spika, nataka nizungumze kitu chengine bahari narudia tena kuhusu suala la Wizara. Wizara zote mtindo wetu ambao naweza kuzungumza kwa suala la kupatia mapato. Suala hili nalisisitiza sana, kila wizara itafute mapato yake ya nguvu ya kujisaidia wenyewe. Kwa sababu mzigo tunaowekea serikali ni mkubwa sana na mbinu za kutafutia, mimi Mhe. Naibu Spika, ningeshauri kila wizara ina Mwanasheria, basi nashauri kila wizara itafute mtu maalum mfanyabiashara awasaidie kufanya biashara.

Nashukuru sana Mhe. Naibu Spika, naunga mkono hoja, najua Mhe. Waziri atafanya kazi vizuri sana. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. (*Makofi*)

Mhe. Shamata Shaame Khamis: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi asubuhi ya leo kupata fursa ambayo ni ya awali sana katika kuweza na mimi kuchangia Bajeti ya Wizara ya Bishara.

Awali ya yote, natanguliza shukurani zangu kwa Mwenyezi Mungu kutujaalia asubuhi ya leo tukiwa tuko salama na tunaendelea na funga na vile vile tukafika mahali patukufu ambapo tunaendelea kuwakilisha au kuwatetea wananchi wetu kwa yale ambayo wametutuma tuje tuwatumikea.

Baada ya hapo, napenda kabisa kwa dhati ya moyo wangu niwashukuru sana wapiga kura wangu wa Jimbo la Micheweni kwa jinsi ambavyo wamenipa

mashirikiano yao ya dhati na nikiwepo sasa naendelea na majukumu ambayo wametaka nije niwatumikie.

Lakini mwisho kabisa katika shukurani napenda sana nimshukuru Mhe. Waziri na watendaji wake wote akiwemo Katibu Mkuu mpya ambaye amepewa fursa hii ya kuweza kuisimamia au kushughulikia na kutekeleza majukumu yake kwa kupitia Wizara hii ya Biashara ambayo ni mpya. Namtakia kazi njema na aweza kushirikiana vyema na wafanyakazi wengine ili ile adhma ya serikali iweze kufikiwa.

Baada ya hapo Mhe. Naibu Spika, napenda niende moja kwa moja katika yale ambayo kwa siku ya leo ningependa na mimi kuyachangia ijapokuwa nina masikitiko kidogo kwamba bajeti hii ambayo imesomwa tunawasilishiwa kitabu hapo hapo cha bajeti na hapo hapo tunapata fursa ya kuchangia. Ni jambo ambalo nataka kusema kwamba wananchi wangu wa Jimbo langu hawatendewi haki na wananchi wa majimbo mengine katika kufanya ile kazi ya ufanisi zaidi. Lakini pamoja na hayo nitaendelea kuitumia hivyo hivyo, nadhani kwa kadri nitakavyosema basi muda nitaweza kuu-*control*.

Mhe. Naibu Spika, mimi moja kwa moja nianze kuchangia katika masuala mazima ya uingizaji wa bidhaa hapa nchini pamoja na mkakati maalum wa kuweza kupambana na zile bidhaa ambazo zimeshapitwa na wakati hapa nchini na hatua mbali mbali ambazo zinachukuliwa na wizara au na taasisi zilizopewa majukumu katika kiufanya kazi hii.

Mhe. Naibu Spika, mimi niseme kwamba tumekuwa tukishuhudia bidhaa ambazo zinaingizwa hapa nchini nyengine kabla hazijaingia kwenye nchi tunakuwa tukipata taarifa mbali mbali kwamba kuna bidhaa zimegundulika. Hizo bidhaa ni *fake*, ni jambo ambalo tunalisikia na hatua tunazisikia zinachukuliwa. Lakini vile vile kuna bidhaa ambazo zimeshafika kwenye maduka ya wafanyakazi wadogo wadogo na hatimae unasikia kama zimekamatwa madukani.

Mimi katika kulichanga jambo hili, napata mashaka sana na moja linalonipa mashaka ni kwamba hususan wafanyabishara hawa wadogo wadogo hapa nchini. Bidhaa zinazoingizwa hapa nchini zinaingizwa na wafanyabiashara wakubwa ambao wao ndio wanaoenda kuziagiza huko ambako wanziagizia na kwa muda ambao wakati mwengine nathubutu kusema hata na wao wanaweza wakazileta bidhaa hapa nchini zikiwa na muda ambao ni sahihi kwa kiwango fulani.

Lakini inawezekana pia na Bandarini tuguse kwa upande mwengine huweza kucheleweshe bidhaa kuitoa pale kwenye Bandari kwa muda mrefu ina inahitajika ifike sokoni kwa wakati pia nako kunaweza kukawa na tatizo pale na hatiame ikiwa sasa serikali inaweza ikawa nayo ni chanzo kwa kuwasababishia wafannyabishara hawa wakubwa kupata hasara.

Tumegundua kuna mrundikano mkubwa wa makontena ambayo yako pale Bandarini, namshukuru sana Mhe. Balozi Seif Ali Idd kwa hatua kubwa ambayo ameanza kuichukuwa na maelekezo kushirikiana na wizara husika kuona kwamba kutafutwa namna makontena pale kuondoshwa ili kupelekwa sehemu nyingine ambapo inaweza ikawa kupunguza pale. Lakini vile vile na bidhaa ambazo zinahitajika zifike sokoani kwa wakati.

Hapa ningeomba sana Mhe. Waziri wa Biashara, kuhakikisha kwamba jambo hili pia nae analisimamia ipasavyo. Kwa sababu tunaweza tukawalaumu wafanyabiashara wakubwa kumbe na sisi imekuwa ni chanzo cha kucheleweshe. Kwa mfano kama sasa hivi tunapata taarifa kuna meli ambazo zimekaa hazijafunga gati pale Bandarini na kuweza kuzishusha bidhaa ambazo pengine zingekuwa zingeweza kuhitajika kutumika kwa mwezi mtukufu huu wa Ramadhani. Ni jambo ambalo nalo tunatakiwa tulizingatie, vyenginevyo, tunaweza tukawatia wafanyabiashara wetu hasara na hatimae tukaweza kuwalaumu kwa kuingiza bidhaa *fake* kumbe na sisi tumeweza kuchangia kuzifanya kwamba zisifike kwa wakati na baada yake zikawa zimepitwa na wakati.

Lakini vile vile kwa hawa wafanyabishara wadogo wadogo inasikitisha sana kidogo kwamba, pamoja na kwamba ni vizuri sana kwamba tuweze kutumia bidhaa zilizokuwa hazijapitwa na wakati. Lakini ningeiomba wizara ikaangangalia utaratibu mzuri ambao tunaweza pia na wao tukawasaidia. Mfanyabiashara mdogo anapokwenda kununua bidhaa anategemea aipeleke kule kwa wakati na iweze kununuliwa pale sokoni na mlaji imfikie kwa wakati.

Lakini hatiame kuna baadhi ya mazingira bidhaa ile nadhani kwa makusudi inaweza ikatumika mbinu na wewe akaweza kununua bidhaa ile na hatiame ikachelewa kufika kwa mlaji hatiame nayo pia ikaweza kugundilika kwamba ikapita na wakati hatimae bidhaa ile inachukuliwa inaangamizwa na hatimae na faini juu.

Mimi ningeomba tuangalie mazingira ya kumsadia kwa sababu nae huyu amelipa leseni kihalali bidhaa amenunua kihalali na yeye anategemea kwamba kule sokoni kwa walaji awauzie kwa muda ambao unafaa. Lakini kutokana na

mazingira na mahitaji pengine ya wananchi au walaji kunapelekea kwamba bidhaa ile ikaweza kuganda sana kwenye duka lake na hatimae mpaka ikafika hicho kibano kikaweza kumpata na hatimae na yeye akaweza kuingia harasa zaidi.

Mimi ningeiomba wizara itafute namna gani ya kuweza kusaidia katika kudhibiti hali hii angalau pia kuwe na mpango maalum kwa yule ambaye analipa kodi vizuri, taratibu zote ambazo anazifata basi tuweze na yeye kuangalia mazingira gani tunaweza kusaidia ili kuepusha hili. Hata kama ikionekana kwamba basi kungefanywa angalau wa kuanzisha Bima ya Mfanyabiashara ili pale ambapo kanunua biashara kihalali analipa kihahali, kodi zote analipa na si zile za magendo basi tuweze kumuangalia kwa upande mwengine kuona kwamba na yeye tunaweza tukamsaidia ili ile hasara isiwe kubwa zaidi kwa upande wake na ule msingi wake usiweze kupotea moja kwa moja.

Tumeshuhudia katika Jimbo langu la Micheweni wafanyabiashara baadhi yao walikamatwa na bidhaa ambazo zilikuwa ni za halali zimeingia hapa nchini na wanalipa kodi hatimae zikakamatwa zimepitwa na wakati, ni kweli, si vyema kuuza bidhaa zile, lakini tungeangalia namna kwa sababu yeye alitegemea wateja watazinunua lakini watajea hawajazinunua kwa wakati.Sasa inapokea hali hii basi kwa yule mfanyabiashara ningeomba basi tuangalie utaratibu muafaka wa kuweza kuona kwamba nao tunaweza tukawasaidia.

Mhe. Naibu Spika, nikiachana na hilo niende kwenye masuala ya Viwanda. Mhe. Naibu Spika, katika Wilaya ya Micheni Jimbo langu ni kwamba Mhe. Rais au tokea kumetangazwa kuwa ni maeneo huru. Maeneo huru yale kulikuwa na sintofahamu tofauti kuna wale walioamini kwamba ni maeneo yataekezwa utalii na kwa bahati nzuri Mhe. Rais alifika katika maeneo ya jimbo langu kutembelea maeneo huru katika kipindi hicho ambacho kimepita cha uongozi wake. Lakini alikutana na wananchi wa kule walimuelezwa bayana kwamba wao hawahitaji utalii na Mhe. Rais, akalikubali jambo hili na akasema kwa vile kwanza eneo la utalii hatuna, lakini pamoja na kwamba eneo la utalii hatuna, lakini pia kuna uwelewa mbaya juu ya dhana nzima ya utalii hapa katika jimbo langu.

Lakini Mhe. Rais, aliwaahidi wananchi kwa kule kutajengwa viwanda, ili viweze kuwasaidia kupata ajira na kuweza kupunguza ukali ya maisha kama vile ambavyo kwa kweli historia ya nchi au katika takwimu zinaonesha katika Wilaya ya Micheweni. Kwa hiyo, kauli hizi ni kwamba tunazipata taarifa mbali mbali hata kwenye Ilani ya Uchaguzi ametaja maeneo hayo. Lakini mpaka sasa

hivi nadhani pengine labda sijapitia vizuri huku sijaona ufafanuzi katika hilo, wala sijaelewa vizuri hasa kama wame-*target* vipi katika hotuba ya Bajeti ya wizara hii. Ningeomba sana kule kuna agizo la Rais au kuna ahadi ya Rais ambayo ameweka yeye na wananchi kule, naomba sana tuangalie uwezekano kama vile viwanda vinatarajiwa kujenga basi vijengwe kwa wakati viweze kuwasaidia wananchi kuweza kupunguza alau umasikini wa kipato.

Hapa karibuni tulipata taarifa kwamba kunataka kujengwa kiwanda cha sukari ikawa kuna taarifa hizo lakini hadi sasa sijasikia mkakati wowote juu ya jambo hili. Kwa hiyo, Mhe. Naibu Spika, ningemuomba Mhe. Waziri, atakapokuja anipe ufafanuzi juu ya ahadi hizi na vile vile ufafanuzi ambavyo Chama cha Mapinduzi kilielekeza kwamba katika jambo hili.

Nikija moja kwa moja katika masuala ya wajasiriamali na ujasiriamali pia. Ukweli ni kwamba Mhe. Waziri, ningependa sana tutumie fursa hii katika hususan katika maeneo ya vijiji vyetu hususan katika Jimbo la Micheweni kuweza kuandaa utaratibu maalum wa utoaji wa taaluma kwa wananchi wetu waweze kuelewa dhana mbali mbali za biashara. Kwa mfano nataka kusema kwamba ukiangalia walio wengi katika majimbo yetu au katika maeneo yetu vijijini bado wanashindwa kujua dhana ya *Entrepreneurship* na *Entrepreneur*. Kwa hiyo, mambo haya mawili ni kwamba bado hayajafahamika, hawajaweza kujua ni yupi mfanyabiashara na zipi hizo biashara.

Kwa hiyo, naomba sana kwamba katika kukabiliana na hili katika jimbo langu la Micheweni kuna fursa nyingi ambazo tunaweza tukazitumia katika kuona kwamba tunawaelimisha wananchi wetu kuweza kujua nini biashara na hiyo biashara yenyewe. Lakini hili linaweza likatusaidia katika kuona kwamba tunaweza kuwasaidia kwa kiwango kwa kikubwa katika dhana nzima ya kupunguza umasikini na kuengeza kipato.

Nadhani katika jimbo langu ni kwamba kuna fursa nyingi, kuna fursa za maeneo ambayo ya kilimo ijapokuwa kuna changamoto ya upatikanaji wa mvua kwa wakati, lakini vile vile kama tukiweza kuwaisaidia katika masuala ya haya makundi ambayo katika masuala haya ya ujasiriamali basi tunaweza tukayasaidia katika kutafuta namna nyengine na kutafuta na kwa kushirikiana na wizara husika kuweza kuona kwamba tunawasaidia wananchi wao.

Lakini vile vile katika jimbo langu la Micheweni kuna fursa nyengine kwamba mfano kuna *SACCOS* ambazo zimeazishwa kule za kuweka na kukopa, ziko mbili katika eneo la Micheweni katika Shehia ya Majenzi na vile vile katika kijiji cha Kibuyuni nako pia iko *SACCOS*. Nadhani watu hawa pia kama

Wizara ya Biashara pia inaweza ikatengeneza mkakati wa kukutanao nao na kuweza kuona kwamba tuweze kuwaisaidia vipi katika zile *SACCOS* ambazo wamezianzisha pia zikaanzisha katika masuala mazima ya biashara ni jambo ambalo tunaweza tukaona tukawazaidia, wakazalisha ajira nyingi zaidi na vile vile wakaweza kuwasaidia wananchi katika masuala mazima ya kuwakoposha hata wengine ambao wakotayari kujiunga na *SACCOS* zao.

Lakini vile vile tunavyo vikundi mbali mbali vya akina mama ambavyo vimejiunganisha pale katika masuala mazima ya kilimo, tumekuwa tukishuhudia hususan katika Shehia ya Majenzi ya Kibuyuni wameweza kuzalisha bidhaa mbali mbali, lakini ukiangalia katika suala la soko wao wenyewe hawana mbinu za kutafuta soko na pia soko linakuwa ni shida hatimae wanazalisha hata zile *time planting* na *time harvesting* zimekuwa bado kwao ni tatizo, jambo ambalo kwa kweli tunaweza tukaona kwamba wanapoteza muda zaidi.

Hivyo, ningeshauri sana wizara kushirikiana na taasisi nyengine kuona kwamba vikundi kama vile tunaweza kuvisaidia vilime au vizalishe kwa biashara zaidi ili viweze kuondokana na tatizo la umasikini.

Mhe. Naibu Spika, niende moja kwa moja katika zao letu la biashara la karafuu. Ni kweli katika zao la karafuu ni jambo ambali ni tegemeo katika nchi yetu na limeweza kutujengea historia kubwa na kuweza kutusaidia katika kuongeza pato la nchi na ni zao ambalo linategemewa. Namasikitiko makubwa kwamba kuna wananchi ambao kwa makusudi bado hawajaelewa nini umuhimu wa karafuu au hawataki kuelewa kwa makusudi basi nadhani hawa pia ni watu ambao wanaturudisha nyuma katika nchi yetu.

Hivyo, niishauri wizara itafute namna ya kuandaa programu maalum za kuweza kutoa taaluma mbali mbali hawa watu waweze kuelewa kwa sababu...

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa, umebakisha dakika mbili.

Mhe. Shamata Shaame Khamis: Zinanitosha hizo.

Kwa hiyo, kuona kwamba hawa watu wanaweza kutoa taaluma ambayo ya kuijua umuhimu wa zao la karafuu kwa sababu hata serikali yoyote ile katika nchi hii au mtawala yeyote ndani ya nchi atakapokuwa amefanikia basi atahitaji kwamba zao hili liweze kumsaidia na kuweza kumuendesha katika kuongeza upatikanaji wa mapato katika nchi yetu.

Hivyo, basi naiomba wizara kwa nia njema kabisa iweze kutafuta namna gani ya kuweza kuona kwamba zao hili inalilinda kwa kiasi kikubwa mno. Kwa sababu sio kwamba katika jimbo langu hakuna mikarafuu lakini matuda ya zao la karafuu yananifikia pia katika jimbo langu.

Mhe. Naibu Spika, moja kwa moja naomba nimshauri tu Mhe. Waziri wa Biashara, tungeweza kushirikiana na wizara nyengine tukaangalia biashara nyengine kwa mfano hicho kilimo cha mwani ambacho kinaonekana sasa hivi uwezekano wa kuweza kuajiri na kuweza kuongeza biashara zaidi imekuwa ni kubwa, kuanza kufanya mkakati maalum kukutana na wafanyabiashara ili kuona kwamba zile kampuni ambazo zinahusika katika ununuzi wa mazao ya mwani basi waweze kutafuta namna ya kuona kwamba tunaziongeza thamani mazao haya, lakini baada yake tuweze kuona kwamba tunatafuta soko, kwa sasa imekuwa ni shida sana kwamba bei ya bidhaa hii imeshuka maradufu pamoja na kwamba imekuwa imeajiri wananchi wengi hususan vijijini na hasa katika jimbo langu la Micheweni.

Ningemuomba sana Mhe. Waziri, kwa nia njema ashiriakiane na wadau wengine katika kuona kwamba tunatafuta namna ya kuona bei ya kilimo hichi cha mwani ambacho kinaajiri wananchi wengi katika nchi yetu basi kinapatia ufumbuzi na bei inaongezeka na wananchi wanaweza kujisaidia zaidi.

La mwisho zaidi naomba tu tuliangalie pia katika zao la mpira, zao hili lilionekana pia linasaidia katika nchi yetu japo kwa kiasi fulani katika pato lake. Hivyo, basi ni vyema kuongeza mkakati kutafuta watu ambao wanaweza kufanya biashara zaidi katika suala kama ni kuyakodisha au ni kubinafsisha, lakini pia wizara ingetafuta namna hapa napo tunaweza kupata uzalishaji mkubwa na tukaweza kuongeza pato zaidi la kuongeza ile makusanyo kama vile awamu hii ilivyo ambavyo inataka tuongeze zaidi katika makusanyo na vile vile mapato ya ndani zaidi. Kwa hiyo, zao la mpira linaweza likatusaidia na mipira tunayo lakini mashamba haya yameanza kuachwa yanaonekana kwamba kupoteza ubora wake.

Mhe. Naibu Spika, mwishom naomba kwamba nichukuwe fursa hii kuwashukuru sana wananchi wa jimbo langu na nawaahidi kwamba niko pamona nao na nitaendelea kushirikiana nao. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nashukuru na mimi kwa kinipa nafasi hii asubuhi nikaweza kuchangia. Sina budi kwanza kama kawaida kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema mwenye kurehemu aliyetuwezesha hapa tukakutana leo.

Mhe. Naibu Spika, pia, nachukuwa fursa hii kumpongeza Mhe. Waziri dada yetu Bi Amina Salum Ali kwa uwasilishaji wake mzuri kwa hotuba hii. Nampongeza pamoja na timu yake yote.

Mhe. Naibu Spika, leo mimi nataka kichangie kidogo hasa nitajikita kwenye zao la Karafuu. Mhe. Naibu Spika, kama tunavyojua katika ulimwengu nchi zote zinakuwa na mazao yao tegemezi ya biashara. Zao tegemezi la biashara katika nchi yetu ni karafuu. Karafuu Mhe. Naibu Spika, miaka ya nyuma iliyopita umri wetu sisi, karafuu zilikuwa zinazalishwa kwa wingi zaidi tofauti na sasa hivi. Pamoja na mabadiliko ya tabia ya nchi kwamba nchi zimeanza kubadilika, uzalishaji umeanza kupungua lakini ni dhahiri pia na uchache wa miti yenyewe umeanza kupotea kwa kiasi kikubwa.

Mhe. Naibu Spika, ni jambo la kusikitisha sana kuiona kwamba mikarafuu kiwango chake, idadi yake inapungua siku hadi siku. Badala ya kwenda mbele sisi Mhe. Naibu Spika, tunarudi nyuma, ni jambo la kusikitisha. Hili kabla ya kuendelea mbele ninaiomba Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kupitia Shirika lake la *ZSTC* ikishirikiana na Wizara ya Kilimo, Maliasili na Uvuvi kulitafutia mbinu mbadala ya kuliendeleza kwa haraka.

Mhe. Naibu Spika, mimi katika mchango wangu wa Wizara ya Kilimo, Maliasili na Uvuvi nilimuuliza Mhe. Waziri, kwamba ana mkakati gani wa makusudi ifikapo mwaka 2020 kuhakikisha kwamba anatutoa katika kiwango cha *tons* elfu tano za karafuu angalau kutufikisha *tons* elfu kumi. Lakini jibu sikulipata vizuri. Mimi ninasema Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Kilimo, Maliasili na Uvuvi kupitia *ZSTC* pamoja na nia nzuri waliyonayo ya kuwakopesha wakulima wa karafuu, lakini *modality* wanayotumia ni ukopeshaji mimi sikubaliani nayo kabisa.

Mhe. Naibu Spika, ninasema hivi kwa sababu gani. Kwa sababu hata wao wenyewe wamezungumza na wamekiri kwenye kitabu chao katika ukurasa wa 49, kifungu cha 119, kwamba shirika linatoa mikopo au limeshatoa mikopo ya jumla ya shilingi mia tatu arobaini na mbili, nukta tatu milioni kwa ajili ya wakulima wa karafuu Unguja na Pemba kwa ajili ya uchumaji. Hivi Mhe. Naibu Spika, unakwenda kumkopesha mtu wakati wa kuchuma. Uhalisia mtu hakupeshwi kwa kuchuma. Sisi tunataka tuongeze. Kwa vyo vyote mtu wakati wa kuchuma atachuma tu zao lake, kwa sababu karafuu tayari imeiva na wala hakuna mtu ambaye ataiacha karafuu yake ianguke chini.

Lakini walitakiwa wawakopeshe wakulima, wapande mikarafuu. Mwenzangu Mhe. Suleiman, kazungumza kwamba tuna maeneo yaliyokuwa yapo wazi. Leo

miche ya mikarafuu, serikali inatoa miche ya mikarafuu kila mwaka. Lakini hebu tujiulize wamefanya utafiti wa kuthibitisha kwamba hii miche ya mikarafuu ambayo imetolewa na serikali imekua.

Mhe. Naibu Spika, jibu mimi ninakwambia asilimia 40 uhakika *for sure.* Mimi nina hakika kwa sababu mimi mwenyewe ni mkulima wa mikarafuu, mimi mwenyewe ni mtu wa karafuu. Na la kushangaza unakwenda kumkopesha mtu kuchuma karafuu, badala ya kumkopesha kupanda mikarafuu. Tutaendelea kupata *tons* elfu tano, baadae mikarafuu itashuka itakuja kuwa mikarafuu tunachuma *tons* elfu tatu.

Mhe. Naibu Spika, wenzetu wanaozalisha kwa wingi walijiwekea lengo kwamba ifikapo muda fulani tunataka tuweze kuzalisha *tons* kadhaa. Wamelifikia lengo kwa sababu walikuwa na mkakati wa mahususi. Sasa mimi ninaiomba wizara pamoja na nia nzuri waliyonayo na mimi ninaunga mkono, wala sina nia ya kuzuia wala kufanya nini. Lakini naomba Waziri atakapokuja anijibu kwamba lini watabadilisha au waone kuwa ipo sababu ya kuwakopesha sasa kwamba wakati umefika wa ku-*invest* pesa nyingi kwenye wakulima wa karafuu. Kwa sababu kama tukubali tukatae, karafuu ndiyo uti wa mgongo wa Kisiwa hichi. Sisi tunategemea mbili sehemu kubwa kisiwa chetu; Tunategemea zao la karafuu, bandari na uwanja wa ndege. Tumeongezewa na utalii Mwenyezi Mungu katujaalia tumepata.

Lakini Mhe. Naibu Spika, ni jambo la kusikitisha kwamba serikali inatoa miche. Mimi ninakwambia kwa uhakika kama ni *ZSTC* wanaotoa pesa kuwapa Wizara ya Kilimo, Maliasili na Uvuvi, waulizwe Wizara ya Kilimo miche tuliyoitoa kwa ajili ya mikarafuu kwa ajili ya kwenda kwa wakulima wamepita mabwana shamba wao kwenda kuiangalia na kuitathimini imekua kwa kiasi gani. Mhe. Naibu Spika, hakuna bado mikarafuu Pemba inakubali, asidanganye mtu mikarafuu inakubali ikipata huduma. (*Makofi*)

Lakini huduma za mikarafuu kwa Pemba wizara au Shirika la *ZSTC* kama linatoa pesa kutengeneza vitalu na wakapanda miche, lakini inaonekana bado mkakati mahususi wa kuilea miche ile hakuna Mhe. Naibu Spika. Inachukuliwa inakwenda kupandwa, ikifika kiangazi inakufa. Mwakani mkulima yule anapewa tena miche anakwenda kupanda ikitokea kiangazi inakufa. Sisi sasa itakuwa kazi yetu ni kupanda kila mwaka. Hivyo, ninaiomba wizara hii ikae pamoja na Wizara ya Kilimo, Maliasili na Uvuvi itumie watalamu wao wahakikishe kwamba miche inayopandwa inakua. Vyenginevyo, Mhe. Naibu Spika, tutakuwa tunatwanga maji kwenye kinu.

Mhe. Naibu Spika, na ninaiomba wizara hili mimi ninalizungumza *seriously* mwakani mutakuja kutoa takwimu na nitakwenda shamba moja baada ya moja ili nije niwaambie hapa fulani mumempa mikarafuu haikua na fulani na fulani. Pesa za serikali tunazipoteza. Lengo la serikali halifikiwi. Mhe. Naibu Spika, ninathubutu kusema kwamba lengo la serikali la kuongeza idadi ya mikarafuu halifikiwi. *Modality* inayotumika kutoa mikopo ya wakulima wa karafuu siyo. Wakopeshwe wakulima kwa masharti ya kupanda mikarafuu, siyo kwa masharti ya kuchuma. Karafuu ikifika kuchumwa Mhe. Naibu Spika, itachumwa tu, hakuna sababu ya mtu kuiacha karafuu zake juu ya mikarafuu. Kinachofanyika pale watu wanaopewa pesa za kukodia wengi si wenye mashamba. Wanaopewa ni wafanyabiashara. (*Makofi*)

Sawa karafuu zitakwenda serikalini, lakini mkulima na serikali haipati faida inayoitegemea. Faida ya serikali inayotegemea itapatikana pale ambapo wakulima watawezeshwa kwa lengo la kuongeza upandaji wa mikarafuu. Naiomba wizara iweke lengo itakapofika mwaka 2020 au 2022 tuwe sisi tuna uwezo wa kuzalisha maelfu ya tani za karafuu. Tuondokane na *tons* elfu tano. Mikarafuu ndani ya miaka mitano, sita, saba inaanza kuzaa, lakini iwe na huduma. Inahitaji huduma na wenye mikarafuu leo ni maskini.

Mhe. Naibu Spika, wenzetu Tanzania Bara kule wana Benki ya Ushirika na Maendeleo Vijijini (*CRDB*) inawakopesha kwa ajili ya kilimo. Hichi ni kilimo cha biashara Mhe. Naibu Spika. Jambo pekee la kufanya ni kuwakopesha wakulima...

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa, umebakiza dakika tatu.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Naibu Spika, uniongeze tano kwa heshima na taadhima naomba uniongeze.

Mhe.Naibu Spika: Kuanzia sasa hivi tano ninakupa.

Mhe. Omar Seif Abeid: Basi Mhe. Naibu Spika, siisemi tena kuhusu zao la karafuu.

Kwa hivyo, mimi ninaiomba hii wizara iweke dhamana kwa mabenki ili mabenki yaweze kuwakopesha wakulima wa zao la karafuu. Karafuu ikumbukwe kama ndiyo uti wa mgongo wa taifa hili. Tukifanya masihara tutakuja kuimba wimbo hapa. Kila siku tunaongeza hatufikii lengo.

Mhe. Naibu Spika, sehemu ya pili, ninakwenda kwenye bandari. Bandari kama tunavyojua sisi hapa tuna bandari yetu ya Zanzibar ni daraja ya pili. Tujiulize kulikoni hapa bandarini hata wafanyabiashara walie. Hivi kweli sisi tunafikia lengo la kukusanya pesa zinazohitajika hapo bandarini. Tutamlaumu Waziri wa Fedha hapa kama bajeti ndogo, tunategemea au bajeti tegemezi lakini tunatakiwa tuwajibika sisi. Sisi viongozi tuwajibike, wafanyabiashara wawajibike na kila mtu awajibike kufikia lengo. Bandari ya Zanzibar wafanyabiashara Mhe. Naibu Spika, wanalalamiko kuhusu mrundikano wa makontena, dhiki iliyopo wafanyabiashara tutawapoteza, watatukimbia watakwenda kushusha mizigo yao pengine. Bandari nyengine ipo. Ipo bandari ya Dar-es-Salaam hatuna hakika tumesikia kwamba kuna makontena mengine ya tende pia yameshushwa Dar-es-Salaam. Mhe. Naibu Spika, tunakwenda wapi.

Mhe. Naibu Spika, mimi ninaomba kama kuna kitu cha kukitizama kwanza Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko, Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji na Wizara ya Fedha na Mipango, kitu cha kwanza waitazame bandari. Mimi ninaamini pamoja na nia nzuri ya serikali, lakina kuna watu bado wana *personal interest*.Hawana nia nzuri na serikali. Serikali ifanye uchunguzi wa kina na ichukue hatua za dharura za watu ambao wanaonekana hawana uaminifu waondolewe, ile ni sekta muhimu.

Mhe. Naibu Spika, wenzetu Kenya wana bandari moja. Asilimia 30 ya bajeti ya nchi ile inatoka bandari ya Mombasa. Inakuwaje sisi leo Zanzibar tuna bandari kama ile tushindwe kukusanya mapato angalau robo ya bajeti yetu sisi ya serikali, kulikoni! Mhe. Naibu Spika, ninarudia tena kuomba kwamba Waswahili wanasema kuwa; "Usipoziba ufa utajenga ukuta". Tusingojee kujenga ukuta sisi. Aliyekuwa hakubali kuwajibika Mhe. Naibu Spika, awajibishwe yeye. Hata mimi Omar kama nimefanya kosa niwajibishwe, ni sawa. Lakini tusioneane aibu. Haiwezekani kama bandari ya Zanzibar vile ilivyo leo ishindwe kuichangia bajeti hii, sisi tuwe kila siku Mhe. Naibu Spika, tunakwenda kupiga magoti kwa watu, haiwezekani tutokane na huko.

Mhe. Naibu Spika, zao la karafuu na bandari tuliyonayo, uwanja wa ndege kama tutavitumia vizuri vinaweza vikatutoa tulipo, vikatupeleka mbali sana. Tusije tukabaki tukawa tunalaumiana humu ndani ya Baraza. Sisi ni watu wazima kila siku ikawa huyu anamlaumu mwenziwe, kumbe hamna kitu. Tufanyeni kazi kwa bidii, tuongeze makusanyo, sote tufanye uadilifu na tulitumikie taifa letu Mhe. Naibu Spika, inawezekana. Mwalimu Nyerere alitwambia i'nawezekana timiza wajibu wako' na mimi sipendi niseme sana, kwa sababu waliokujwa hawa wote wana majukumu mapya. Mimi naomba pia

Wawakilishi wenzangu bado kipindi cha kuwakwaza hawa bado, hawa tuwapeni muda tuje tuwaulize mwakani.

Mhe. Naibu Spika, mimi ninaamini kama tutafanya kazi kwa nia moja tunawea tukafikia lengo. Shirika la Biashara la Taifa *ZSTC* wawajibike, wawe karibu na wakulima wa karafuu ili tuone kwamba uzalishaji wa karafuu umeongezeka. Tuangalie changamoto zilizopo ili waweze kuzitatua.

Mhe. Naibu Spika, baada ya haya sitaki niseme tena, ninachotamka kwamba ninaiunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia. Mhe. Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mheshimiwa. Mchangiaji anayefuata ni Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy na baadae atafuatia nilikuwa nimemtaja Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi, lakini Dkt. Makame ninakuomba unipe dakika tano Mhe. Maryam, ameomba achangie kwa dakika tano ili aweze kwenda na shughuli nyengine, halafu baadae utafuate wewe. Mhe. Nadir karibu.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: *Bisimillahi Rahman Rahim*. Ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia uzima kama yangu na kuwajaalia Waheshimiwa wote wazima. Mimi nimpongeze sana Mhe. Rais Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein, kwa uteuzi wake mzuri wa Mhe. Balozi Amina Salum Ali, kamuamini na mtendaji mzuri na ndiyo maana akampa Wizara iliyokuwa nzuri na nzito. Na *inshaallah* Mwenyezi Mungu amjaalie aweze vizuri kwa wepesi. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, vile vile, mimi nitachangia hotuba hii lakini nikimaliza nina masuala yangu saba ya kuja kwa Mhe. Waziri, aje anijibu tu, sina madhumuni ya kupiga buti lakini ya kumuuliza tu ili nipate ufafanuzi zaidi.

Mhe. Naibu Spika, nitaanza na biashara. Mhe. Naibu Spika, kwanza ningeanza na suala zima la kutaka kueleza kwamba Wizara hii ya Biashara, Viwanda na Masoko ndiyo kila kitu. Wizara zote hata kuna Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo, lakini *at the end* inaishia kwenye Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko. Kwa sababu kwenye Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kuna utalii lakini unaposema unaingiza mapato tu, unapoingiza *income* maana yake ni tayari biashara ile. Sasa wizara hizi zote tayari zinahusiana kabisa kabisa na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko.

Mhe. Naibu Spika, mimi ningeanza kuelezea mambo machache. Ili biashara iende ndani ya nchi yetu ya Zanzibar basi tuhakikishe kwamba tunaziangalia kodi. Kwa kusema la ukweli Mhe. Waziri kodi za Zanzibar ni nyingi sana. Ukiangalia watu wanalipa *more than fifty percent or fourty five percent* ukijumlisha *TRA, ZRB* na kodi nyengine ndogo ndogo za wizara nyengine. Hii ni kodi kubwa sana. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, mimi ningeomba sana na kumuomba na Mhe. Rais sana kwa kuwa sisi tupo pamoja na Jamhuri ya Muungano ya Tanzania, tuna mambo tuna-*share* nao zaidi ya mambo ishirini na nne katika kitabu kile chetu; Ikiwemo mambo ya *immigration, defence* na mambo mengine, *banks* na mambo mingi yapo ndani, yapo ishirini na nne *actually*.

Lakini mimi ningeomba zaidi Mhe. Naibu Spika, wakakaa Mhe. Rais wetu wa Zanzibar kwa usikivu wake Mhe. Waziri na Waziri wa Fedha na Mhe. Mwanasheria Mkuu angalau akaomba hili suala la mahoteli, maduka, viwanda, hili suala kwenye kodi hizi zikawa *ZRB* tu wanakusanya, *TRA* wangetuachia. Kwa sababu hii nchi ni ndogo na kodi nyengine haya mambo ya *immigration* na mambo mengine ambayo tuna-*share* nao wacha wachukue.

Lakini tukisema mpaka kodi hizi nyengine za viwanda, maduka ya nguo, maduka ya *electronics* wasikusanye kodi tunaumia vibaya sana. Mimi ningeomba ushauri wangu basi angalau Mhe. Rais na Mhe. Waziri, mungeenda mukaomba hili suala likaondoshwa ili kodi ya *TRA* isikusanywe kwenye mapato haya ili nchi angalau basi *ZRB* ikaweka *from eigthteen percent, twenty five percent* itakuwa *no problem*. Lakini hivi vitu vinazidisha kodi kuwa nyingi na hii nchi itakuwa hayendi kwa kodi kama hizi, tuzungumze ukweli. Kuna mambo lazima tuwe wazi na tuyazungumze tusiyaachie la si hivyo nchi itakufa. Haiwezekani nchi ndogo kama hii, *resources* zenyewe ndizo hizo hizo, halafu kodi zaidi ya *fourty five percent* ukijumlisha. Mimi ningeomba sana hili suala lije liangaliwe.

Vile vile, kuna hii *Zanzibar Bureau Standard (ZBS).* Ili biashara iwe nzuri basi na vifaa vinavyoletwa ndani viwe vizuri. Kuna mambo tusiyaruhusu, kuna mambo yanaletwa *electronics*, *hardware* ni vitu vya umeme vya hatari lakini vipo, yaani sijui hata niseme kwenye kiwango gani, kiwango kibovu na wale wanaonunua ni wanyonge. Ndiyo maana tunasikia *shot* kila siku hazishi, nyumba zinaungua, maduka yanaungua, vitu vibovu wanauziwa. Ningeomba sana hii taasisi ikawa inasimamia sana kwenye vitu *fake* ambavyo isiviruhusu, hasa vya umeme, chakula na mambo mengine hasa kama dawa, hivi ni vitu

hatari sana. Tukisema tu tupitishe pitishe kwa uenyeji kwa kumuonea mtu huruma tutakuwa hatwendi.

Vile vile, kuna vitu ambavyo vinaletwa used kutoka Uingereza, kutoka Marekani, Canada na nchi nyengine. Hivi kule vimeshatupwa, watu wanavitupa jaani kabisa, lakini Wazanzibari wanakwenda kuokota, ndugu zetu wa Unguja na Pemba wanaokota wanakusanya wanavitia kwenye kontena wanavileta huku. Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri, hivi vitu na ukenda kuangalia ukifanya utafiti basi vina bei kuliko vitu vya dukani. Leo kaulize friji la *used* utaambiwa laki nne kwa sababu la Uingereza wanauza kwa sababu ya jina.

Lakini ukenda *deep* ukiiangalia *compressor* imetoka nchi nyengine, lile dude limetoka nchi nyengine. Lakini tusifanye hivi kwa sababu isiwe Zanzibar tena sehemu ya mitumba. Yale madude yametupwa ni chakavu hayaruhusiwi tena tunakuja kuuziwa sisi na wanauziwa wanyonge laki nne, laki saba vitu vya *used*, wakati dukani unapata friji jipya kwa laki nne au tano dogo. Mimi ningeomba sana haya mambo ya *used* mengine yapigwe marufuku, kusiingizwe uchafu hatuutaki Zanzibar, huu ni uchafu.

Vile vile, ili biashara za Zanzibar ziwe nzuri na ziwe nyepesi na ziende vizuri, basi bandari na *airport* Mhe. Waziri, lazima tukubali kwamba makontena yale yanaondoshwa, ili meli inapofika isiambiwe isubiri, makontena mengine yatiwe huku ili ile ishushe. Serikali ina viwanja vingi, kwa nini musikae nao wakahakikisha wanachukua kazi ya ziada ya kuhamisha viwanja na wakayapeleka makontena yale sehemu nyengine. Tuliambiwa juzi kwamba wameshazungumza na Manji wataweka pale pale, tukisema tupeleke pale pale ni kazi ya zeze, kwa sababu yule anataka kufanya *investment* na tukisema pale tum-*block* hata kama ni kwa muda wa mwaka, lakini tutakuwa tunafanya kazi ile ile.

Haya akishaanza kujenga tutapeleka wapi makontena. Mimi ningeomba achukuwe hatua ya dharura Mhe. Waziri, ukakae na Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kwa sababu viwanja viko vingi Zanzibar, serikali haishindwi kuchukua kiwanja kilichokua chake, hainyang'anyi mtu, kiwanja chake mali yake ichukuwe.

Mhe. Naibu Spika, nimepewa mfano pale Kibandamaiti kuna viwanja tele, Maisara mbele, kizuiliwe kimoja kiwekwe makontena. Lakini tukisema tuweke kwenye *investment* inataka kufanywa *project* kubwa halafu tupeleke pale, baada ya mwaka tutafute kwengine, itakuwa *too late* haya mambo. Mimi ningeomba sana bandari Mhe. Waziri ili biashara zije kwa wingi, hivi sasa

wafanyabiashara wamenuna na wamegoma wengine hawaleti biashara kwa sababu ya usumbufu tu, vitu vinakaa miezi mitatu au minne bandarini havijashuka.

Mhe. Naibu Spika, vile vile, suala la *Airport* uhakikishe Mhe. Waziri, unalimaliza na *income* itakuwa kubwa zaidi, jambo kuwa haiko kwenye wizara yako, lakini Idara nne hizi ziko chini yako anaweza kusema kwa njia yoyote ile; Idara ya Utalii, Idara ya Uvuvi, Idara ya Mawasiliano na Waziri wa Fedha na Mipango, hizi zinakuhusu kwa njia yoyote ile, ukiangalia yale mapato unayoyapata hata kama ni Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo, au Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji. Lakini mwisho wake inaziingizia *income* na *income* ni biashara.

Sasa wizara hizi lazima muwe makini. Ndio maana nikasema kwmaba Mhe. Rais, kakuteuweni Waheshimiwa Mawaziri na Manaibu Mawaziri kawaaminini, na mkimuangusha, basi mmeiangusha serikali, mmeangusha nchi na mmemuangusha na yeye. Mnatakiwa mfanyekazi ya ziada mshirikiane ili haya mambo yaende upesi, ili nchi iende, la si hvyo nchi itakuwa haiendi.

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye suala la viwanda. Mhe. Naibu Spika, Zanzibar kama tutaifanya ndio *headquarter* labda ya visiwa ndani ya Afrika au duniani, basi tunaweza kwa njia ya viwanda vidogo vidogo na *size* ya kati na hata viwanda vikubwa. Mimi kwanza niwapongeze sana wale wa-*local*, kama kina Bakharesa, Turky na wengineo ambao wamefanya viwanda Zanzibar, nawapongeza sana. Lakini ninachotaka kusema ni kwamba viwanda tumekaa navyo hivyo hivyo. Ukitizama Zanzibar kuna Viwanda vya Maji karibu sita, sijui vitano; Kiwanda cha Sukari kimoja, Kiwanda cha Maziwa na yeye Mhe. Bakharesa pia tumshukuru na yeye kafanya kazi ya ziada kuja kujenga kwao, hajaenda kujenga kwengine.

Mhe. Naibu Spika, lakini hapo nyuma kulikuwa kuna viwanda vingi Zanzibar, lakini vimefungwa fungwa sijui kwenye mazingira gani kusema la ukweli. Lakini kwenye maswali yangu yatakuja baadae. Kwa hivyo, mimi ningeomba Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi na Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko mkashirikiana. Kwa sababu tunao uwezo wa kufanya Kiwanda hapa cha Samaki, tunao uwezo wa kufanya Kiwanda cha Mihogo ikauzwa na kupelekwa nje, Kiwanda cha Mbatata *chips* zinazouzwa kwenye ma-*packets* kama nchi za nje, tuna mbatata za kutosha tunazo rahisi. Tuna samaki, tunao uwezo wa kutengeneza dawa, vidonge vya samaki ni bei kubwa sana duniani, tuna samaki wa kutosha wa kila aina wa kuweza kutengeneza vidonge vya dawa za samaki.

Mhe. Naibu Spika, tunao uwezo wa kufanya Kiwanda cha Karafuu, kutengeneza mafuta ya karafuu, sabuni ya karafuu, dawa za karafuu za kuchua na vitu vingi, yaani tuna vitu vya maajabu ajabu ambavyo hatuvitumii. Kwa hivyo, ningeomba sana wizara yako Mhe. Waziri, serikali isione tabu, najua haina uwezo lakini kuwekwa *PPP*, yaani (*Private Public Partnership)* ni nzuri sana, ambapo serikali imeweka. Sio tatizo serikali iwapokee watu, wako watu wanataka kuwekeza, lakini wanaogopa kuingia wao kama wao, wanataka na mkono wa serikali uwa-*support*. Leo viwanda hivi vidogo vidogo hakuna hata kiwanda kimoja kitakachofika dola milioni moja, vitaishia dola laki nne, dola laki tano na nusu au dola laki sita. Serikali ikitoa dola laki mbili na nusu ikapata *share* asilimia 30 au 40 kwenye viwanda vile na iliyobakia ana asilimia 60, basi serikali itakuwa mbali imeshasukuma, lakini nchi inapata *income* na serikali ina *income* yake kama *share* au *partner* kwenye ile kampuni.

Mhe. Naibu Spika, ningemuomba sana Mhe. Rais, Waziri wa Fedha na Mipango, pamoja na Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko wasione tabu ya kuwa-*support* wafanyabiashara, wako wafanyabiashara wanataka kuja. Mimi ninao kama watatu wanataka kufanya viwanda, lakini wanasema lazima wapate mkono wa serikali, wawe kwenye *safe hands*, hawawezi kupitia kwa watu ambao hawawajui, wako tayari kuwekeza kwenye viwanda karibu vitatu vizuri na vikubwa ambavyo *East Africa* hakuna.

Lakini serikali ikubali kuji-*commit* kwenye *one million dollar,* watowe dola laki tatu, au laki nne wachukuwe asilimia 40 kama walivyofanya kwenye *Zantel*, serikali inamiliki *shares* au kwenye kampuni nyengine. Kwa njia hii tutakwenda, Zanzibar tunao uwezo wa kufanya kama kisiwa au ni nchi yenye viwanda vidogo vidogo vingi au *size* ya kati vingi ndani ya Afrika hii au ndani ya dunia hii.

Mhe. Naibu Spika, kuna mfano mdogo tu. Mhe. Naibu Spika, tunao uwezo kama tunaambiwa mfano, simu inatengenezwa labda Hangury lakini *assemble in China*, simu nyingi sasa hivi asilimia 90. Lakini tuna uwezo sisi wa kwenda kuongea nao *Sumsun* wakaja kufanya *assemble in* Zanzibar, kwa sababu ya *cheap labour*, ni sehemu rahisi, mishahara midogo ni tofauti na nchi nyengine na ndivyo wanavyokwenda kuhamia China na nchi nyengine. Marekani inatengeneza mashine tu, lakini ufungwaji wote unafungwa China, kwa sababu ya ku-*save* yale mapato. Wafanyakazi rahisi, kodi rahisi na vitu rahisi, kwa hivyo na Zanzibar tufanyeni hivyo. Mimi naamini tunao uwezo wa kufanya viwanda zaidi ya 200, ningemuomba sana Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko angetenga sehemu ya Fumba au sehemu yoyote ya kuwa na viwanda vingi wakaweka karibu viwanja 20 ili watu wanapokuja

wanamwambia sehemu ipo hii hapa, unao uwezo wa kufanya kiwanda fulani, masharti yake ni haya. Lakini leo atakuja mwekezaji hapa ataanza kuzungushwa *ZIPA*, atakwenda ardhi, akatafute eneo tu hajalipata, lakini vitu vikiwekwa tayari basi kazi inakuwa imeshaondoka.

Mhe. Naibu Spika, vile vile, ningeendelea kwenye mchango wangu, kuna kitu muhimu sana ambacho nimekisahau, *Zanzibar Chamber of Commerce*. Mhe. Naibu Spika,...

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, umebakiza dakika tatu.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Na mimi Mhe. Naibu Spika, naomba dakika tano kwa hisani yako, pamoja na hizi tatu ziwe tano.

Mhe. Naibu Spika: Hapana, sasa kila Mjumbe akiomba hizo dakika tano, basi itakuwa tuna dakika 20 kila Mjumbe, na wengine wanataka kuchangia. Malizia.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: *Chamber of Commerce* ni muhimu sana na ningependa sana Mhe. Waziri, ukaonana naye kila baada ya muda...

Mhe. Naibu Spika: Utaandika kwa maadhishi. Unao uwezo mkubwa wa kuandika kwa maandishi ukaiwasilisha kwa Mhe. Waziri.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Sawa namalizia hizo dakika tano zangu sitaki nyingi. Dakita tatu umesema ni zangu na mbili zako wewe.

Mhe. Naibu Spika: Nimekwambia zimebakia dakita tatu.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Haya, basi sawa. Hii taasisi Mhe. Waziri, kaanayo karibu sana na kila baada ya muda unahakikisha kwamba wafanyabiashara unakua nao ili kuyatatua hayo matatizo na kuangalia hali iliyokuwepo.

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye suala la masoko. Mhe. Naibu Spika, tuwe makini sana hasa kwa hawa wanaochenjisha pesa, mimi nahisi wanatumia njia za utapeli. Kwa sababu dola mia anakuambia shilingi 2,200, dola 10 au 20 anakuambia 2,100. Dola ni dola haina tofauti, lakini nashangaa cha ajabu mpala leo kwenye masoko yale wanaachiliwa *Bureau De Change* wanaweka bei wanazozitaka. Kweli dola 20, 10 na 100 ina tofauti gani. Kwa hivyo, wanakuambia ukileta 150 *rate* shilingi 2,200, ukileta 10, 25 *rate* shilingi

2,000, hiyo haielekei, huo ni utapeli wa njia ya pesa. Kwa hivyo, ningemuomba sana Mhe. Waziri, suala hili akaliondosha ni utapeli dhahiri kabisa unaonesha, dola ni dola haina tofauti yoyote katika nchi yoyote ukienda ndio hivyo hivyo.

Vile vile, ningeiomba sana wizara ikawasaidia wafanyabiashara kuwakuza kwa kuwatangaza nje ya nchi, ili hizi biashara, *products* tukazitoa ndani ya Zanzibar na kuzipeleka nje ya nchi. Mimi ningetoa mfano mdogo tu, wizara yenyewe binafsi ni lazima iende kwenye matamasha duniani ya kuzitangaza biashara za Zanzibar, kuna matamasha tofauti duniani iende isichoke, ikatangaze bidhaa za Zanzibar, tuna utajiri na tuna vitu gani ambavyo mnao uwezo wa kuja kufanya. Pia, wakawaalika wale wawekezaji wakaja wakajua kwamba, tuna samaki wa kutosha, tuna karafuu, tuna *fruits* na tuna mashamba ambayo mnaweza mkafanya zabibu, wakaenda kutangaza vitu ambavyo tunavyo.

Mhe. Naibu Spika, mimi naamini wameshafanya, lakini kuna nchi ambazo hawakwenda, hivyo, nawataka waende, nawaomba sana waende ili hii nchi izidi kutambulikana kibiashara kuwa tuna utajiri gani wa biashara.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, mimi ningeomba sana hawa waheshimiwa matajiri ambao wana biashara kubwa, kuna baadhi ya biashara wawaachie wanyonge Mhe. Waziri. Mhe. Naibu Spika, mfanyabiashara mkubwa anazalisha, mfano natoa kama sabuni, *juice*, maji na maziwa, halafu anataka mpaka kusambaza asambaze yeye. Vitu kama chapati na vyengine vidogo vidogo wangeachiwa wanyonge. Hao wafanyabiashara wakubwa wangeachiwa wazalishe ile *product*, halafu wawapelekee wale wasambazaji wawe ni watu wa kawaida. Mpaka maduka imefika hatua sasa hivi wanafungua wenyewe hao matajiri wakubwa ya kuuza vitu vidogo vidogo, wakati maduka yako mengi wanyonge wanayo wawapelekee.

Vile vile, Mhe. Naibu Spika,...

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, muda wako umekwisha.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Ahsante sana. Mimi nashukuru na nampongeza sana Mhe. Waziri, lakini nina haya maswali yangu kidogo nataka nimpe. Mimi nina maswali yangu saba. Swali la kwanza nitaomba kujua wale waliochuma karafuu...

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, kama umeandika basi yapeleke kwa maandishi.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Naomba kidogo Mhe. Naibu Spika, dakika moja tu.

Mhe. Naibu Spika: Hapana. Ulikuwa utumie muda wako ule ule wa dakika zako 15, Mhe. Nadir.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mhe. Naibu Spika, wajumbe wote uliwapa dakika moja, mbili.

Mhe. Naibu Spika: Sasa nimekuongezea muda. Mhe. Nadir, peleka kwa maandishi.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Haya ahsante. Mimi naiunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia, sitaki kuitia vishindo, lakini maswali yangu nitayapeleka kwa maandishi.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante. Sasa nampa nafasi Mhe. Maryam Thani Juma. Mhe. Maryam uliomba muda mdogo.

Mhe. Maryam Thani Juma: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa nafasi hii ya kuweza kuzungumza machache katika Wizara hii ya Biashara, Viwanda na Masoko.

Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kunifikisha katika Baraza hili siku ya leo nikiwa mzima wa afya. Mhe. Naibu Spika, mimi nianze kwenye zao hili la karafuu. Kwanza naipongeza Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuweza kuongeza bei ya zao hili la karafuu. Zao hili ni muhimu sana kwa sababu wananchi wetu wa Zanzibar ndio zao ambalo wanalitegemea katika maisha yao.

Mhe. Naibu Spika, vile vile, nampongeza Katibu Mkuu pamoja na watendaji wake wa wizara hii. Lakini Mhe. Naibu Spika, cha kusikitisha ni watendaji wa wizara hii kwenye upimaji wa zao hili la karafuu. Wananchi wengi wanalalamika tena wanalalamika sana kutokana na upimaji wa mizani zao wafanyakazi wa shirika hili. Mezani kwa kweli sijui huwa wanazifanya vipi na wananchi hawa wanalalamikia sana mizani hizi.

Kwa hivyo, naishauri wizara hii iangalie tatizo hili kwa sababu wananchi wetu wanapata tabu sana kuhangaika mpaka kuzipata karafuu hizi, wengine ni waokotaji na wengine ni wakulima na tabu wanayoipata kwa zao hili la karafuu. Kwa hivyo, naiomba wizara hii ijitahidi wafanyakazi wake mizani zao

ziwe ni mizani madhubuti na waziweke sawa ili wananchi na wao waridhike na zao hili la karafuu wanapolipeleka pale kwenye upimaji, kwa sababu malalamiko yamekua mengi sana.

Mhe. Naibu Spika, suala hili la karafuu naiomba wizara hii ishirikiane na Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi ili wanapotoa mikarafuu kupanda, nashauri wakae kwa pamoja na Masheha, wale ambao wanapewa mikarafuu hii waipande wawe wanaifuatilia kwamba wamepewa mikarafuu mingapi na imekua mingapi, sio kila siku wanatoa mikarafuu hii na baadae hawajui mikarafuu kama imekua mingapi, wao wanatoa tu. Kwa hivyo, ikipandwa mikarafuu kwa wingi ndio tunapopata zao hili kuzaliwa kwa wingi na wananchi wakafaidika pamoja na serikali kwa ujumla.

Mhe. Naibu Spika, nije kwenye suala la viwanda. Tuna kiwanda chetu Mhe. Waziri, Kizimbani Wete Pemba, kiwanda hichi cha ujasiriamali kipo pale Kizimbani na kimetulia bila ya kufanyiwa kazi. Kwanza naiomba wizara hii kiwanda kile wawashajihishe wajasiriamali, wawepa mafunzo ili waweze kukitumia kiwanda hiki kilichopo Kizimbani Wete Pemba.

Mhe. Naibu Spika, naomba nimuulize Mhe. Waziri, je, kiwanda hiki anakifahamu na kama hakifahamu basi namuomba Mhe. Waziri, aje kukitembelea kiwanda hiki kilichopo Kizimbani Wete Pemba. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, suala hili la kiwanda japo kuwa suala hili mtashirikiana na Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi. Lakini naomba tujengewe kiwanda katika jimbo ama katika Wilaya, kwa sababu wananchi wengi hivi sasa ni wakulima wa zao la tungule. Ningeiomba wizara hii ingejenga kiwanda hiki ili wananchi wakapata mazao yao ya tungule kutengenezea tomato, na baadae wakatengenezewa soko la kuuzia tomato hizi ili kuweza kujipatia kipato katika maisha yao ya kila siku. Kwa hivyo, naiomba wizara ijitahidi kutujengea kiwanda cha tungule hata kama ni cha Wilaya au cha Mkoa cha kutengenezea tomato, ili waweze kujiendeshea maisha yao ya kila siku. Hivyo, naoimba wizara hii ijitahidi na hilo.

Mhe. Naibu Spika, pia na zao la pilipili. Kuna wakulima wengi sasa hivi wanajitahidi kulima pilipili lakini hawana soko la kuuzia pilipili manga. Kwa hivyo, ningeiomba wizara hii ikajitahidi kuwashajihisha hawa wafanyabiashara ili zao hili nao liwe na soko zaidi. Kwa hivyo, mimi sina mengi yalikuwa ni hayo yanayohusu kiwanda kilichopo Kizimbani. Naomba nimuulize Mhe. Waziri, je, ni lini atakuja kukitembelea kiwanda hiki kilichopo Kizimbani Wete Pemba.

Mhe. Naibu Spika, kwa haya machache naunga mkono Wizara hii ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa asilimia mia moja, ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, nilimtaja Dk. Makame Ali Ussi atakuwa mchangiaji wetu, baada ya Mhe. Maryam Thani Juma. Lakini Mhe. Said Soud Said pamoja na Mhe. Juma Ali Khatib, wameniomba wachangie muda huu kwa sababu wana shughuli nyengine za kitaifa. Kwa hivyo, Mhe. Said Soud Said karibu.

Mhe. Said Soud Said: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nachukua nafasi hii kuzungumzia hoja hii ya bajeti ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko. Kwanza sina budi nimpongeze Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa kuwaona wapanda mikarafuu katika visiwa vya Unguja na Pemba, kwamba walikuwa na kazi kubwa na nzito na hatimae akaamua kulipandisha bei zao la karafuu, jambo ambalo limewanyanyua Wazanzibari katika kipindi kifupi cha uongozi wake.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nataka niseme kwamba mkarafuu ni sawa na mgonjwa wa sukari. Mgonjwa wa sukari hataki kidonda na mkarafuu hautaki kuguswa, ukiubandua kidogo basi unakufa. Kwa hivyo, natoa nafasi hii kusema kwamba wananchi wa Zanzibar kwa sababu zao hili ni letu, basi tujaribu kwa kiasi kikubwa sana kuhakikisha kwamba tunapanda mikarafuu na tunaishughulikia. Serikali inajitahidi kutoa zao hili au miti hii bure kwa sababu ya kutaka kuendeleza uchumi huu ili kila mtu awe nao, na kila mtu umsaidie pale ambapo utaimarika katika maisha yake.

Mhe. Naibu Spika, Wazanzibari zao la karafuu lina historia kubwa na unapotafuta asili yake, hata ikawa hii ni zao la karafuu basi ni hadithi ndefu ambayo inahitaji wakati maalum ambao naweza nikautoa na sio hapa. Lakini ninachotaka kusema ni kwamba hatuwezi kufanikiwa kuwa na mikarafuu mingi kama vile zamani, kama hatutorudi kwenye historia ya upandaji wa mikarafuu. Awali mikarafuu ilipopandwa hapo zamani ilikuwa inatiliwa maji kwa ulazima asubuhi na jioni, kwa ulazima. Huwezi kupanda mkarafuu halafu ukauweka ukategemea mvua za kawaida eti mkarafuu huo upate kukua, haiwezekani. Nataka niwaambie kama tunataka kuliimarisha zao la karafuu katika visiwa vya Unguja na Pemba, basi ni lazima turudi kwenye historia ya upandaji wa mikarafuu, ili tuweze kuwa na zao hilo kwa wingi sana kama hapo lilipokuwa likizalishwa kwa wingi sana.

Mhe. Naibu Spika, pia, nachukua nafasi hii kusema kwamba ili tuweze kuwa na biashara nzuri ndani ya Zanzibar tunahitaji kuwa na nidhamu, biashara

haiwezi kuimarika ya aina yoyote kama haina nidhamu. Kwa hivyo, nidhamu ya biashara ni kwa wafanyabiashara kuheshimu taratibu za biashara, ili serikali ilioko madarakani ikawa haipati lawama kwa wananchi wake, inasikitisha sana kwamba fursa iliyotolewa na Serikali juu ya wafanyabiashara imekuwa chanzo na chimbuko la wananchi kulaumu Serikali, watu wanajipandishia bei kwa utaratibu wao wanaotaka wao, watu wanasahau kwamba kodi zinazotolewa na biashara ndizo zinazoongeza maendeleo ndani ya nchi, wakusanyaji wa mapato *ZRB, TRA* wanavyokwenda watu wanakimbia. Sasa nidhamu ya biashara katika visiwa hivi imekosekana na hatimae kila mtu anacheza ngoma vile anavyotaka yeye, lakini tunapenda kuthibitisha hilo kwamba Serikali hii ya awamu hii itafanyakazi ya kusimamia nidhamu ya biashara.

Tumepata masikitiko mengi kwamba watu wanajipangia bei wanavyotaka wao, sio Serikali kama haijapata habari, inajua, lakini inajipanga namna gani iweze kusimamia nidhamu ya biashara, hata wafanyakazi kama wao watakuwa wanafanyakazi bila ya nidhamu basi hiyo kazi itakuwa haiwezekani, hata sisi Wawakilishi kama tutakuwa tunakuja hapa kwa wakati tunaotaka sisi basi nidhamu ya Baraza itakuwa haipatikani.

Kwa hivyo, mazingira haya ya nidhamu ni mazingira muhimu sana na nawaomba Wawakilishi muonyeshe mfano wa nidhamu kuhudhuria katika Baraza hili kwa wakati maalum, saa tatu iwe saa tatu, lakini leo inafika hatua mpaka viti vinakuwa vitupu, nidhamu inapatikana hivyo? Sasa jambo lolote haliwezi kufanikiwa kama hakuna nidhamu na sisi tumesema kwamba hatutovumilia ndani ya Serikali hii tutapasua majipu, haya ni majibu haya, kuweka viti vitupu namna hii ni majipu, hii ni kazi, tumeomba kazi kwa wananchi kwa maana ya kuja kuwasemea na kuwatetea, lakini leo mnakuja hapa saa mnayotaka nyinyi, nidhamu gani hiyo? Hatuwezi kwenda hivyo lazima kila kitu chende kwa nidhamu.

Kwa maana hiyo Mhe. Naibu Spika, ningetaka tu nimalizie kwa sababu muda ni mfupi na wachangiaji ni wengi, lakini ningetaka niseme kwamba suala la kushughulikia walipa kodi mahoteli, suala la kushughulikia walipa kodi wa leseni, nidhamu ya Serikali itatumika, tunatoa wazo na fikra kwa wafanyabiashara wote kuhakikisha kwamba Wizara hii ndio Wizara yao na Serikali yao iko tayari kusimamia shughuli zote zitakazoweza kuwaletea maslahi wananchi wa Zanzibar bila ya kupoteza mapato, mapato ndio yanayoweza kuiongezea Serikali nguvu za kwenda.

Sasa leo ikiwa kutakuwa hakuna nidhamu ya ukusanyaji wa mapato, hakuna nidhamu ya ukataji wa leseni, tusilaumu Wizara ya Biashara na sisi

Wawakilishi ndio wenye mamlaka ya kuweza kusimamia hayo mbele huko majimboni kwetu tukaona mambo yanavyokwenda, tukaona biashara zinavyoendeshwa, wale watu wanaowalipa *ZRB* nondo na Saruji, maana kuna watu wengine wa *ZRB* hulipwa nondo na saruji wakajijengea majumba yao huko, tutoe taarifa, hayo ni majipu.

Sasa Wizara hii itakuwa inafanya kazi ya kupokea malalamiko tu ha-*increase* ikaja juu katika mazingira ya kusimamia, kuna biashara nyingi tunataka kuzifufua kama Serikali, tunaupandaji wa michikichi, mirangi rangi, vanila, tangawizi, mihiliki, hizo ni biashara ambazo Wizara hii iko tayari na inajipanga katika maingira hayo. Lakini ikiwa sisi wenyewe Wawakilishi tumekaa kule katika mazingira ya kuona wahalifu wanaiumiza Wizara hii na tunanyamaza matokeo yake tunailaumu Serikali, Serikali hii ni yetu sote, kila mzalendo wa Zanzibar ana haki ya kulinda Wizara hii ya Biashara ifanikiwe. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. (*Makofi*)

Mhe. Juma Ali Khatib (MBM): Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwanza awali ya yote nampongeza Mhe. Rais Dkt. Ali Mohammed Shein kwa kumchagua Mhe. Balozi Amina, kwa kweli ni mchapakazi hodari na ni mwanamke mwenye ujasiri mkubwa, mwenye kujiamini, tumeshuhudia kwa nyakati tofauti alijaribu kwanza kugombea nafasi ya kuwa Rais wa Zanzibar, lakini bahati mbaya kura zake hazikutosha. Amejaribu kugombea nafari ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini kwa bahati mbaya hakufanya vizuri sana kwa sababu ya kura hazikutosha, lakini ameweka rikodi nzuri sana kwa taifa letu na nchi yetu na kuonyesha kwamba wanawake wanaweza.

Kwa hivyo, kupitia kwake Mhe. Waziri, ni kama kioo kwa wanawake wenzake, kwa hivyo, nataka kuwaomba wanawake wawakilishi mushirikiane na dada mwenzenu kupitisha bajeti hii na kumsaidia katika Wizara, kwa sababu kwa bahati mbaya yeye hana Naibu Waziri, kwa hivyo, kazi nyingi anafanya yeye nampa pongezi Mhe. Waziri wa Ardhi, kwa sababu nimeona tokea alipofika hapa amekaa pembeni kwa Mhe. Waziri, kumpa msaada. Hii ni kuonyesha kwamba Baraza hili la Mawaziri linafanya kazi kama wale askari wa mwevuli, linafanya kazi kwa mashirikiano makubwa sana.

Mhe. Naibu Spika, mimi kwa upande wangu nataka kuipongeza Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar pale walipotoa uamuzi wa kutoa mikopo kwa walikuma wa karafuu, nataka kuungana na Mhe. Omar wa Konde aliposema kwamba kuna haja sasa hii mikopo itolewe kwa wale wanaotaka kupanda mikarafuu, ni kweli hoja yake ina mashiko, kuna haja sasa tukaimarisha wale

wakulima na wao ili karafuu ziwe nyingi na mikarafuu iwe mingi hawa wakulima na wao wanahitaji wapate mikopo kwa ajili ya kufanya haya mazao yawe mengi zaidi na miche ya mikarafuu iwe mingi zaidi.

Lakini vile vile nataka kuwaomba wananchi wa Unguja na Pemba tuienzi mikarafuu yetu tuliyokuwa nayo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imefanya juhudi kubwa sana pale walipoamua kutoa miche ya mikarafuu bure, hili ni jambo la kupongeza sana kwa kweli, lakini leo inafika wakati kwa sababu ya chuki zetu za kisiasa au chuki za kibinafsi tunakwenda kuikata mikarafuu wakati mikarafuu yule mkulima nanufaika, anapata uchumi, maslahi, maendeleo na kusomesha watoto wake pamoja na familia yake. Kwa kweli inabidi sisi hususan watu wa Unguja na Pemba tufikirie mara mbili, kitu gani kinakufanya mpaka unachukua hasira kwenda kuikata mikarafuu au minazi eti kwa sababu ya chuki za kisiasa, nawasihi na nawaomba kwa unyenyekevu wananchi hasa wale wenye hasira wafikirie mara mbili mbili.

Mhe. Naibu Spika, ilifikia wakati fulani hapa Unguja na Pemba tukaambiwa kwamba mikarafuu inakufa tukaletewa dawa ya *Dieback* na *Sudden Beck*, mikarafuu mingi sana ilipotea, taifa letu lilipoteza uchumi mkubwa sana, lakini Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa nyakati tofauti ikachukua hatua za makusudi kuliimarisha zao hili ikiwemo kupandisha bei na kupanda miti mingi sana.

Sasa nataka kuwaomba wananchi tusirudi kule tulikotoka wale watu wenye umri kama wangu au walionizidi wanakumbuka wakati wa *Dieback* na *Sudden Beck,* Pemba ilikufa mikarafuu mingi sana Mhe. Naibu Spika. Kwa hivyo, sasa hivi tunatakiwa tupande mikarafuu, sio tuikate mikarafuu, siasa tumemaliza sasa hivi ni wakati wa kushikana mikono tukafanya kazi.

Mhe. Naibu Spika, tukitaka tusitake sisi ndio Wazanzibari na sisi ndio wenye nchi na sisi ndio ambao kuwa tutanyanyua nchi yetu na sio mtu mwengine, kilicho mbele yetu sasa tuondoe tofauti za kisiasa kwa kunyanyua uchumi wetu, tuangalie nini tatizo letu, hasira ni hasara, unapokasirika kwenda kuua uchumi wako, mimi naomba itolewe Elimu ya Uraia, bado watu wa Unguja na Pemba hatuna Elimu ya Uraia, huwezi kuharibu vyanzo vya mapato vya nchi, huwezi kuharibu vyanzo vya mapato vya uchumi. Kwa kweli hili jambo mimi linaniuma sana ninapoona kwamba kuna mkulima amepanda mikarafuu kama wataalam walivyosema baada ya miaka mitano sita au saba ndio unaanza kuvuna zile karafuu.

Lakini leo kwa hasira anakuja mtu kuja kukata mkarafuu ule hauna kosa na hausemi, kwa kweli ni jambo baya, ukiangalia kwamba nchi hii asilimia kubwa sana ni Waislam, hata Ukristo pia unakataza mambo haya. Kwa hivyo, nawasihi watu wa Unguja na Pemba hususan wale ambao wana hasira za kisiasa, tuondoe hasira, hii tukitaka tusitake ni nchi yetu na kilichopombele sasa tuondoe tafauti zetu na tushirikiane.

Mhe. Naibu Spika, jambo jengine napenda kuwashauri wananchi kwa namna moja au kwa namna nyengine wale wakulima au wale wanaokwenda kuchuma karafuu tumeshuhudia kwa wakati mmoja au wakati mwengine wakikata matawi yale ya mikarafuu, hili jambo ni baya na hili jambo kupitia Wizara hii basi naomba watoe elimu hata Wizara ya Kilimo pia vile vile, unapokwenda kuchuma karafuu uchumi karafuu, ukikata vitawi au ukikata matawi unaufanya ule mkarafuu kama ulikuwa unatoa gunia moja au mbili ina maana zao litakalokuja utakuwa hauwezi kutoa. Kwa sababu unapoukata pale unachukua muda kuweza kuchipua tena kitawi chengine na unachukua muda kuweza tena kuzaa, kwa hivyo, ni vizuri sasa ikatolewa elimu kwa wale hususan watoto wadogo wadogo wanapokwenda kuchuma karafuu wasivikate vitawi.

Ahsante Mhe. Naibu Spika, napenda kuwasihi na kuwaomba Waheshimiwa Wawakilishi, sote kwa pamoja tushirikiane tupitishe bajeti hii ili tuweze kumpitishia Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko, bajeti yake aende akafanye kazi kwa kushirikiana na Katibu Mkuu wake, Wakurugenzi wake na Wasaidizi wake wote wa karibu ambao kuwa kwa pamoja walishirikiana katika kutunga hii hotuba ilikuwa ni nzuri sana.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo yote naunga mkono hoja hii asilimia mia moja. Ahsante Mheshimiwa. (*Makofi*)

Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi: Kama ilivyo kawaida Mhe.Naibu Spika, napenda kukwambia ahsante sana kwa kunipa nafasi hii na mimi niwe mmoja katika wachangiaji watakaochangia katika Wizara hii muhimu sana ya Biashara, Viwanda na Masoko. Kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza Mhe. Waziri wa Biashara na Viwanda Mhe. Balozi Amina Salum Ali, kwa hotuna yake nzuri hii ambayo imewasilishwa hapa leo na ndio tunayoichangia.

Pili, napenda kukupongeza wewe Mhe. Naibu Spika, kwa utaratibu mzuri wa kutupa nafasi na inapotokea dharura unatwambia ni vizuri sana nakushukuru kwa hilo.

Baada ya kuzungumza hayo nizungumzie biashara, biashara ni mtindo, mpango au utaratibu wa kuuza na kununua au kubadilishana bidhaa, biashara ni muhimu sana katika uchumi, kwa hivyo, tunaweza kusema biashara na uchumi ni watoto pacha, bila ya biashara hakuna uchumi na bila ya uchumi hakuna biashara. Kwa hivyo, nasema hii Wizara ni muhimu sana, sasa nikienda katika hii bajeti kwanza nianze Mhe. Waziri, pale alisema katika *Paragraph* ya 19, amesema kwamba, kama nilivyoeleza hapo awali sababu kuu za kushuka zilizopelekea usafirishaji wa bidhaa duniani kupungua, zikatajwa hapa, kwanza ni kuzorota kwa uchumi wa China, athari za masoko ya kifedha, madeni kwa nchi zinazoendelea. Lakini mimi nikiongezea hapa kidogo kwamba hata uzalishaji wetu pia hapa Zanzibar ni mdogo, kwa hivyo, pia unasababisha kushuka kwa biashara.

Nikienda kwenye ukurasa wa 10 jaduweli Nam. 2, hapa kuna usafirishaji na uagiziaji bidhaa, kwa kweli hii *Import* na *Export balance*, yaani uagizishaji na usafirishaji huu jamani tuushughulikie sana, kwa sababu siku zote sisi tunaagiza zaidi kuliko tunavyosafirisha, ukitizama 2011 hapa utakuta kuna tofauti kubwa sana baina ya tunachosafirisha na tunachouza, katika mwaka unaofuata ni hivyo hivyo, hakuna mwaka ambao labda tume-*balance* au tumepanda. Sasa hapa kibiashara tunatakiwa tukaze mkanda kweli kweli, si hivyo siku zote tutakuwa na uchumi ambao kwa kweli hautatuwezesha kujitegemea katika mambo yetu haya ya kimaendeleo.

Nikienda pia kwa usafirishaji baina ya sisi na ndugu zetu Bara hapa ni kwamba tunakwenda vizuri kwamba, kuna wakati bidhaa tunazopeleka sisi zinakuwa nyingi, lakini hapa tulipenda sana kulikuwa na ufafanuzi ni bidhaa gani ambazo zinapelekwa Bara zilizosababisha sisi tukawa tunapeleka bidhaa nyingi kuliko wao, kwa sababu ninavyojua tunaagiza bidhaa za chakula nyingi sana hapa, sasa kutokana na kuagiza kwa bidhaa nyingi sana huko sasa tukisema kwamba sisi tunapata zaidi kwa biashara kuliko wao kidogo pana wasi wasi. Sasa ni vizuri ingesema katika nyanja gani, pengine katika nyanja zilizokuwa si za chakula, inawezekana ikawa hivyo, kwa hivyo, tungefafanuliwa.

Na hilo limenipelekea kusema kwamba kitabu kizuri sana, kimeeleza vizuri lakini hakuna jaduweli kule mwisho, majaduweli haya yanaeleza tu *tax* yenyewe lakini hakuna *appendix* kwa mfano ningependa tuone *appendix* hapa au viambatanisho vyenye muhtasari wa mapato, wapi pamekusanywa nini na wapi pamekusanywa nini ili tupate ku-*compare* kwa vizuri zaidi, tupate pia muhtasari wa matumizi kwa mujibu wa programu au kwenye kiambatanisho pia tungejua hapa pametumika vipi na hapa pametumika vipi, ingawa

tutakwenda huko kwenye kitabu, lakini na hapa tungeonyeshwa kwa ufupi katika kiambatanisho kwamba kuna jaduweli kama hiyo.

Pia, kungekuwa vizuri kuwa na jaduweli la wafanyakazi sasa ili tuka-*compare* huku kuna upungufu au kuna nini na vituo vyao, maeneo yaliyofanyiwa ufuatiliaji pia tungeyapata hapa tukajua eneo fulani na eneo fulani, tukapata kuuliza ni eneo gani halikufuatiliwa pia ingekuwa ni vizuri sana na hata idadi ya mikarafuu ni vizuri tukaona, yaani mashamba ya mikarafuu yako mangapi, mangapi ya Serikali na yanazalishwa vipi tungejua ili tungepata kuchangia vizuri zaidi. Lakini hiyo sisemi kwamba hichi kitabu si kizuri, ni kizuri sana na mimi nakiunga mkono kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

Sasa nikienda kwenye mambo ya karafuu, karafuu ni uti wa mgongo wa uchumi wa Zanzibar, hatuna bidhaa nyengine tunazouza kwa wingi kama hii, karafuu inahitaji matunzo mazuri ili tuzalishe. Lakini uzalishaji tulionao sasa hivi kidogo nao unatia mashaka, mikarafuu pengine haipungui milioni moja. Tuseme mkarafuu mmoja tu uzalishe kilo kumi tu *average* za karafuu kwa mikarafuu milioni moja hatupungui tani elfu kumi, tunapata tani elfu tatu, elfu nne si zaidi ya elfu tano. Kuna mwaka mmoja hapa karibuni Mhe. Dkt. Shein alipoanzisha hii programu tulipata tani elfu tano. Na hiyo ni kubwa kuliko miaka mingi hata 20 iliyopita. Nimpongeze sana Mhe. Dkt. Shein kwa kuanzisha utaratibu ule wa kuhuisha mikarafuu. Kama si hivyo ninafikiri hata tani elfu moja tusingepata.

Sasa mimi ushauri wangu nadhani kuna haja ya uzalishaji wa karafuu, hatuwezi kukosa tani elfu tano, tunapata tani elfu nne, elfu tatu, tunaweza tukapata hata tani elfu kumi na tano hata ishirini tunaweza kuzipata. Sasa tulenge kwenye kuzalisha zaidi, tutoe huduma zinazohitajiwa, mikarafuu yetu ipaliliwe vizuri ifanyiwe kila kitu vizuri, tutoe *incentives* ili tuone hatutofikia hata tani elfu kumi. Tukipata tani elfu kumi tutafika mbali sana kimapato. Hilo naomba sana Wizara ya Biashara tulishughulikie sana hili ili mapato yetu yaweze kuongezeka.

Suala hili huliuliza mara kwa mara kuna *brand* ya karafuu yetu tushakaa vikao vingi sana na Wizara ya Biashara, Wizara ya Kilimo kwamba lazima tuwe na *brand*, na sasa hivi si chini ya miaka 3, 4 tunazungumzia habari ya *brand*, lakini sijaona karafuu zetu zikawa na *brand* kuwa ile ni *property* yetu inapokwenda nje, yaani ukiwa na *brand* unaweza hata ukaweka kwenye *internent* ukauza kwenye mataifa mengine, sisi tunauza karafuu Indonesia, India na nchi nyengine chache sana. Duniani karafuu tunaweza tukaiuza kwa kutuma nembo yetu ile, ile *brand* yetu ikawa na *barcode* yake wakaiona *quality*

ya karafuu yenyewe tukapata wateja wengi zaidi. Tunaomba sana tuhimize hii *branding* ya karafuu ili iweze kutusaidia katika biashara yetu.

Suala jengine ambalo ningependa nilizungumzie ni *Chamber of Commerce* tena nitalizungumzia kwa ufupi sana. Hii *Chamber of Commerce* madhumuni yake kwa sababu inaitwa *Chamber of Commerce Industry* nadhani kama hivyo, hii inawashughulikia hawa wakulima na wengine. Sasa hii ingekuwa ni kianzio kikubwa sana cha kutafuta masoko ya bidhaa zetu tunazozalisha hapa, kwa sababu nimeona hapa mnunuzi mkubwa wa bidhaa zetu kwa Zanzibar tunazozalisha ni India ambaye hununua *almost* 60% ya bidhaa tunazozalisha hapa. Lakini kwa mwaka huu uliopita hata ununuzi wa bidhaa zetu hizi India umepungua, kwa hivyo nadhani hebu tuwahamasishe hawa *Chamber of Commerce* wafanye kazi zao kwa mujibu inavyotakiwa, *Chamber* wahamasishe waweze kutusaidia katika kufanya biashara. Hawa wakikusanya bidhaa wakafanya maonesho sehemu mbali mbali za dunia wanaweza kutusaidia sana ku-*promote* au kuongeza uuzaji wa bidhaa zetu.

Jengine ambalo ningependa nilichangie lakini si kwa umuhimu wake. Nadhani kuna haja ya kuimarisha vile viungo vya biashara kwa sababu Zanzibar ni *Spice Island*, kuna viungo kama hiliki ilikuwepo na iliwahi kusafirishwa hata nje, kuna baadhi ya wafanyakazi walipelekwa Malabar India, kwa sababu kule India Malabar ndio kunakozalisha hiliki kwa wingi, wakapelekwa kusoma lakini sasa hivi hakuna hiliki. Sidhani kama kuna shamba moja ya hiliki kuwa nayo hapa Zanzibar. Sijui labda haiwi au vipi lakini nadhani tujaribu kuangalia uwezekano wa kulima hiliki, manjano, pilipili manga, zote hizi zina soko duniani, midalasini na kadhalika. Tukiweza kuzalisha hii tutaisaidia karafuu yetu hii kusonga mbele, hata pilipili kichaa nazo pia zinatakiwa. Minazi ingawa nayo inakatwa lakini pia kama minazi tutaipanda kwa wingi tukapata *copra* ile tukauza, pia kuna soko zuri sana. Kuna watu siku hizi wanatengeneza unga *coconut powder,* tui, ukilitia kwenye chakula ni sawa sawa na umeweka nazi uliyoikuna sasa hivi. Kwa hivyo tuna *chances* nyingi sana za kufanya biashara tukaweza kuendeleza nchi yetu mbele. Kupunguza huu urari wa umaskini na kadhalika.

La mwisho, sitaki kuchangia sana kwa sababu nasema hii ni wizara muhimu sana, nasema biashara ya mafuta na hili suala pia kuliulizia sana. Biashara ya mafuta duniani zinakuwa kama petroli tunachukua mfano wa petroli kunakuwa na *super* na *ordinary*. Lakini mafuta haya tunayopata hapa yanafanana kidogo na *super,* kwa sababu wanayatia rangi baada ya kwisha kuya-*refine* wanayatia rangi yanakuwa mekundu kidogo. Sasa nadhani sijui EWURA hata Tanzania Bara tunakwenda kwa mtindo huo huo wa mafuta ya aina moja tu ya petroli

wakati *specification* za *engine* zina mahitaji tofauti ya petroli. Utatumia *engine* ambayo inahitaji *ordinary* unatia mafuta ambayo hayatambulikani hujui kama ni *super* ni nani, maisha kuishi kwake kunakuwa kudogo, mashine zile tunaziua. Tabia kama hii wafanye matajiri hawajali hata wakitia maji ikiharibika atanunua nyengine, sisi masikini, ni vizuri tukapata bidhaa ambayo itatufaa kuendesha kitu chetu kikadumu kuliko mradi kutumia tu baada ya miaka fulani unakuta kitu kimekufa kabisa.

Mimi nashauri labda EWURA tuzungumze nao vizuri sana wafanye *categorization* ya mafuta hasa ya petroli; yaliyo *ordinary* na tupate mafuta ya petroli yaliyo *super* au kama wana maelezo mazuri zaidi ya kutueleza kwamba haya tunayoyafanya yako *neutral* na ambayo sidhani, *technical* sidhani kama iko hivyo, haiwezi kuwa. Lakini kama wana maelezo kwamba hiyo inatosha basi, lakini ni vizuri tufanye utafiti wa kutosha juu ya matumizi ya mafuta haya tunayotumia ya aina moja tu kwa magari tofauti na *engine* yenye mahitaji tofauti ya mafuta.

Baada ya kusema hayo nirudie kwa kumpongeza sana Mhe. Waziri wa Biashara pamoja na upya wake lakini shughuli za biashara zinakwenda vizuri, namtakia kheri sana katika kufanikisha biashara bora, aondoshe kabisa mtindo wa kuuziwa wananchi biashara mbovu zilizokwisha chakaa. Na pia aondoshe kabisa haya mambo ya kuuza kwa bei wanazotaka, leo watauza bei hii, kesho anauza bei hii, maana yake anajipangia bei anayotaka.

Kwa hivyo, narudia kusema kwamba naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja na nawaomba wenzangu waiunge mkono. Ahsante sana.

Mhe. Ali Khamis Bakari: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kwa kunipa nafasi hii kuweza kuchangia machache katika hotuba ya Biashara na Masoko. Awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetuwezesha siku ya leo tukakutana hapa tukiwa wazima pia azifanye saumu zetu kuwa makbul *In shaa Allah*.

Mhe. Naibu Spika, hii wizara ina mambo mengi na wachangiaji ni wengi kusema ukweli, na mimi nataka nidokoe dokoe tu baadhi ya sehemu zangu ambazo nilitaka kutoa mchango kwenye wizara hii.

Mhe. Naibu Spika, nije katika suala la biashara. Kwanza nimshukuru Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Serikali yake kuwapa wananchi biashara hii kuweza kufanya biashara kwa ajili ya kupata kipato na wengine wakaendelea kuwa matajiri na kuingiza bidhaa nchini. Lakini la

kusikitisha Mhe. Naibu Spika, nimwambie Mhe. Waziri hawa watu ambao walipewa hiki kibali kwa kufanya biashara kwa kuingiza ndani ya nchi, kusema ukweli mimi nataka niseme kwamba walishachoka hii hali ya kuleta hii bidhaa.

Kuna haja sasa ya serikali kufuata mfumo wake ule wa zamani wa maduka ya serikali, kwa sababu hawa wananchi ambao wanafanya biashara hizi tunawaita matajiri. Biashara ambazo wanaleta kwanza ni mbovu, pili wanawanyanyasa wale ambao wanawafanyia biashara hususan wale wananchi kwa sababu wanashughulikia masuala ya siasa, jambo ambalo wao wanachukua jukumu kubwa kwa serikali kwamba watawezesha hii hali ya kuleta hizi bidhaa katika nchi na kuwafanya wananchi wale wapate hizi huduma tofauti tofauti. Sasa hivi imeonekana kwamba watu wanaleta hizi bidhaa lakini wanashirikiana na masuala ya siasa jambo ambalo si zuri, kuna baadhi ya watu wengine wanawauzia huduma hii ya biashara lakini wengine hawauziwi bidhaa.

Vile vile, wanaleta bidhaa ambazo kwa kusema ukweli ni feki, kwa mfano kuna huu uingizaji wa mchele wa mapembe, kusema ukweli mchele huu sasa hivi inafikia kuwa kadhia kwa kusema ukweli hali halisi ya uingizaji wa mchele huu wa mapembe kusema kweli ni mbaya. Hata binadamu hahitaji hata mchele ule kuula. Maradhi mengi sasa hivi yanajitokeza kwa mchele ambao tunaoutumia, tunatafuta mchawi na hali ya kuwa uchawi tunakwenda kuutafuta sisi wenyewe. Kwa nini mchele huu tusiukemee kwa wale wafanyabiashara ambao wanaleta na tukaanza kununua mchele wetu wa hapo Dar es Salaam, kama kule Shinyanga, Mbeya na baadhi ya sehemu nyengine tukashirikiana nao kwa pamoja tukawa tunatumia mchele wao. Na kwa nini twende tukaagize mchele nje ambao una gharama kubwa lakini haufai kula hata binaadamu. Kwani tukikosa kula huu mchele sisi ndio tutakufa, kwa nini tusiweze kutumia baadhi ya nyenzo nyengine tukaweza kuishi. Kwa mfano kuna unga wa ngano, kuna maharage yote yanahitajika kula mwanadamu na kuweza kupata nguvu. Hata mtama kwa kusema ukweli, mahindi ni vitu ambavyo sasa unaweza ukavitumia na afya yako ikawa vizuri.

Kwa hivyo, mimi naona suala hili la huu mchele wa mapembe nimuombe waziri aliangalie sana. Watu wanaleta mchele lakini sio mzuri wingi wao wanaubadilisha mapolo. Kama mara hii yameletwa ya *blue* mara nyengine yanaletwa meusi, yanaletwa kijani. Kwa hivyo hii kuna haja ya kuangalia kwa kina mchele huu wa mapembe, hilo la kwanza.

Lakini la pili hapa hapa kwenye ufanyaji huu wa biashara kutoka nje, kuna hawa ambo wanaleta haya mafuta ya kula. Kusema ukweli mimi sijui mafuta yale ya kula yanatokana na kitu gani kusema ukweli. Hebu tuangalieni mpango

wa zamani wazee wetu waliokuwa wakiuboresha kwenye ufanyaji wa mafuta ya nazi, kwa nini tusirudie kule suala hili la mafuta ya nazi watu wakawezeshwa kuzalisha yale mafuta na wakapata bei nzuri.

Huduma hii ikiboreka baadhi ya wananchi watapata pesa za kujikwamua na mahitaji yao ili kuona kwamba yale mafuta yanazalishwa kwa wingi na kuweza kutoa huduma katika serikali yetu na wananchi kwa ujumla. Jambo ambalo mafuta haya ya kula sasa hivi yaliyoingia kwa mfano keshokutwa tunategemea baada ya kumaliza mwezi mtukufu wa Ramadhani kunakuja sikukuu. Ukimaliza kufutari jambo la mwanzo unauliza jamani kuna maji mafuta yale yashaingia tumboni. Lakini hapo zamani wazee wetu walitwambia walikuwa wakitumia mafuta ya nazi basi kwa muda wa siku tatu kama ni chakula kilichopikiwa mafuta nazi kiko salama hakichachi, hakifanyi chochote. Lakini sasa hivi ukipikiwa chakula ndani ya mafuta haya basi ndani ya siku mbili mtihani, kutajitokeza maradhi haya na haya.

Vile vile, nikiendelea kwenye masuala haya ya biashara kumeingia biashara ya sabuni, sasa hivi ukipita njiani unasikia kengele, haya sabuni, sabuni zile sasa watu wanazitumia kutokana kwamba ni rahisi kumbe tunanunua maradhi tukijiongezea. Jambo la mwanzo ukitumia sabuni zile ambazo zimejitokeza ndani ya sehemu zetu za hawa wafanyabiashara wadogo wadogo, *fungus* zimekuwa kubwa, kumekuwa na maradhi ya kucha za mikono jambo ambalo kusema kweli maradhi tunayaleta wenyewe.

Nimuombe Mhe. Naibu Spika, nimwambie Mhe. Waziri na hili pia aliangalie kuna wafanyaji wa biashara wa sabuni sijui sabuni hii inazalishwa kutoka wapi na inafanywa kwa kitu gani. Kuna mambo yetu mengi kwa mfano huu mwani nilisikia unatolewa sabuni na baadhi ya sehemu vitu vyengine ambavyo vipo hapa kwa nini tusiweze kubuni mambo ambayo ni mazuri na yatawafanya wananchi kuweza kuona kwamba afya zao ni nzuri na kupata vipato zaidi.

Mhe. Naibu Spika, niendelee kwenye masuala ya leseni ya huu ufanyaji wa biashara. Kwa kusema kweli sijui nimuulize Mhe. Waziri mara hii ndio wamepewa hii nafasi ya hii serikali kwa kupitia hii wizara. Sijui kuna utaratibu gani ya hizi huduma ya kutolewa leseni kwa baadhi ya hawa wafanyabiashara. Kwa sababu mimi najua kama unataka kuajiriwa lazima kwanza ufanye *interview*, unaulizwa umefika darasa la ngapi katika kufanya hili jambo unaloliomba ukafanya *interview* na baadae ukaonekana lile jambo ambalo unaliomba unaliweza na ndio ukapewa. Lakini wafanyabiashara siku nyengine wanapewa hizi leseni, pengine hawa watu walikwishaugua maradhi ambayo hayafai ni kichaa ama pengine wana kasoro tofauti tofauti. Sasa mtu unampa

leseni hatima yake ndio kama hivi, tunasikia kule huyu anauziwa biashara huyu hauziwi. Sasa hebu tuone kwamba kuna elimu maalumu ambayo ya yule mfanyaji biashara kwanza akubali yale masharti ambayo yatatolewa pale na kuona kwamba yeye anachukua lile jukumu lakini akijua anafanya biashara yake lakini hana ubaguzi wa aina yoyote.

Ukija kwenye masuala ya wale wafanyabiashara wachuuzi wanaouza samaki kadhia ni kubwa, ukienda kwenye masoko ya samaki hali ni hiyo hiyo kwa wale ambao wananadisha samaki na ukija kwenye biashara nyengine za magari na mambo mengine hali imekuwa tete.Tutaendelea kusema siasa lakini hatuwasimamii majukumu yao sisi ambao tunawapa zile leseni au kuwawezesha katika kufanya zile biashara zao. Nikuombe Mhe. Waziri ukishirikiana na watendaji wako, najua wewe ni mzuri na wao ni wazuri hebu tuangalieni mambo mazuri ya kubuni, kwa sababu hii wizara najua ilishapangiwa mipango yake. Lakini si vibaya kuona kwamba mnabuni mambo mazuri ya kuwafanya wananchi na nyinyi kwa pamoja ile wizara ikazidi kuwa na changamoto ambazo ni nzuri kuepukana na zile za zamani.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea jana nilichangia kwa maandishi kwenye Wizara ya Afya kuhusiana na suala la *pampers*, kusema kweli sikupata kulizungumza kwa kina leo hapa kwa kuwa na hili ni suala la biashara na zinatoka mbali.

Juzi mimi na Mheshimiwa mwenzangu Nadir tulikwenda kule bandarini kulikuwa na baadhi ya mizigo fulani tunakwenda kusimamia. Kusema kweli mimi pale katika dakika ambazo nimekaa nimeona makontena zaidi ya matano sita, mimi fikra zangu tunaletewa tende kwa ajili ya Ramadhani. Kuja kufunguliwa ni *pampers* tupu, jamani *pampers* zinaleta maradhi ya mirupuko lakini vile vile ni hatarishi kwa matumizi ya halisi ya watoto wetu.

Wallahi laadhim mimi ninayesema hapa kuna siku tayari nimeshaifanyia uchunguzi *pampers* ile, na kama Mhe. Naibu Spika, utanipa muda japo mdogo niilete *pampers* mbele yako tuiangalie kwa pamoja basi sote tutagundua kama *pampers* zile hazifai kutumia watoto. Kama mtoto utamfunga *pampers* ile kwa muda wa masaa mawili ukimfungua, chululu yake kama ilikuwa ni nyeusi basi itakuwa rangi ya bluu. Kama ni nyeupe basi itakuwa rangi nyengine. Jambo ambalo wazee wetu wanajisahau wanazifunga *pampers* zile kuanzia asubuhi mpaka mtoto limvuke mwenyewe kwa uzito. Sasa hii hali kusema kweli ni nzito, kwa nini tusirudie yale mambo ya zamani watoto kufungwa nepi na mambo mengine. Pia zile inafanya wazee wetu kuona kwamba hawasimamii majukumu yao ipasavyo kuwaacha watoto wale kutowahudumia kila baada ya muda. Mtu anaona mimi nimvishe mwanangu *pampers* ndio inatosha, mtoto

analia anajikuna yeye kubwa atamuuliza una nini kumbe *pampers* limeshamtosha linamchuna.

Mimi niiombe wizara kuwa kupitia Wizara ya Afya washirikiane, jamani kuna baadhi ya mambo kweli tunafanya biashara tunahitaji pesa lakini tujue tunanunua maradhi tukiyaleta kwenye nchi yetu. Vile vile, ukiangalia kwenye hali halisi ya mfumo mzima wa mazingira hapa kuna kipindi kuna mifuko ile malboro. Mimi nakumbuka naenda skuli nachukua mfuko ule nafunga kijiti yupo hasa malboro hivi ukimuangalia unamuona na kama ile SUMA iliweza kukemewa na ilikuwa watu wanafanya biashara hapa hapa na ikatoweka, sasa hivi tumeingia na mifuko yetu ya kaki. Kwa hivyo na hizi zinahatarisha hali halisi ya mfumo mzima wa maradhi ya saratani na mambo mengine. Kwa hivyo, kuna haja hasa ya kuzikemea, kwa sababu sasa hivi unapopita popote basi utakutia ma-*pampers* yamejaa na kama utapita nyakati za usiku unaweza ukatishika ukasema jamani kuna nini mbona watu weupe namna ile kumbe ni marundiko ya *pampers*. Mhe. Waziri hili tatizo ni kubwa sana. Kwa hivyo, kuna haja ya kuliona hili mkalikemea.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea mara nyingi nitaonekana nikizungumza hilo kwa hilo lakini si vibaya. Kule Pemba ndani ya Jimbo langu la Tumbe kuna soko ambalo serikali ilitumia pesa nyingi sana ukubwa wake naweza nikasema linafikia hata hii nusu ya Baraza lako. Ndani ya soko lile kuna mkahawa, ndani ya soko lile kuna vyumba vya kupumzika kwa baadhi ya wafanyakazi, kuna sehemu ya kukoga ndani ya soko lile, kuna sehemu ya kufanya biashara kwa ajili ya duka, kuna sehemu za mkahawa kuuziwa chakula. Hizi zote ni sehemu ambazo zitatoa huduma kwa wananchi ambao wanakaa pale na kuifanya serikali kupata mapato. Lakini jambo la kushangaza soko lile lipo limekaa kama gofu la makumbusho ya kale halina linalofanyika.

Mhe. Naibu Spika, najua changamoto zipo za wananchi kama ilitokezea kadhia ya sintofahamu za kutokushirikiana, lakini ninavyojua mimi mtoto siku zote anapomtia mzazi wake kinyesi kwenye mwili, basi mwili ule haukatwi unapanguswa na watu wanaendelea na shughuli zao kama kawaida. Kwa hiyo, hawa ni wananchi ambao labda ilitokea kadhia ama changamoto fulani juu ya serikali, lakini tuone tunachukua juhudi za makusudi kuona soko lile linatumika na hali halisi ambayo ilitegemewa kufanyika pale iwe inafanyika.

Kwa hiyo, nimuombe Mhe. Waziri lile soko tushirikiane pamoja na Wizara ya Uvuvi twende kule tukaseme nao wale watu, ili muweze kutoa mikakati maalumu kuona lile soko linatumika, lengo sio kukaa pale Tumbe watu wakaanza kuangalia tu kama sehemu za minara ya maonesho. Lengo ni

kufanikisha wavuvi wauze samaki wao, pia tukizingatia kama kwenye kuuza samaki basi vile vile hali halisi ya afya zitakuwa nzuri, kwa sababu samaki wanauzwa katika sehemu nzuri, ukilinganisha kuna baadhi ya watoto wetu wanajisaidia ovyo ovyo. Kwa hiyo, samaki wakiuzwa pale wewe utapata kufaidika.

Vile vile, hawa wavuvi wa jimbo langu mimi nataka niseme kitu kimoja kwamba wamejisahau kiasi fulani, kwa sababu pale samaki wale waliokwenda wavua kama itafika Magharibi hawajapata soko kuna sehemu ambazo zilitengwa kwa ajili ya kuweka samaki, ili siku ya pili mnada ule uendelee, leo soko limekaa halitumiki wala halifanyi lolote. Kwa hiyo, nikuombe Mhe. Waziri ukishirikiana na watendaji wako ambao wako Pemba tushirikiane ili twende tukaone lile soko kama linapata huduma zake kama ilivyopangiwa.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea mwenzangu aligusia suala la ukulima wa pilipili. Pilipili kusema kweli ni zao kubwa sana tena lenye kuongezea kipato, kwa hiyo tuliangalieni kwa macho mawili suala hili la ukulima wa pilipili. Suala hili ni moja ambalo litailetea faida serikali na wananchi watapata kufaidika.

Hapo zamani mimi nakumbuka pale nyumbani kuna mzazi wangu alikuwa na mipilipili kama minne au mitano sasa hivi imekufa kusema ukweli. Lakini nataka niseme kwamba pilipili zile nilikuwa nakwenda kuzichuma mimi mwenyewe binafsi, ndani ya mwaka nadhani inazaa kama mara tatu na ikizaa haina kinyongo mipilipili. Pilipili ambayo inatoka ndani ya kisiwa chetu cha Pemba pamoja na Unguja basi kwanza ina harufu nzuri zaidi na pia ni kali kuwasha kwake. Kwa hiyo, tuangalieni wenzetu ambao wanalima zao la hiliki, hiliki sasa hivi kilo moja nafikiri ni shilingi 35,000. Sasa na sisi kama watu wataendelea kulima hizi pilipili basi hali halisi ya kipato kwa wananchi pamoja na serikali kitapatikana, kwa sababu kwanza mpilipili hauna kinyongo.

Mhe. Naibu Spika, upandaji wa mpilipili ni mche ule ule wa mpilipili ambao umetambaa chini unaung'oa ukiwa na mizizi unaufunga. Vile vile unaupandia mjiti tu wa kuweza kwamba ule mjiti unaendelea kusimama, kuna mijiti yake maalumu unaisimamishia kwenye mashimo na kuitilia maji baada ya siku mbili inakubali inakuja zake. Kwa hiyo, hebu tulione hili suala la ulimaji wa pilipili tunaliboresha ili wakulima waweze kupata pesa na kuzidi kuongeza kipato kwa serikali.

Mhe. Naibu Spika, mimi nikiendelea kwenye wajasiriamali. Kule Pemba sasa hivi tunao wakulima wetu…

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa umebakisha dakika tatu.

Mhe. Ali Khamis Bakari: Haya namalizia Mhe. Naibu Spika, dakika mbili *in shaa Allah* zitanitosha.

Kuna wakulima wajasiriamali ambao wamejitokeza kwa kubuni kuhusiana na habari ya makumbi wanaweza kusuka kamba. Kwa hiyo, makumbi tunayo, minazi tunayo, kwa nini tusione wakulima wale wadogo wadogo tukawawezesha wakazidi kupata kipato zaidi na kuiendeleza ile biashara ambayo wameiandaa, na serikali vile vile ikawaboresha kwa ajili ya kuliweka soko au kuwawekea sehemu maalumu au kiwanda kwa ajili ya kuona kamba zile zinatengenezwa hapa hapa na sisi tunaweza kupata kipato.

Sasa hivi tumeona ukulima wa mwani lazima watu wapate kamba, tunaagizia kamba kutoka nje, tunaagizia kila kitu kutoka nje lakini kumbe tuna mambo tukiweza kuyabuni hapa tunaweza tukapata pesa sisi wenyewe na kuonekana kwamba Zanzibar ina mfumo wake maalumu wa kuweza kubuni baadhi ya biashara ndogo ndogo na kuwaongezea wananchi wake kipato na wakapata kujikwamua na matatizo madogo madogo.

Mhe. Naibu Spika, halikadhalika kuna na mapolo sasa hivi haya ambayo yanatolewa mchele vile vile kuna watu wanayaboresha kufanya kamba na kuweza kutumia kwa shughuli zao ndogo ndogo. Mhe. Waziri na hili nalo tuliangalieni kwa macho mawili, kuona kwamba kunawekwa angalau viwanda kule Pemba japo hivi vya masuala haya ya utengenezaji wa hizi kamba kwa kutumia usumba.

Ni jambo zuri sana na wazungu hasa wanafurahia humo kwenye mahoteli ukienda kwenye vitanda ambavyo vimetengenezwa basi vingi utavikutia vimefungwa kwa kamba zile za kutumia makumbi.

Mhe. Naibu Spika, ulinambia muda wangu ni mdogo, ninayo mengi kidogo lakini kwa vile muda hautoshi *in shaa Allah* mengine nitachangia kwa maandishi, naiunga mkono hotuba hii asilimia mia moja, *in shaa Allah*.

Mhe. Abdalla Ali Kombo: Mhe. Naibu Spika, kwanza naunga mkono hoja mia kwa mia sina tatizo nayo, leo kwangu ni ushauri na tahadhari basi.

Mhe. Naibu Spika,...

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa samahani kidogo. Waheshimiwa Wajumbe, mnapokuwa na mchango wa maandishi tulikubaliana hapa kwamba ipite kwangu michango ili mimi niweze kuisajili nani na nani kachangia, kwa sababu tunaipeleka chini pale wakati wa kupiga buti, kwa hiyo, tujue nani kachangia kwa maandishi. Kwa hiyo, nawaomba sana ipite kwangu halafu ndio mimi nampelekea Waziri. Ahsante endelea Mheshimiwa.

Mhe. Abdalla Ali Kombo: Mhe. Naibu Spika, nataka kumjuilisha Mhe. Waziri kwamba yeye wizara yake ndio wizara wezeshi ya mambo ya viwanda. Sasa ningependa tu kumuuliza Mhe. Waziri amejiandaaje ama anashirikiana vipi na sekta saidizi. Kwa mfano, Wizara ya Kilimo na Mifugo na sekta nyengine, wasi wasi wangu mkubwa kwa zile sekta saidizi hasa Wizara ya Kilimo na yeye mwenyewe amesema kwamba kuna wafanyabiashara juzi wamekwenda na watakwenda kwenye maonesho ya biashara Dar es Salaam. Wengi wa wafanyabiashara wetu wanajihusisha na biashara ya *spice*, lakini wasi wasi wangu kwa biashara hii kwa Unguja na Pemba sasa hivi hizi *spices* sijui kama ameshazungumza na Wizara ya Kilimo na *private sectors* kwamba zipo na muda unakwenda.

Mhe. Naibu Spika, unajua sisi watu wa Unguja na Pemba ni watu wa kujisifu, simkanyagi Mjumbe aliyepita kwamba karafuu yetu nzuri, hiliki yetu nzuri kila kitu chetu sisi kizuri tu lakini hatuna.

Tahadhari ambayo nataka kuitoa hapa sasa hivi Tanzania Bara na hasa Morogoro maeneo ya Kinole juu wanalima karafuu nyingi sana, na *spices* za aina zote wenzetu wanazilima sasa hivi. Sisi tunabakia kwamba yetu nzuri, yetu nzuri, wewe una nusu polo mwenzako ana polo 30. Sawa na iwe harufu nzuri, tamu lakini una nusu polo mwenzako ana polo 30, na mbaya zaidi hapo tunapokwenda sijui Mwenyezi Mungu atusaidie wasije wakaweka hata ile alama ya kwamba inatoka Zanzibar. Kwa hivyo, hiyo ni tahadhari.

Mhe. Naibu Spika, nakuja kwenye *vanilla*. *Vanilla* sasa hivi Bukoba ukiacha ndizi ni zao la biashara. Kilo ya *vanilla* sasa hivi Bukoba ni karibu shilingi 80,000, watu hawa wote wa Morogoro na Tanga wamechukua miche yetu kutoka Zanzibar, lakini sisi wenyewe tumebakia tu *Zanzibar Island*, *Spice Island* na kujisifu tu lakini hatuna kitu. Kwa hivyo, hiyo Mheshimiwa ni tahadhari, majisifu yetu yafike pahala tujue nini tunakifanya.

Kwa hiyo, namuomba Mhe. Waziri wa Biashara ayajue haya mambo kwamba tunajisifu lakini wenzetu wanayo na hawako masafa marefu. Tusije tukapiga kelele kama Kenya, Kilimanjaro sijui nini tayari wenzetu na nadhani sina

uhakika hali ya hewa ya Morogoro juu ya milima ni nzuri zaidi kuliko Zanzibar. Hilo la kwanza.

Mhe. Naibu Spika, jambo la pili naomba ufafanuzi zaidi kwa Mhe. Waziri wa Biashara kwenye kitabu chake ukurasa wa 15 alisema uzalishaji wa sukari unaimarika.

Ninachofahamu mimi kinachoimarika sasa hivi Mahonda kiwandani ni uharibifu wa miwa, hatuchukui mwezi, miezi mitatu tunasikia miwa imeshakatwa. Sasa hapa kidogo nataka ufafanuzi unaimarika uzalishaji wa miwa au uzalishaji wa matatizo.

Mhe. Naibu Spika, na halafu ikiwezekana kama uzalishaji unaongezeka, akija basi atutajie takwimu za mwaka 2013/2014 kuonesha dhahiri kwamba huu uzalishaji unaongezeka.

Mhe. Naibu Spika, kuhusiana na kadhia ya Kiwanda cha Mahonda hasa kuhusu uharibifu, ningemuomba Mhe. Waziri wa Biashara akakaa na Wizara ya Kilimo, akakaa na Wizara ya Tawala za Mikoa, akakaa na Wizara ya Uwezeshaji pamoja na wananchi wa Kaskazini "A" na "B".

Uharibifu wa Mahonda unaonekana dhahiri kwamba sio wa siasa kama ule wa Pemba na sehemu nyengine. Ni uharibifu unaotokana inawezekana na ukosefu wa kazi kwamba wenyeji labda hawapati kazi, ama wenyeji wana tatizo fulani. Kwa hiyo, ningemuomba Waziri wa Biashara akakaa na wizara hii wakafikia pahala wakaulizana tatizo ni nini. Lakini pia Mahonda ninachofahamu mimi kuna Mwakilishi ambaye ana *influence* kubwa sana kwa wananchi, pia na yeye mngemwita mkakaa pamoja. Hii tusichukue tena muda wa kuja kungojea imekatwa, imechomwa, aah, tukaeni pamoja tujue wananchi wanachokitaka, najua lazima kutakuwa na kitu wanakigombania. Kwa hiyo, nakuomba sana Mhe. Waziri.

Mhe. Naibu Spika, ningemuomba Mhe. Waziri atapokuja atusaidie gharama hasa za uzalishaji wa mwani kwa eka, kutoka *land preparation* mpaka *harvesting* yaani vijiti, mishipi, uvunaji, vyote. Nauliza haya kwa sababu tupate jibu na baadae tuwaambie wakulima kuna nini, hawa matajiri sio wapuuzi kuteremsha bei mia saba mpaka mia tatu, wanajua kitu ambacho kipo. Sasa atuletee gharama hizi tujue kuwaambia wananchi wetu jamani eeh hawa watu kuna kadha, kadha. Tukishakuijua bei au tujue chochote na pia ningemuomba Mhe. Waziri na yeye pia atupe ushauri wake ili tujue kuna nini.

Mhe. Naibu Spika, mwisho nadhani kilimo cha mwani ni somo tosha kwa wale watu wanaojishughulisha na kilimo cha karafuu kusema kwamba karafuu iende kwa watu binafsi. Nina uhakika na karafuu hivyo hivyo kama bei itateremka, kwa maana hiyo na wanunuzi walio binafsi nao bei ya karafuu watateremsha. Kwa hivyo, nadhani hili liwe somo. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Naibu Spika, na mimi nakushukuru kunipa nafasi hii kuweza kutoa mchango wangu wa mawazo katika hotuba hii ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko aliyowasilisha Mhe. Amina Salum Ali.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nataka ni-*acknowledge* Mhe. Waziri wa Biashara mimi amenisaidia sana kuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi, na inawezekana yeye mwenyewe amesahau, lakini kwa kweli katika watu ambao alinipa chachu kubwa sana ya kuingia katika Baraza la Wawakilishi ni yeye, kipindi hicho niko Umoja wa Vijana na yeye akiwa Kamanda wa Umoja wa Vijana wa Wilaya ya Mjini. Mhe. Amina nakushukuru sana kwa msaada wako na naamini tutaweza kushirikiana zaidi huko mbele.

Mhe. Naibu Spika, nataka nimpongeze sana Mhe. Waziri katika kipindi kifupi ameweza kuandaa bajeti yake ambayo ina takwimu za kutosha, na mimi Mhe. Waziri nimempandisha daraja namwita wa kimataifa, kwa sababu sio wa Kitanzania Tanzania, ni wa kimataifa. Kwa hiyo, tunategemea ndani ya miaka mitano atatuletea mawazo sio ya kuangalia tu uchumi wa Zanzibar kwa ndani ya Zanzibar na Tanzania. Atatumia uzoefu wake, ujuzi wake, utaalamu wake na maarifa yake katika kuhakikisha kwamba anawaondoa wafanyabiashara wa Zanzibar kutoka hapa walipo na kuwasogeza katika hiyo anga ya biashara za kimataifa.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nataka niipongeze sana Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya uongozi wa Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kuendelea kuwaonea huruma wananchi na kutokuongeza kodi katika bidhaa za vyakula kwa hapa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli hiyo mimi nasema kwa Dkt. Shein ni *sadakatul-jaria* kwa wananchi wake, na naomba sana serikali iendelee kutupa nafuu ili kuweza wananchi wetu kuishi katika maisha yaliyokuwa nafuu.

Mhe. Naibu Spika, lakini la pili nataka niwapongeze sana wajasiriamali wote wa Zanzibar. Mhe. Naibu Spika, katika hiki kipindi kifupi hasa katika ndani ya mwaka huu ambao tuliokuwa nao 2015/2016 kwa kweli wafanyabiashara wetu

wajasiriamali wadogo wadogo hasa wale wanaofanya biashara za vyakula na zile za maji maji wamepata athari kubwa sana kutokana na maradhi ya kipindupindu, na kwa kweli kitu ambacho nawasikitikia sana. Wanaingia katika mwezi mtukufu wa Ramadhani na wanakwenda wakati wa sikukuu wakiwa hawana kitu mkononi. Biashara zao zimefungwa, na mimi nawaomba tu wafanyabiashara wetu hawa wajasiriamali wawe wastahamilivu, haya kwa kweli ni mipango ya Mwenyezi Mungu, lakini kikubwa zaidi tuwaombe wananchi kuimarisha usafi, kuhakikisha kwamba wanafuata ile miiko ya usafi ili kipindupindu kiondoke. Ndugu zetu hawa waweze kufanya shughuli zao za biashara ndogo ndogo ili wapate kujiongezea kipato.

Mhe. Naibu Spika, nataka niingie katika mchango wangu zaidi wa mawazo kwa wafanyabiashara. Mimi nataka niwapongeze sana wafanyabiashara hasa wanaoleta vyakula hapa Zanzibar.

Mhe. Waziri ameeleza katika hiki kitabu kwamba pamoja na mambo yote yanayojitokeza, lakini bado vyakula vipo ndani ya nchi na kwa kweli hali inaridhisha. Naomba niwape moyo sana waendelee kuleta vyakula watuuzie wananchi, lakini bado watuuzie katika bei ambayo iliyokuwa nafuu. Nimejaribu kuangalia kitabu cha Mhe. Waziri hapa katika bei ya vyakula, kwenye ukurasa wa 12 na 13. Ukiangalia takwimu za bei ya vyakula zilizoandikwa hapa ni tofauti na bei ambazo tunazouziwa huko madukani. Sasa hili namuomba Mhe. Waziri wale watendaji wake ambao wanasimamia sekta hii ya mwenendo wa bei, wajaribu kurudi tena katika masoko ili wananchi wetu wapate ile nafuu ambayo serikali yetu ilikusudia.

Mhe. Naibu Spika, lakini jengine namuomba sana Mhe. Waziri kuna mwenzangu mmoja hapa alizungumza Mhe. Amina ni mtu jasiri sana. Mhe. Waziri ambaye asiyekuwa na Waziri Maalum Mhe. Ali Khatib na ni kweli anayemjua Mhe. Amina hebu aende kwenye *hansard* katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania atamjua nani Mhe. Amina Salum Ali ambaye sasa hivi ni Waziri wa Biashara. Nilikuwa naomba suala moja alifuatilie.

Mhe. Naibu Spika, hivi sasa ninavyozungumza kuna makontena mengi ya wafanyabiashara wa Zanzibar yamekwama katika bandari ya Dar es Salaam. Kwa kweli Mhe. Naibu Spika, wafanyabiashara hawa fedha tunajua wanavyozipata wanakopa katika mabenki, mabenki kuna riba, leo kontena inakaa miezi mitatu katika bandari ya Dar es Salaam, kwa kweli *this is unfair*.

Sasa mimi naomba Mhe. Naibu spika Mhe. Waziri wetu wa Biashara, kwa sababu mimi namjua ni mjasiri ambaye anaweza kujenga hoja na hili tatizo

likaweza kuondoka. Tunaishukuru serikali yetu kwa kutoa tamko kwa Waziri wa Fedha kwamba katika mwaka huu kuanzia Julai 1 zile *differences* za ushuru wa magari kwenda Bara italipwa hapa Zanzibar, lile kwa kweli nalipongeza sana, itasaidia kuongeza mapato kwa Zanzibar lakini vile vile itaendelea kuondoa usumbufu kwa wafanyabiashara wetu hasa wanaopeleka magari kule Dar es Salaam.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli bado narejea tena suala la makontena yaliyokwama Dar es Salaama, mengine makontena yana tende, tulitegemea tuzipate mwezi huu mtukufu wa Ramadhani tumezikosa, muna nguo mule zinatakiwa kwa ajili ya Sikukuu, kwa hiyo wafanyabiashara kwa kweli wamekaa wanakunja mikono kwa kweli wanapata hasara kubwa sana. Hili nilikuwa naomba Mhe. Waziri alichukulie hatua za haraka, aangalie nini cha kufanya ili makontena yatakayoshuka Dar-es-Salaam yawe *very smooth* yanatoka Dar-es-Salaam yanakuja zake hapa ili wafanyabiashara wetu wasipate matatizo.

Mhe. Naibu Spika, nazungumzia suala la Bandari ya Mpigaduri. Tunaishukuru sana serikali yetu. Mradi huu wa Bandari ya Mpigaduri ninavyokumbuka umepelekwa mpaka katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, lakini tulikosa *support*, sasa hebu naomba Mhe. Waziri, najua kwamba ni mpya, ameingia juzi, sijui kama ameshashiriki katika vikao vya Afrika Mashariki vinavyozungumzia miradi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Wenzetu zimejengwa barabara, Holili, Horohoro, sijui wapi huko kuunganisha baina ya nchi; Kenya na Uganda na wapi, katika miradi ya kuunganisha Jumuiya ya Afrika Mashariki. Lakini leo tumekosa *support* ya Afrika Mashariki, na leo Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inahangaika wao wenyewe kutafuta wafadhili wa ujenzi wa Bandari ya Mpigaduri. Sasa nilikuwa naomba tu Mhe. Waziri, je huu mradi wa Bandari ya Mpigaduri katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, kuna mpango gani ambao wa kuweza ku-*support*.

Mhe. Naibu Spika, lakini vile vile kuna mradi ule wa *roll on* na *roll off*, ambao ndio ulikuwa mradi pekee wa Zanzibar, ambao kungelijengwa bandari kavu ambapo hizi boti au mameli ambayo yatakayokuwa yanawasafirisha wafanyabiashara na magari yao kwenda katika nchi za Afrika Mashariki na kurudi siku hiyo, mradi huu sijui umefikia wapi.

Mhe. Naibu Spika, vile vile katika suala zima la uwekezaji. Bado Zanzibar tuna tatizo la urasimu wa wafanyabiashara wetu hasa wanapotaka kuwekeza. Naomba sana Mhe. Waziri wa Biashara, kwa kushirikiana na Mhe. Waziri wa

Ardhi pamoja na Mhe. Waziri wa Fedha, kuna muwekezaji mmoja Mzanzibari Mzalendo ameamua kufanya mradi wa aina yake wa ujenzi wa chelezo hapa Zanzibar katika eneo la Mangapwani; ameshafanya *EIA* katika eneo lile, *EIA* iko vizuri, amelipa *compensation* vizuri lakini mpaka leo hati ya ardhi bado hajapewa, na mwananchi yule kwa kweli ameshatumia fedha nyingi, anaendelea kuwa mjasiri, ame-*invest* fedha nyingi, lakini bado serikali inamkwamisha.

Mhe. Naibu Spika, hili nilikuwa naomba Waheshimiwa Mawaziri watatu hawa; Mhe. Waziri wa Biashara, Mhe. Waziri wa Ardhi na Mhe. Waziri wa Fedha waje wakae pamoja kuangalia muwekezaji yule wataweza kumsaidia vipi.
Mhe. Naibu Spika, nilikuwa pia nataka nijue hawa wafanyabiashara wetu ambao ni *small and medium enterprises*. *BoT* wana fedha pale kwa ajili ya kusaidia wafanyabiashara wadogo wadogo pamoja na wakati ambao ndio hawa wanaoitwa *small and medium enterprises*.

Wenzetu Tanzania Bara wamefaidika sana na fedha hizi, wanaweza kupewa *grant* karibu bilioni nne kwa ajili ya kuwekeza aidha viwanda au miradi mingine, sijui kwa hapa Zanzibar sisi tumeweza kufaidika vipi. Wenzetu Rwanda Mhe. Naibu Spika, mfumo huu wanao, mwekezaji anapokwenda pale kuna *funds* zimewekwa na serikali kama *catalyst* ya kuweza kuwa-*support* wafanyabiashara au wawekezaji wanaotaka kuwekeza katika nchi ya Rwanda, wenzetu wanatumia *BoT* kupitia *SME* lakini hapa Zanzibar hili suala naona hatujafanikiwa.

Mhe. Naibu Spika, kuna suala moja ambalo bado nitaendelea kulisema, suala la serikali yetu kuruhusu kuletwa makuku na sasa hivi yanaletwa masamaki. Hii ni kurejesha nyuma wafugaji wetu na wavuvi wetu. Bado ninaendelea tena, leo ukitoka hapo nje ya Baraza la Wawakilishi utakuta tayari wachuuzi badala ya kwenda huko Fumba na sehemu nyengine kwenda kuwafata wavuvi ambao wamevua samaki *fresh* leo wanafukuzana hapa Chukwani mbele kidogo ya Baraza la Wawakilishi na masusu yao wanakwenda kutuletea samaki waliokaa huko kwao zaidi ya mwaka mmoja na nusu uliopita, leo ndio tunakwenda kutowelea futari, baada ya kujenga afya zetu sasa hivi afya zetu zinaendelea kuporomoka kwa ajili ya kununua haya makuku na masamaki ambayo yameshapitwa na wakati.

Mhe. Naibu Spika, pia nilikuwa naomba Mhe. Waziri, awasaidie ma-*supplier* katika mahoteli mbali mbali ya Zanzibar. Leo wananchi wetu wengi katika suala zima la ku-*support* uwekezaji wamejiajiri katika sekta ya *supplying*, wanapeleka bidhaa mbali mbali ikiwemo samaki na vitu vyengine katika

mahoteli mbali mbali, lakini baadhi ya mahoteli kwa kweli wamekuwa wakorofi, wanakaa miezi sita watu hawajalipwa, wengine mpaka mahoteli yanafungwa ma-*supplier* wale walifika mpaka serikalini kwa Makamo wa Pili wa Rais ili kuweza kupatiwa malipo yao, na wengine mpaka leo wameshindwa kupata haki zao akiwemo mwekezaji wa hoteli ya Venta Club.

Kwa kweli naomba Mhe. Waziri, akae na wafanyabiashara wenye mahoteli ili kuangalia wale ma-*supplier* waweze kulipwa kwa wakati.

Mhe. Naibu Spika, lakini pia nilikuwa naomba Mhe. Waziri, afanye utafiti wa kutosha kuangalia vurugu zinazotokezea katika mashariki ya kati iwe ni fursa kwa Zanzibar kuwa ni kivutio kikubwa cha biashara kwa hapa kwetu. Kama nilivyosema Mhe. Waziri yeye ni wa kimataifa, anaweza akaangalia ni namna gani ataweza kuhamasisha wawekezaji mbali mbali duniani hasa ambao waliokuwa wanawekeza katika Falme za Kiarabu waje Zanzibar kuja kuwekeza na mazingira yawe mazuri.

Mhe. Naibu Spika, nimejaribu kuangalia katika kitabu cha Mhe. Waziri, ukurasa wa 7. Ukurasa wa 7 imeelezwa bidhaa ambazo zinazosafirishwa na zinazoagizwa katika nchi za Ulaya, Asia na Afrika, kwa kweli tuko mbali kweli kweli na tutaendelea kuwa mbali. Maana yake wenzetu wanasafirisha bidhaa karibu 5,000 sisi ndio kwanza tuko 338, sasa hebu angalia *gape* baina ya Afrika na Ulaya kwa kweli tuko mbali sana. Sasa hiyo nazungumza kwa Afrika, kwa Zanzibar sisi ndio tuko mbali zaidi.

Mhe.Naibu Spika, lakini jengine nilikuwa ninamuomba, Mhe. Abdalla amezungumza vizuri suala la mwekezaji wetu wa kiwanda cha sukari pale Mahonda.

Hili suala liko *very sensitive*, mwekezaji yule sisi ilikuwa tufanye jitihada zote, tumpe *support*, tumpe moyo ili na wawekezaji wengine waje hapa Zanzibar. Lakini leo kuna mambo madogo madogo kama alivyosema Mhe. Abdalla Ali siyo mambo ya kisiasa ni mambo ya kijamii, viongozi wetu wakae na wananchi wa kule, wasimtie hasara mwekezaji yule.

Mhe. Naibu Spika, wenzetu Mauritius uchumi wao asilimia kubwa unaendeshwa na mapato ya miwa, leo sisi Zanzibar leo kuna kiwanda kimoja tu. Mimi nilitegemea kwamba kiwanda kile kilikuwa kiwe na uzalishaji mkubwa halafu ukiacha lile shamba la Mahonda katika maeneo mengine yenye mabonde ambayo yanaweza kulimwa miwa wananchi wahamasishwe walime miwa ili waende wakamuuzie mwenye kiwanda kile cha Mahonda. Sasa leo

baada ya kiwanda kukisimamia vizuri kifanye kazi vizuri leo kila siku utasikia miwa imechomwa, sijui nini kimefanyika hivi, kwa kweli haituletei raha na ninamuomba Mhe. Waziri azungumze na mwekezaji wa kiwanda cha sukari cha Mahonda, kama anaweza kuzalisha zaidi basi atafute au tutafute maeneo mengine ambayo wananchi tuwahamasishe walime miwa ili waende wakamuuzie katika kiwanda kile cha sukari.

Mhe. Naibu Spika, leo tunaambiwa Tanzania Bara soko la sukari lipo jingi sana, kwa hivyo mwekezaji yule anaweza akazalisha sukari na wananchi wetu wakapata ajira kupitia ukulima wa miwa katika maeneo yao mbali mbali, ambao wenzetu hata kule maeneo ya Mwanza kule, huku Kilombero wanafanya utaratibu huo, hata Uganda mwekezaji ana kiwanda lakini wananchi wao ndio wanalima miwa wanakwenda kumuuzia mwenye kiwanda. Kwa hiyo wananchi wale wanapata ajira ya uhakika, wanafanya kilimo cha uhakika, anajua nikilima miwa soko tayari lipo.

Mhe. Naibu Spika, nilikuwa tu nataka maelezo kidogo katika ukurasa wa tisa. Katika biashara ambayo imefanyika Tanzania na nchi za nje India kwa kweli imechukua nafasi kubwa. Lakini pamoja na kwamba imechukua nafasi kubwa karibu asilimia hamsini ya usafirishaji wa bidhaa zetu zinakwenda India, labda Mhe. Waziri, alikuwa aje atwambie ni bidhaa gani ambazo tunazosafirisha kiasi kama hicho.

Mhe. Naibu Spika, lakini vile vile kuna *gape* hapa, kutoka 2014/2015 India tuliuza karibu 63 milioni lakini mwaka 2015 tumeuza 21 milioni, sasa hebu nilikuwa nataka nijue kuna tafauti gani, bidhaa gani tunazosafirisha na kwa nini tukaweza kushuka kwa kiasi kikubwa kama hicho.

Mhe. Naibu Spika, vile vile katika bidhaa zinazosafirishwa kupelekwa Tanzania Bara ukurasa wa 10 hapa tumeelezwa kwamba tumeweza kuagiza bidhaa za milioni 95 kutoka Tanzania Bara lakini sisi tumejaribu kusafirisha karibu bidhaa za milioni 401. Hili kwa kuliangalia kwa haraka haraka utaona labda Zanzibar tuna uzalishaji mkubwa sana, lakini kwa bahati nilipoangalia kwenye kitabu kule mbele wamesema kwamba bidhaa tunazosafirisha kupeleka Tanzania Bara ni zile ambazo zinazozalishwa Zanzibar na zile zinazotoka nje ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, sasa hapa nilikuwa naomba tu Mhe. Waziri, mwakani katika kitabu chake hii *figure* asituletee pamoja, kwa sababu itatudanganya na itatulemaza, tutaona kwamba labda tunasafirisha kwa wingi kumbe vile bidhaa tunazosafirisha nyingi zinatoka nje ya nchi inakuwa kama ni *transshipment*.

Sasa nilikuwa ninaomba mwakani atakapokuja kuleta takwimu zake atuletee bidhaa tulizosafirisha Zanzibar kupeleka Tanzania Bara, na vile vile bidhaa ambazo zinazotoka nje ya nchi tukapeleka Tanzania Bara, na kwa kuwa sasa hivi Wizara ya Fedha ya Jamhuri ya Muungano na Zanzibar tumeshakubaliana kwamba bidhaa zinazotengenezwa Zanzibar kodi zake zitalipwa katika kile kituo cha mlaji, sasa bidhaa za Zanzibar zitalipiwa kodi Bara na bidhaa za Bara zitalipiwa kodi Zanzibar. Kwa hiyo hii tutapata kujua ile *difference* ya uzalishaji wetu.

Mhe. Naibu Spika, soko la mwani ukurasa wa 14 Mhe. Abdalla Ali Kombo amelizungumza, lakini na mimi nitalizungumza katika muelekeo mwengine. Juzi Mhe. Waziri wa Kilimo, alipokuwa akijinasibu, alipokuwa akichukua *floor* aligaragara sana hapa, na kwa kweli tulimpigia makofi sana kwa sababu maneno yake kama angelikuwa ndio vile ambavyo alivyosema yatatekelezwa au ataweza kuyatekeleza kama vile, kwa kweli tungelipiga hatua kubwa sana.

Mhe. Naibu Spika, nilikuwa nataka nijue Waziri wa Kilimo juzi alitwambia amepata soko kubwa sana la mwani Afrika ya Kusini, lakini katika kitabu cha Mhe. Waziri wa Biashara, sijaona lile soko la mwani ambalo ni kubwa sana kutoka kule Afrika ya Kusini ambalo Mhe. Waziri wa Kilimo alisema lingeliweza kuondoa bei ya mwani kutoka hii ya sasa hivi bei ya Shilingi elfu tatu mpaka ikafika shilingi alfu saba na kuendelea, yaani bei karibu mara tatu. Sasa hili je sijui Waziri wa Kilimo alikuwa anajifurahisha tu au hili suala limeshafanyiwa utafiti; kwa sababu wakulima wa mwani wanasubiri jawabu kutoka kwa Mhe. Waziri muhusika, Mhe. Waziri wa Biashara.

Mhe. Naibu Spika, lakini vile vile hali ya viwanda vidogo vidogo tumeona hapa, viwanda kwa kweli vimekuwa vingi. Mimi nashukuru sana Mhe. Waziri aliposema wanaandaa utaratibu wa kuwafanya hivi viwanda vidogo vidogo kuvirasimisha kuviondoa katika *informal* kuja katika *formal*. Kwa kweli wananchi wetu wengi wanawekeza katika viwanda vidogo vidogo lakini bado hawana utaalamu, hawana uzoefu, lakini vile vile utaalamu na uzoefu ungeliwawezesha kuweza kutengeneza *capital* ambayo ingeliweza kuwasaidia katika ku-*push* vile viwanda vyao. Kwa hiyo kwa kweli hili nalipongeza lakini naomba masuala haya huko nyuma tumeshazungumza sana katika Wizara hii ya Biashara na Viwanda. Lakini naomba sasa itoke katika maneno iende katika utekelezaji.

Mhe. Naibu Spika, wenzetu Tanzania Bara kule kuna *SIDO* ina-*support* sana, viwanda vidogo vidogo...

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa malizia, nimekupa muda mrefu sana.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Haya namalizia Mhe. Naibu Spika. Kwa hiyo mimi nadhani ili nisichukue muda wako sana kwa heshima uliyonipa naomba niunge mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Lakini bado nilikuwa ninaomba *conflict* baina ya wananchi na mwekezaji wa kiwanda cha Mahonda hizi zisuluhishwe, lakini pia Mhe. Waziri aje atupe uzoefu wake kwa nini Mauritius uchumi wao unaendeshwa kwa miwa na wanatumia mbinu gani ili na sisi tuchukue mbinu zile tuzitumie kwa upande wa Zanzibar.

Baada ya hayo machache Mhe. Naibu Spika, nakushukuru naunga mkono hoja. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Hamza Hassan Juma. Mchangiaji anayefuata ni Mhe. Hassan Khamis *Diaspora*, baada ya Mhe. Hassan tuna mchangiaji Simai Mohamed Said, baada ya Mhe. Simai atakuja Mhe. Jaku Hashim na baada ya Mhe. Jaku Hashim ajitayarishe Mhe. Waziri Salama Aboud.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi Hassan Khamis Hafidh Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Welezo kwa kunipatia nafasi hii ya kuwa mchangiaji katika Wizara muhimu sana kwa maendeleo ya Wazanzibari wakwezi na wakulima wa nchi hii.

Mhe. Naibu Spika, kwanza napenda kuchukua fursa hii adhimu kutoka ndani ya moyo wangu kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kumteua Balozi Amina kuwa Waziri wa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar.

Kwa kweli mimi mwenyewe nilivyosikia jina limetajwa yeye ndiye waziri nilifurahi, kwa sababu nilijua ana uzoefu wa aina mbili, ana uzoefu wa ndani ana uzoefu wa nje, sasa wizara imepata mama atakayeweza kuilea na kuweza kuifikisha pahali inapotakiwa kufika. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, mimi *personally* namuelewa, nilikutana naye katika kiasi mikutano miwili nje ya nchi na siku moja tuko Marekani alitoa *speech* basi nilikuwa nimekaa na Mnaijeria, *is this from* Zanzibar, nikamwambia *yes, she is from Zanzibar and her name* is Bi. Amina. Kwa sababu kwa jinsi alivyoitoa *speech* ile, *speech* ilivyopangika, alivyokuwa anaiongea *speech* ile kwa umakini na kwa kujiamini kabisa, kwa hivyo Balozi Amina nakupongeza sana

na najua sasa wizara imepata mtu ambaye ataweza kuipeleka pahala inapotakiwa. (*Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, mchango wangu utakuwa unalenga au una shabaha moja tu ya kuwasaidia wananchi wa Zanzibar katika kupata maendeleo ya haraka kwa sababu wao ni wana mapinduzi na ni wakwezi na wakulima.

Mhe. Naibu Spika, sasa ninaanza, ukurasa wa 14 wa kitabu cha Mhe. Waziri unaelezea maendeleo ya viwanda, Mheshimiwa mimi hapa nina masikitiko makubwa. Zamani...

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa nakuomba kidogo ukae. Waheshimiwa Wajumbe nataka sasa hivi na kidogo nilikuwa nataka kubadilishana na Mhe. Mwenyekiti, ili aweze kumaliza na michango ya wizara hii. Lakini kabla ya kufanya hivyo naomba kutoa matangazo mawili.

La kwanza ni kwamba ile semina ambayo tuliyokuwa tuifanye tarehe 2 RasGas haitokuwepo tena Jumapili na badala yake itakuwa siku ya Jumanne baada ya kumaliza mswada wa sheria ya matumizi, hilo la kwanza. Lakini la pili nilikuwa naomba wajumbe baada ya kumaliza kikao wajumbe wa CCM wabakie hapa kuna mazungumzo ya muda mchache sana, ni hayo tu. Mhe. Mwenyekiti karibu.

Hapa Mhe. Mwenyekiti (Shehe Hamad Mattar) alikalia kiti

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa endelea.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Ahsante sana Mhe.Mwenyekiti, kwanza nakupongeza sana kwa kuchukua kiti. Sasa ninaanza, ukurasa wa 14 wa hotuba hii ya bajeti unaelezea maendeleo ya viwanda.

Mimi hapa nina masikitiko makubwa, hapo zamani kumbukumbu yangu nakumbuka kwamba Zanzibar kulikuwa kuna viwanda vingi, kulikuwa kuna kiwanda cha sigara, kulikuwa kuna Kiwanda cha Maziwa, Kiwanda cha Viatu, Kiwanda cha Samli, Kiwanda cha Madishi pale viwanda vidogo vidogo, palikuwa pana viwanda vingi ambavyo viwanda vyote hivi vilikuwa vinatoa ajira kwa vijana wetu Zanzibar, lakini leo viwanda hivi vyote wametokea wajanja, wengine wamevinunua, wengine wamevichukua, hatuoni tija yake katika kutoa ajira kwa vijana.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuchukua fursa hii kumuomba Mhe. Waziri, Zanzibar au dunia nzima kwa jumla vijana ni wengi na vijana hawana ajira. Kwa upande wa Zanzibar masikitiko ya vijana kukosa ajira yamekuwa ni mengi kiasi ambacho kama utakaa na kijana anavyosikitika machozi yatakutoka. Namuomba sana Mhe. Waziri atafute kila linalowezekana viwanda hivi vilivyokuwepo zamani basi viweze kurudi hapa Zanzibar, ili vitoe fursa ya ajira kwa vijana, tuanzie kwa vile vile vilivyokuwepo zamani tu, ili tuweze kutafuta viwanda vipya. Kabla ya kutafuta viwanda vipya tutafute vya zamani, viwepo, vitoe fursa kwa vijana. Hilo ni ombi Mhe. Waziri katika kutafuta kuwanusuru vijana kuingia katika mambo yasiyofaa.

Mhe. Mwenyekiti, mchango wa pili utakuwa ni ushindani wa kibiashara. Kabla sijatoa ushindani wa kibiashara naomba niseme mfanyabiashara ni nani. Nilipokuwa nachangia hotuba yangu ya bajeti ya Wizara ya Fedha nilisema mfanyabiashara naomba kila mtu anisikilize kwanza, mfanyabiashara ni mtu yeyote yule anayetafuta kupata faida, sasa nilisema wazi wazi kwamba mfanyabiashara hana dini, dini ya mfanyabiashara ni faida, na mfanyabiashara kitabu chake ni ghilba na udanganyifu.

Naomba nirudie, mfanyabiashara hana dini, dini yake ni faida, kitabu chake anachokifuata ni ghilba na udanganyifu. Naelewa kwamba nchi nyingi duniani zikiwemo nchi za Kiafrika zilihama kutoka Mfumo wa Ki-*socialist* zikenda katika Mfumo wa Ki-*capitalist*.

Mfumo wa Ki-*capitalist* ni *idea* ya Adam Smith kwamba *leave the business to regulate itself,* zitajipanga katika masuala yote ya *profit* na mambo mengine. Lakini nchi za wenzetu zilipohama katika mfumo huu hazikumuachia mfanyabiashara kufanya anavyotaka, baadhi ya nchi za Kiafrika baada ya kuhama katika mfumo huu tumemuachia mfanyabiashara anafanya anavyotaka. Mfano Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar leo hii mfanyabiashara wa mafuta ya petroli anaanza kuyaficha akayaweka mpaka siku anayotaka yeye akawasumbua wananchi, anawatesa kwa sababu anangoja bei ipande. Jambo kama hili nchi nyengine duniani halipo, lakini Zanzibar lipo na linatokea.

Mhe. Mwenyekiti, nilitoa mfano pale Darajani wauza mbatata walikubaliana tuuze mbatata kilo shilingi 2,000 akatokea mmoja akawa anauza mbatata kilo shilingi 1,500; wakajiuliza mbona anauza sana huyu kumbe anakwenda anauza shilingi 1,500 lakini usimtaje, walipogundua wakampiga. Hiyo yote ni kuonesha mfanyabiashara hana dini. Nilifanya utafiti nikagundua kumbe

zamani kulikuwa kuna Tume ya Bei, kazi yake kubwa ni kuzi-*monitor* bei na kuziwekea *regulation*, lakini leo nilipomuuliza swali hilo akasema Mhe. Waziri ipo idara inayoshughulika na mambo ya bei lakini mimi nahisi idara hii haifanyi kazi vizuri au haifanyi kazi zake ipasavyo. Kwa sababu mfumo wa bei Zanzibar upo *adhoc* unakwenda unavyotaka wenyewe.

Leo hii kunde, mbaazi, choroko kwa sababu ya Mwezi wa Ramadhani vimepanda bei huwezi kuamini, kwa sababu hakuna *monitoring agency* au hakuna tume ya bei inayoi-*regulate*. Sasa namuomba Mhe. Waziri aniambie je, kuna sheria hapa au sera inayoongoza hii mifumo ya bei na kumlinda mtumiaji? Kwa sababu watumiaji wa Zanzibar, wakwezi na wakulima wanapata shida sana jinsi ya vitu vinavyopanda bei siku hadi siku bila ya mpango. *Sometimes* utaona kama wafanyabiashara wa Zanzibar wanawakomoa wananchi, ambao wananchi wetu wote ni wanyonge lakini inabidi lazima tunuue bidhaa zile kwa sababu tunazihitaji na hatuna pengine pa kuzipata.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo nakwenda katika *SADC* na *EAC*. Mheshimiwa najua Tanzania ni mjumbe au ni mwanachama wa taasisi hii, na taasisi hizi lengo lake kuu ni kufanya biashara baina ya nchi na nchi. Lakini namuomba Mhe. Waziri wafanye utafiti wawahamasishe wananchi, wawaambie wananchi kwamba kuna *business opportunities* katika hizo nchi ili Wazanzibari nao wajikite waende wakafanye biashara katika hizo nchi.

Kwa mfano, andazi la Zanzibar kama litawekwa vizuri likiuzwa Burundi, Rwanda, Kenya wananchi wetu wataweza kupata ajira sana. Mhe. Mwenyekiti, naomba Mhe. Waziri aliangalie soko la nchi nyengine la *East Africa* ili Wazanzibari wafanyabiashara waweze ku-*penetrate* katika masoko hayo.

Mhe. Mwenyekiti, nakuja katika hoja nyengine ya bidhaa feki. Ni wazi kabisa Zanzibar ni miongoni mwa nchi duniani zinazoingizwa bidhaa feki kwa kiwango kikubwa. Ninashangaa kuna taasisi imeundwa kazi yake kufanya *regulation* ya hizi bidhaa lakini bado bidhaa feki, vyakula visivyokuwa na viwango vinaingizwa kwa kiwango kikubwa sana na vinatusababishia maafa na madhara tofauti hasa maradhi.

Mhe. Mwenyekiti, nachukua fursa hii kumuomba Mhe. Waziri namuamini sana, namjua anaweza, aliangalie jambo hili sana ili kuwalinda wananchi wetu wakwezi na wakulima wasipate athari ya maradhi kila siku yanayosababishwa na wafanyabiashara wanaoleta bidhaa feki nchi hii kwa sababu ya kupata faida.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Waziri pia aje kunijibu utaratibu gani wanaotumia katika kuziangalia au kuzi-*monitor* bidhaa feki hapa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, kuna wajasiriamali, katika watu ninaowapenda sana duniani wajasiriamali wa Zanzibar, wanajitahidi, wana bidhaa nzuri, lakini wanahitaji kusaidiwa kwa kiwango kikubwa wanafanya kazi nzuri. Namuomba Mhe. Waziri kwa vile yeye ni *International person,* ajitahidi awatafutie masoko nje, lakini kabla hatujawatafutia masoko nje tujitahidi kuwafanyia *good packaging* pamoja na *quality* za vitu ziwemo.

Nataka kutoa mfano, mbona Ghana, Cameroon nchi hizo zimeweza kuuza bidhaa zao masoko ya nje. Nchi kama Uingereza, Marekani na Canada kama wafanyabiashara wetu wanne tu wataweza kupata masoko hayo basi Zanzibar itafaidika kwa sababu wengine watakuwa wanauza kule na wengine wataajiriwa watakuwa wamepata ajira.

Mhe. Mwenyekiti, bidhaa ni nzuri lakini wizara ichukue juhudi ya makusudi kuwatafutia masoko ya nje, lakini waangalie *packaging* na *quality* ya bidhaa hizo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba kutoa wazo, kwa sababu Zanzibar bado hatuna *good regulation* za bidhaa katika mfumko wa bei umekuwa mbaya, naomba kusema bidhaa kama tungule, mihogo, viazi, bidhaa zote Zanzibar ziwe zinapimwa, mbona nchi za wenzetu zinapimwa kwa kutumia mezani ili kuweza kusimamia hizi bei isiwe zinapanda kwa kutaka mfanyabiashara, ukipanga fungu huwezi kuzi-*regulate* zile bei. Mfanyabiashara asubuhi akiamka anafanya anavyotaka yeye, hatuwezi kumfanya kitu, lakini itapokuwa tunapima taasisi hii inayoshughulika na bidhaa kupanda itaweza kabisa kufanya *regulation* za bei hizi.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Waziri akija hapa aniambie wanatumia utaratibu gani katika kupata *data* za bidhaa zinazoingia Zanzibar kwa mfano tungule, bidhaa zote zinazoingia Zanzibar utaratibu au mfumo gani wanatumia kupata *data*. Kwa sababu naona bidhaa ni nyingi lakini *data* hazipo za kutosha.

Mhe. Mwenyekiti, kwa leo sina mengi lakini nimuombe sana Mhe. Waziri kwamba ana wizara muhimu kwa maendeleo na maslahi ya Wazanzibari, Wanamapinduzi, Wakwezi na Wakulima. Lakini bado wizara mimi kama unaniuliza naihisi haijalala lakini bado inasinzia. Namuomba sana, namuamini sana waziri aliyepewa wizara hii ni waziri jembe ana sifa za *International*

person. Mhe. Waziri namuomba sana wizara hii aisimamie ili wananchi wetu wapate manufaa.

Mhe. Mwenyekiti, wafanyabiashara duniani kote wana sifa moja tu ya kutopenda wananchi, wanapenda faida. Kwa hiyo, namuomba sana Mhe. Waziri aangalie wafanyabiashara wasipende faida bali wapende na wananchi, wafanyiwe *regulation*, *otherwise* watatuharibia wananchi wetu wanawaongezea bei zisizokuwa na mpango.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo machache naomba sana kuunga mkono bajeti hii kwa asilimia 91 na asilimia tisa(9) naweka mpaka ataponijibu maswali yangu. Ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Simai Mohamed Said: Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona na mimi. Nianze kwanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu na pia kwa niaba ya wananchi wangu wa jimbo la Tunguu nichukue fursa hii pia kumpongeza rafiki yangu, dada yetu, mama yetu, Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko kwa kuteuliwa katika wizara hii.

Pia, niseme kwamba ni jambo kubwa kwa akina mama kwa sababu Mhe. Waziri alikuwa kagombea katika kinyang'anyiro cha Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na katika historia aliyoiweka katika nchi yetu na Chama cha Mapinduzi ni mama pekee aliyeweza kufika sio katika wagombea wote waliochukua fomu 42, lakini pia katika waliorudisha 38 na kufika katika tano bora na mwisho pia kupigiwa kura na Halmashauri Kuu ya Chama cha Mapinduzi kufika katika tatu bora. Kwa hiyo, nichukue fursa hii pia kumpongeza sana, na pia kumpongeza Mhe. Rais kwa kumpa nafasi hii yenye umuhimu kwa taifa letu na nchi yetu kwa ujumla.

Vile vile, niseme pia ni sifa kubwa kwa akinamama kuwa leo Mhe. Waziri kukamata wizara hii na mimi ningependa kama ningekuwa Mhe. Waziri sio jamaa yangu lakini pia naomba awe rafiki yangu. Kwa sababu kwa kweli huyu mama ana sifa nyingi, ni mzoefu basi nichukue fursa hii kumuomba Mhe. Waziri tuwe marafiki, tuwe karibu, ninapokuwa na yeye karibu na mimi nitapata kuchota hayo mengi aliyokuwanayo ili na mimi niweze kufaidika, na nitambe kuwa mimi nina rafiki ambaye kwa kinamama na kinababa ni mtu muhimu katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia nikiri kwamba hivi leo afya yangu haiko vizuri, lakini tayari maoni yangu na mawazo nimeyapeleka katika hii wizara maswali na maoni na ninaamini Mhe. Waziri atanisaidia. Lakini niseme pia

nitazungumza machache ambayo ninahisi yataweza kumsaidia na kusaidia nchi yetu.

Suala la kwanza, nataka kuipongeza serikali kwa maamuzi makubwa waliyoyachukua katika siku mbili za nyuma hasa baada ya wafanyabiashara na kilio cha Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kuzungumzia suala zima juu ya makontena matupu ambayo yamekuwa kikwazo ndani ya Bandari yetu ya Zanzibar, ambayo imekuwa ni katika bandari muhimu kwa visiwa vyetu vya Unguja na Pemba katika kuhakikisha kwamba faida nyingi ambazo zinapatikana katika bandari hii.

Huu ni mfano mkubwa sana kwa nchi yetu na demokrasia kuonesha kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar japokuwa sisi sote humu ndani au wengi ni Wajumbe wa Chama cha Mapinduzi mbali ya wale walioteuliwa, ni kwamba serikali imekuwa sikivu, imeweza kuchukua maoni na kuheshimu mapendekezo ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kama sisi *backbencher* na kufanya maamuzi ya haraka.

Tunampongeza Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa kwenda jana bandarini na kufanya maamuzi haya kuhakikisha kwamba, bandari yetu inaweza kufanya kazi na kukidhi haja kwa ajili ya wafanyabiashara wetu, ili hizi fedha zipatikane ndani ya serikali zaidi ya mabilioni yasipotee zirudi katika hazina yetu na kazi izidi kwenda mbele. Hili ndio jambo kubwa kabisa, napenda niipongeze tena na tena, ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti, pia nataka niseme wizara hii kuchukua nafasi kuweza kuwasaidia wananchi wetu kuweka unafuu katika Mwezi Mtukufu wa Ramadhani, kuweza kuwasaidia wananchi kwa kuleta unafuu katika biashara mbali mbali kuweza kuondoa *duty* na ushuru wote ili uweze kutoa *charges,* wameweza kuupunguza na kuleta unafuu kwa wananchi wetu.

Vile vile, nataka nizungumzie matatizo ambayo pia yanatokezea ya *multiple licensing*, kwamba makampuni mengi ya biashara au taasisi nyengine zinakuwa zinapata matatizo ya kulipa leseni moja, mbili, lakini pia wanakuwa wanapitiwa na Halmashauri. Ni vizuri pia katika suala zima la *licensing* likajulikana moja kwa moja ni taasisi gani, ni leseni gani na hasa wafanyabiashara wa chini wanapopitiwa na Manispaa, wanapita watu wa Baraza la Mji, mara wanapita Halmashauri, kuna maeneo mengine mara wanapita watu kutoka Serikali Kuu. Kwa hiyo, lazima ijulikane iwe kuna wepesi na kitu ambacho *transparent,* kinajulikana kwamba ni leseni gani

anatakiwa mtu akate na kwa biashara ipi, tuondokane na masuala haya ya urasimu.

Hapa nataka nimshauri Mhe. Waziri ni muhimu kwamba kama alivyozungumza mjumbe mmoja leo asubuhi, kwamba wizara yake inagusa maeneo mengi, inagusa katika sehemu ya utalii na kama tukirudi nyuma katika mwaka 2005/2010 wizara hii pia ilikuwa inaitwa *Ministry of Tourism, Trade and Investment;* yaani Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji. Sasa ni muhimu wizara hii inagusana na maeneo mengi, kama nilivyosema utalii, Wizara ya Fedha ukienda kwenye mawizara mengine ya Mhe. Haroun Ali Suleiman masuala ya Utawala Bora, Wizara ya Kazi, kwa hiyo maeneo mengi wizara hii inaingia pamoja na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji.

Kwa hiyo, biashara ni katika eneo moja muhimu sana kwetu, ukipita Zanzibar hata hivi leo kila nyumba moja utakayopita nje kuna mlango wa duka, biashara ndio maisha yetu hata huko nyuma tulikotoka na katika mkakati wa kupunguza umasikini Zanzibar tumezungumza maeneo matatu, *tourism, trade and services*. Hii yote ni biashara moja kwa moja, kwa hiyo ni lazima wizara yake iunde kitengo ambacho kitakuwa ni kilio cha kuwasikiliza wafanyabiashara.

Hili tatizo lililotokea juzi kuhusiana na biashara masuala ya kontena halitakiwi kabisa kuja Barazani, linatakiwa limalizwe ndani ya serikali watu waweze kulisikia. Wanazo taasisi zao kama *Zanzibar National Chamber of Commerce, Industry then Agriculture* walikuwa walibebe hili, wawe nalo na kuwe kuna kitengo, lakini kwa bahati mbaya limetoka limekaa muda mrefu na mwisho limeishia Barazani kwa Wajumbe limekuja hapa likapigiwa kelele.

Mhe. Mwenyekiti, hivyo mimi nashauri sana kiundwe kitengo cha kushauri, cha kusaidia na pia kutoa *guidance* na *advice of the board* katika upande wa Wizara hii ya Biashara, Viwanda na Masoko, kuwasaidia wafanyabiashara wetu wa ndani pamoja na wawekezaji kwa ujumla. Lakini pia katika maoni yangu nataka niseme kwamba suala la mpango mzima wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Mwenyekiti, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hivi sasa imepanga katika mpango mkubwa ambao uwe unasimamia kutoa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutoka hapa tulipo na kwenda katika mpango mkuu kama wa nchi ya Malaysia, ambapo wameanzisha kitengo kinaitwa *BRN (Big Results Now*).

Mimi ningemshauri sana Mhe. Waziri, atafute njia ambayo serikali yetu pia katika mpango mzima wa *BRN* Zanzibar itashiriki kiasi gani, Zanzibar itakuwa inafanya kazi kwa ukaribu gani pamoja na Serikali ya Jamhuri ya Muungano, Zanzibar itakuwa inafanya kazi vipi kwa kupitia Ofisi ya Makamu wa Pili ambao wao ndio kiunganishi pamoja na Ofisi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano Mhe. Samia Suluhu Hassan kule Tanzania Bara, ili kuhakikisha kwamba Zanzibar katika mpango mzima wa *BRN* ambao wamei-*adopt* kutoka Malaysia na sisi tutakuwa hatuko nyuma, tunakuwa tuko nao pamoja katika huo mpango ambao wao wanalenga katika miaka ya mbele kwa pamoja.

Pia nataka nitoe rai na wazo kwamba tayari katika kikao hiki tuna mpango wa kuletewa sheria na sera ya mafuta na gesi. Lakini Mhe. Mwenyekiti, katika suala zima la mafuta na gesi kuna kitu kinaitwa *value chain*, yatakuja makampuni tafauti ambayo yatahitaji, lazima wananchi wetu hasa wawekezaji tusiangalie wale wafanyabiashara wetu wa ndani ambao ni wazalendo, tuangalie pia mpango mzima wafanyabiashara ambao wazalendo na ambao ni wakubwa watatumiaje hizi huduma kuwasaidia wafanyabiashara wadogo wadogo.

Ni mfano mzuri sana kama Mzee Said Salim Bakhressa kama kwenye biashara zake za boti, anachukua vijana anawafundisha ili waweze kufanya ile kazi moja kwa moja, hata kwenye kiwanda cha maziwa tumeona.

Kwa hiyo, katika suala zima la mafuta na gesi ile *value chain* yote ambayo wananchi wanatakiwa wafaidike tusije tukakuta kwamba katika *service* hii ambayo itahitajika ndani ya mafuta na gesi watu wanatoka nje wanakuja hapa kuja kushiriki.

Kwa hiyo, lazima wananchi wetu tuwatayarishe na wawekezaji wetu wa ndani ambao ni wazalendo tuhakikishe tunawashika masikio kwamba watu ambao wataajiriwa, watu watakaoingia katika kazi yote nzima ni Wazanzibari. Pia tuangalie katika suala zima la *real estate*, mambo ya kukodi nyumba, makao makuu yao kazi zao watafanya wapi wasije wakaondoka wakenda Dar es Salaam, wanakuja Zanzibar na Helkopta na kuondoka, lazima makao makuu yao yote yafanyike katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba wakodi nyumba, wafanye biashara, wakodi magari; huduma zote hizi asilimia 99 tuzipate sisi hapa Zanzibar kwa ujumla.

Mhe. Mwenyekiti, pia, nataka nizungumze suala la *Diaspora* ambao hawa Mhe. Rais katika hotuba yake ukurasa nafikiri wa 72 alizungumza kwamba:

"Napenda nitoe shukurani zangu za dhati kwa 'Wanadispora' kwa michango mikubwa wanayoendelea kuitoa, ya hali na mali, kwa ajili ya kuendeleza sekta za kiuchumi na kijamii hasa kuendeleza elimu, afya, biashara na uwekezaji. Nawaomba waendelee kuwa pamoja nasi kwani; *'Mtu Kwao ndio Ngao"*.

Haya namnukuu Mhe. Rais katika ukurasa wa 72 katika hotuba aliyokuja kufungua katika kikao chetu cha Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, lazima kwanza wizara yetu hii kwa kushirikina na wizara nyengine zote kwa ujumla na serikali, kwanza kutambua kwamba hawa *Diaspora* tulikuwa tunaambiwa kuwa ni wazalendo hawa ambao wako nje wanatusaidia sisi, wanashirikiana na serikali yetu tunao wangapi na tayari taasisi yao ipo na wana mkutano mkubwa wanatarajia kufanya mwezi wa Agosti.

Katika mkutano huu mimi nashauri sana unaofanyika Agosti uendane pia pamoja na mazungumzo ya wajasiriamali wadogo wadogo na pia kutoa fursa katika maeneo tafauti ambayo tayari serikali yetu inataka kuyalenga katika miaka ya mbele, hasa kwa upande wa Kaskazini Unguja pamoja na kisiwa cha Pemba.

Sisi tuna mpango wa kujenga suala zima la masomo ambayo masoko haya yatakuwa ni madogo, lakini baade masoko haya serikali kwa kushirikiana sisi pamoja na Wabunge na Wawakilishi kuifanya kuwa ni *centre* moja kwa moja ya huduma ambazo zitaweza kuwafikia. Kwa sababu malengo ni kuhakikisha kwamba hizi nafasi za kibiashara, fursa za huduma zinasogezwa kwa wananchi huko mikoani.

Hapa patakuwa na *role* kubwa sana, kwa hiyo lazima wizara yetu pamoja na zile fursa zote ambazo hazikuwepo ni muhimu hawa wananchi ambao waliokuwa wengi ni masikini wako vijijini wanaweza kuona na kuzipata, hawa wasiwe wako nyuma, wapelekee waone, wafundishwe, na walelewe,.

Pia katika mnasaba huo huo nataka nizungumze kwamba kuna umuhimu wa hizi fursa za kibiashara katika kuwatayarisha wanafunzi na vijana katika maskuli kwamba kuwatafuta watu, kwa sababu mwanafunzi anamaliza kidato cha nne cha sita anakwenda chuo lakini katika kufanya katika eneo ambalo yeye anataka kufanya kitu gani anakuwa hajui anakuwa kama amepotea.

Kwa hiyo, ni muhimu hizi katika elimu wanazozipata katika biashara lakini pia ni vizuri pia wakazipata katika *theory* kuwatafuta watu kwenda kuwasomesha huko maskulini kuwatoa katika maeneo tafauti. Lakini hawa pia kutafuta wadau ambao ni Wazanzibari, Watanzania tafauti.

Hakuna tatizo kumualika mfano Mzee Said Salim Bakhressa kuwatia na wanafunzi Bwawani elfu moja akaongelea kuhusu maisha yake alianza vipi kutoka anafanya biashara ndogo ya *ice cream* mpaka leo amekuwa na viwanda na matajiri, ni mfano ili kuwafanya watu kuweza kuwapenda mashujaa na kuingia katika mashujaa hasa ya biashara, na inawezekana na katika elimu hizi pia tuisukume vijijini ili wananchi wetu wawe na matumaini. Wananchi wetu ni masikini wanahitaji kuelimishwa na kupewa ile ndoto ambayo serikali itakuja kuifanya waweze kuiona moja kwa moja.

Pia, nataka nizungumze kidogo mfumko wa bei ambao hutokana na serikali wakati wa mwisho wa mwezi inapolipa mishahara pamoja na maeneo ya sekta binafsi. Mhe. Waziri kuna tatizo wakati mwengine wakati serikali mwisho wa mwezi inapowalipa mishahara kwa wafanyakazi wake pamoja na sekta binafsi hutokezea pale suala la *demand and supply*, kwamba mahitaji yanayohitajika na fedha zinazoingizwa watu wanaponunua manunuzi zinakuwa zinabadilika.

Ni vizuri wafanyabiashara wakatafutiwa njia ya kuhakikisha kwamba pale wanakuwa hawawaumizi wananchi katika suala zima katika ambapo wao wanakuwa wameshapa zile huduma zao hasa baina ya tarehe 5 na tarehe 15. Kwa sababu unakuta baina ya tarehe 20/23/24 na 25 kama serikali italipa mishahara tarehe 24 mpaka tarehe 28 unakuta hasa wao wafanyabiashara wanakwenda kulipwa fedha ambao wale waliokuwa wamekopa. Lakini baina ya tarehe 1/2/3 unakuta zile huduma zinaanza kupungua pesa inakuwa ipo nyingi nje lakini pia mahitaji yanakuwa madogo, unakuta sasa vitu vinaanza kupanda bei.

Ni muhimu pale huduma zote hasa katika mboga mboga vyakula ambavyo ni *chicken, beef* na vitu vyengine vyote hivi vinakuwa vinabakia haviko *stable*. Nimemsikia leo Mjumbe alikuwa akichangia aliuliza swali la bei ya nyama kwa pamoja. Lakini haya yote mahitaji ambayo ni *daily commodities* tuna tatizo kubwa kwa pamoja hasa katika masuala ya nyama hapa kwa ujumla. Kwa hivyo, ni vizuri ikatafutwa njia ambayo haya masuala moja kwa moja yakaondolewa na yasiwe yanatokezea.

Mhe. Mwenyekiti, pia nilikuwa nataka nitoe rai moja mimi nilikuwa Mjumbe wa Baraza la Biashara ambalo kwa muda mrefu nafikiri sasa hivi halijafanyika.

Mimi ninaamini kwa upeo wangu na kwa mawazo yangu kwamba Baraza la Biashara la Zanzibar ambalo linaitwa *Zanzibar Business Council*, ni katika eneo muhimu sana ambapo serikali itaweza kukaa pamoja na sekta binafsi kuweza kuzungumza changamoto walizonazo.

Mhe. Waziri nakushauri wakati mtakapofanya tena kikao chengine cha Baraza la Biashara, nakuomba uchague Waheshimiwa Wawakilishi 5 pamoja na Spika wetu waje kuwa ma- *observer*, ili kuweza kusikia yale mnayozungumza, wao hawahitaji kuchangia wasikilize, wawe tu ma- *observer* washiriki na kile kikao kitakachofanyika Ikulu baina ya wale mawaziri 10 na wale wenyeviti ama taasisi 10 wakae wazungumze. Lakini pia pafanyike *follow up* baadhi ya ambao wanakubaliana.

Kwa kweli lazima nikiri katika mengi ambayo yamezungumzwa katika Baraza la Biashara imekuwa ni eneo la kupiga kelele lakini mgawanyo wa kazi baada ya yupi atakuwa afanye kitu gani halipo. Hili pia linatokana na mapungufu ambayo hii Jumuiya ya Wafanyabiashara na wawekezaji na *Zanzibar National Chambers of Commerce Agriculture and Industry* kwamba kutokuwa wao wenyewe, kutokuwa wako pamoja katika jambo ambalo wanalolitaka pia. Ni muhimu wao wenyewe pia washikane waangalie ni yepi wataweza kuyafanya kwa maslahi ya nchi.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa muda wako umemaliza.

Mhe. Simai Mohamed Said: Naomba minalizie dakika moja ku- *summary*

Mhe. Mwenyekiti: Nakupa umalizie.

Mhe. Simai Mohamed Said: Ahsante. Baada hapo pia napenda nishauri utapokuja kufanya *summary* uzungumzie suala zima la *Finance bill Act* iliyopitishwa mara hii 2016 kwa wafanyabishara wa Zanzibar wataathirika upande gani hasa wa ndani katika biashara zao za ndani ya Zanzibar, na pia katika huduma ambazo wale wanaokwenda kwa upande wa Bara kama kweli kuna athari ambayo imefanyika wizara yako kwa kushirikiana pamoja na Wizara ya Fedha mtahakikisha vipi kwamba wao wanaondokana na hizi changamoto, na kama watafaidika ni jambo gani ambalo mtazidi kuhakikisha kwamba linakuwa endelevu.

Baada ya hapo mimi nakushukuru kwa nafasi naunga mkono hoja asilimia mia kwa mia. Naomba sana Mhe. Waziri atakapokuja anisaidie kwa ufupi kabisa

mawazo na pia kama nilivyosema kwamba naomba sana awe rafiki yangu wa karibu sana, ili niweze kuchota yale ambayo aliyokuwa nayo.

Baada ya hapo nashukuru sana kwa fursa, Mwenyezi Mungu akubariki. Ahsante Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi*)

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyeniwezesha hapa kusimama na nikaweza kupumua pumzi zake hizi, si ujanja wangu wala akili yangu, wala si maarifa yangu, na sijui saa ngapi atazihitaji, huo ndio mtihani sasa, na aliyekuweko mbele msubiri nyuma.

Mhe. Mwenyekiti, nichukuwe fursa hii kumpongeza Mhe. Waziri na watendaji wake na Katibu wake mpya na Waziri mpya, nafikiri tunaweza tukapiga hatua pengine mbele.

Nije na kilio changu kidogo (*ZBS*) ukurasa wa 45. Mhe. Mwenyekiti, leo nitachangia kwa lugha nyepesi na kwa muda mfupi kabisa, naona wizara yenyewe leo haina vishindo vikubwa.

Niombe serikali au wizara hii iongeze nguvu sana kuhusu kwenye viwango. Tumeshuhudia nyumba nyingi sasa zikiungua kutokana na waya *fake* za nyumba, bidhaa nyingi kutoka China, pasi, majiko ya gesi chini ya viwango. Hapa serikali kidogo iongeze nguvu baada ya walizoziwekeza.

Vile vile, Mhe. Waziri nitataka kujua una wataalamu wangapi katika kitengo hichi, una maabara ngapi. Unajua Mhe. Mwenyekiti, tuna mchezo tunafanya sisi humu ndani tunafanya ndugu zetu wa Tanzania Bara wakati sisi hatujawa tayari kuanzisha kitu yanatu- *cost* sana mambo haya, *mbuzi anakula majani kutokana na urefu wa kamba yake*, tusifate mtu, tumeanza na vitu chungu nzima nikitaka kuvitaja hapa nitakuja kukera watu bure haina haja mwezi mtukufu wa Ramadhani huu mengine weka akiba.

Halafu nitataka maelezo kuna maabara ngapi na una wataalamu wangapi na unahitaji wataalamu wangapi katika *ZBS*. Wanaoumia ni wanyonge wa nchi hii, ambao waliotupigia kura sisi, si kitu kizuri. Halafu nitataka kujua mashirikiano yenu nyinyi kati ya *TBS* na *ZBS* yako na ndugu zetu wa damu.

Mhe. Mwenyekiti, nije kunako mwani huu ndio ulioniandikia historia humu ndani. Mhe. Mwenyekiti, huwa nasema mara nyingi kuna milango mitatu ya

kuingilia humu ndani, mara nyingi hurudia. Uteuzi wa Mhe. Rais, viti maalum au kuchaguliwa na wananchi.

Mwenyezi Mungu kanijaalia neema kubwa sana nimezungukwa na bahari, wapiga kura wangu wote jimboni kwangu, huwa naumiwa ambao wametuchagua wamesema tuje huku tuwasemee mwani umekuwa kilio kikubwa. Lakini mimi naomba serikali isemee tu sijui, iweke wazi bora wapate kujua wananchi kuliko kesho, keshokutwa, mwaka, mwakani, tuko mbioni, matunda yake utayaona muda mfupi tu, wanaoumia ni wananchi na wametuchagua kuja kuwasemea.

Ikiwa leo karafuu wametafuta utaratibu wa kuzipandisha bei na kununua leo kwa sababu gani. Mimi nilikuwa sitaki hata kuzuia kitu katika wizara hii lakini hapa kidogo nitahitaji maelezo na Mhe. Rais aliagiza, si maneno yangu, wizara nne ziende zikakae; Biashara, Kilimo, Fedha na Afya. Sijui wamekaa vikao vingapi wakafika hatua hii hatuwezi kwenda.

Nije na kiwanda cha sukari mwekezaji yule nataka kujua zile nyumba alizopewa mwekezaji kule au ameshakabidhi serikali au tulikuwa na huruma za mdomo tu vitendo hatuna. Mwekezaji anazidi kuumia yule, siku zote mua wake unapigwa moto kule. Basi tumuonee huruma zile nyumba zake zilizochukuliwa na serikali wamkabidhi, miaka mingapi, nafikiri juzi juzi tu kapata kibali cha sukari kupeleka Tanzania Bara sijui ndio huo mua wake au vipi, na hapa nitahitaji maelezo ana kibali kweli cha kupeleka sukari kule naye.

Nije kwenye zao letu ambalo tunalitegemea na Mwenyezi Mungu alijaalie lizidi kuendelea la karafuu. Hapa serikali niombe kwa makini kabisa na anisikilize sana Mhe. Waziri.

Baada ya kuwakopesha wakulima kwenda kuvuna karafuu hapa mngeongeza nguvu katika miche ya karafuu huu ushauri wa bure wala sitaki kulipwa mimi. Baada ya kuwakopesha wale kwenda kuchuma karafuu uongezeni nguvu kwenye miche ya mikarafuu inazidi kupungua tu Pemba mikarafuu, na ndio tunayotegemea ndio uti wetu wa mgongo huu.

Leo Pemba niende nikaulize kuna daktari bingwa wa mifupa aliyekuwepo kule Pemba, anayeanguka kwenye mkarafuu anatibiwa vipi. Tuseme la ukweli jana tumemaliza Wizara ya Afya hapa tumezungumza tusiwe na huruma ya mdomo vitendo vinatakiwa. Leo mnyonge kaanguka kwenye mkarafuu Pemba kule, nani anamuhudumia, Mwenyezi Mungu aendelee kumsaidia, ndiye anayetuponesha sisi.

Leo hata daktari mmoja wa mifupa hakuna kule Pemba, na *x-ray* zenyewe mtihani ukipiga kelele *ya Allah*. Hapa nahitaji maelezo kuhusu kupelekea angalau daktari bingwa mmoja kisiwani Pemba kwa kutibu hata kwa msimu wa karafuu iwe hivyo hivyo kama mvua za masika mwaka hata mwaka.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia kuhusu Sekta ya Viwanda. Mimi nafikiri sasa mfike pahali baada ya kuwa sasa hakuna ajira tutafute miundombinu kwa kutafuta wawekezaji waje. Lakini tusije kuweka wawekezaji tukaja kuwatesa tuwe makini, sio mtu anaomba kibali cha uwekezaji miezi sita, mitatu panda ngazi shuka, kwenda kusini mpaka mtu anafariki dunia. Tuwe makini hizi nafasi wenzetu wanazitafuta, twendeni tukajifunzeni Rwanda mpaka Rais anaongezwa muda, hakuna vibali vinavyokaa kwa muda mrefu, hebu tujaribu kufundishana kwa wenzetu, tunasoma nini? Tunatafuta wawekezaji akaja hapa mtu anawekeza mtu ana ardhi yake, na *lease* anafutiwa, sababu huijui. Tufike wakati tujenge utamaduni tusiwe na huruma ya mdomo tu, vitendo vikawa havionekani.

Nije kwenye Shirika la Bandari niendelee kuungana na mwenzangu Mhe. Simai Mohamed Said (Mpakabasi). Namshukuru sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, na namuomba tena Rais mwenyewe na Makamu wa Pili wa Rais kama alivyofanya Mhe. Rais John Pombe Magufuli aende Mnazi Mmoja akatembee, kama jana akifika Bandarini afanye siku aende Mnazi Mmoja akaione hali Hospitali ya Rufaa itakayokuwa.

Leo Mhe. Waziri, hebu nambie wafanyabiashara wale waliokaa na mizigo mumechukua hatua gani angalau kuwafariji na kuwapa pole. Leo mwezi Mtukufu wa Ramadhani wengine wana maduka pale kwenye lile jumba la Treni pale, wafanyabiashara ambao sasa hivi wangejisaidia, mumekwenda kuyavunja pale hakuna chochote, njia imefungwa watu hata kufanya ibada wanasongamana utafikiri wako *Swafa* na *Mar-wa*. Tungesubiri wale watu, wameomba, ni binaadamu, mwezi mmoja mpaka iishe Ramadhani, leo hakuna *movement* yoyote, mimi nawakuta watu mpaka barabarani pale hakuna kinachoendelea, hakuna *movement* yoyote, hakuna kibali, hapana *permit*, hakuna *Construction* yoyote, kilichofanywa hicho kibali kichukuliwe kipelekwe *UNESCO*, watu wameomba wana biashara zao za Ramadhani angalau tuwafikirie jamani huu mwezi mkubwa. Watu wanaleta Makontena, wana biashara zao za mwezi wa Ramadhani. Sasa Wizara ya Biashara imechukua hatua gani kwa wafanyabiashara, ni wizara yenu hii.

Vile vile, nakuombeni tena Wizara ya Biashara mkakae na Miundombinu mtafute utaratibu pale pahali palipoazimwa kuweka Makontena kwa muda wa

miezi sita baada ya Waheshimiwa kupiga kelele humu ndani, mkatafute pahali isije kufika pahali tena mpaka nyumba inataka kuanguka ndio mkatafute pahali.

Mkatafute eneo Wizara ya Biashara na Miundombinu, wizara mbili hizi mkakae Mhe. Ali Abeid Karume na Mhe. Amina Salum Ali mkafikirie pahali mkae, miezi sita pale ni muda mdogo na baada ya kupiga kelele humu ndani Waheshimiwa hoi hoi nacho kilindo ndio tukafikia hatua hii ya pale angalau makontena yatawekwa hivi sasa.

Inafika wakati meli Zanzibar zinataka kuja uchumi tunao tunapiga kelele, rizki tunaipiga teke, maana yake meli ngapi sasa hivi unafikiri ziko nje zinataka kufunga gati Bandari ya Malindi zinashindwa, hii ndio hali. Mhe. Mwenyekiti, mimi nafikiri mchango wangu ulikuwa ni mdogo na ulikuwa ni mwepesi sana, sio mzito kama hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, nije kunako mfumko wa bei, ndugu zetu wa Pemba vitu vyao vinakuwa bei juu kuliko hapa Unguja sijui sababu gani mtatwambia wizara.

Mhe. Waziri hebu kafanye utafiti, kwa sababu gani vitu vinakuwa bei juu kuliko hapa Unguja, sababu gani. Mfumko wa bei unapanda na kushuka, leo kaangalie pale pale kwenye *butcher* ya nyama Marikiti huyu anauza shilingi elfu 9000, huyu 8000 hapa 10000 hawa watatu hawa moja, mbili, tatu wao kwa wao. Mnatoka huko afisini kwenda kuangalia ile hali. Lazima kuwe na utaratibu hapo hapo ukienda huyu anauza elfu 9000, huyu 8000 huyu 10000 uhalali uko wapi. Lazima kuwe na kitengo cha kudhibiti hali ya mfumko wa bei, wanaoumia ni wanyonge wa nchi hii, wakulima na wakwezi, ambao ndio waliotuchagua kuja kuwatetea au kuwasemea shida zao. Mfumko wa bei bwana bei juu Pemba, bei ya mchele hapa na Pemba tafauti, ya saruji hapa na Pemba tafauti. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, nataka kujua ile kauli ya serikali kuhusu nguo za ndani imefikiwa wapi yaani mitumba iliwahi kutolewa kwenye Baraza hili, ipo au haipo? Sio jambo baya wanyonge ndio wanaoumia lakini vile vile zina mitihani zile nguo pengine zina maradhi vile vile tusije tukaumiza watu, hapa kidogo niko katikati siko huku wala huku.

Nataka kujua *formular* yake ikoje maana mnyonge hawezi kununua nguo ya sikukuu kipato chake kidogo, lakini pengine ile nguo akivaa inaweza kumdhuru, siwezi ku- *balance* hapa...

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa muda wako bado dakika moja.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Jengine la mwisho kwa kumalizia bila kunambia muda wangu umekwisha. Utamaduni wetu naomba urudi tena kama zamani katika nyumba zetu kupanda miti kama zamani, minazi, mikarafuu. Lakini leo njia yote barabara utakuta imepandwa miarubaini si kitu kizuri, tungerudisha minazi au mikarafuu tukapanda mule angalau mtu akaja akaona aah ndio uchumi wa nchi huu, lakini tunarudia kupanda miarubaini, barabara yetu ni miarubaini.

Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru sana.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Awali nilimtangaza Mhe. Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira lakini kwa vile kuna mchangiaji mmoja tu Mhe. Suleiman ninamuomba achukue fursa hii na baadae Mhe. Mhe. Waziri amalizie.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi ninashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niende kwenye suala la viwanda. Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar tulikuwa na viwanda vingi, kama kile Kiwanda cha Sigara, Kiwanda na Maziwa na viwanda vyengine.

Mhe. Mwenyekiti, leo hii Zanzibar hata kile Kiwanda cha Soda pale Maruhubi hakifanyi tena kazi, halafu tunasema vijana wetu wapate ajira. Hivi ninataka nimuulize Mhe. Waziri, kwa sababu viwanda ni nyenzo moja ya kuwaongezea vijana kupata ajira na kuiongezea serikali mapato, lakini ikiwa hatuna kiwanda hata cha tumbaku hapa Zanzibar, kweli hizo ajira kwa vijana wetu tutazitoa wapi?

Hivyo Mhe. Mwenyekiti, ninamuomba Mhe. Waziri kwa vile yeye ni mama na mama ni mlezi, aliangalie hili na airudishe Zanzibar kupitia wizara yake hii, kama yeye ni simamizi kama pale zamani kwenye sekta hii ya viwanda.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye suala la karafuu. Zanzibar tunategemea zao moja tu la karafuu kama ndiyo biashara tunayotegemea inayotupatia kipato zaidi. Lakini nimuombe Mhe. Waziri ukienda kwenye sekta ya bahari kuna bidhaa ambazo kwamba zina bei kubwa zaidi kuliko hiyo karafuu. Kwa sababu

kuna vibenza vile vya kome. Hivi vibenza vya kome Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri hufika kilo moja shilingi laki moja na havishuki bei hivi vikafika elfu ishirini, hutembea hapo hapo kwenye laki moja, thamanini na kwenda na juu zaidi.

Hivyo, Mhe. Mwenyekiti, nimuombe Mhe. Waziri hili aliangalie, kwa sababu hapa pana mapato makubwa zaidi na liingie kwenye sekta ya biashara, na ikiwezekana hata serikali waweze kulichukua suala hili la vibenza vya makome.

Na huko huko kwenye suala la bahari kuna mazao yanaitwa majongoo. Zao hili nalo lina pesa kubwa sana, bei yake halipishani sana na vibenza vya kome. Kwa hivyo na hili ninaliomba Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri aliangalie ikiwezekana hata ikiwa na majongoo nayo iwe Serikali ya Zanzibar inaweza kumiliki wenyewe na kununua na kusafirisha kama vile inavyofanya karafuu. Kwa sababu hawa wavuvi wanaovua huko hawajui hata wanapopelekwa kusema la ukweli. Lakini ni kwamba vitu hivi havishuki bei vina bei kubwa. Hivyo naiomba serikali kupitia wizara yako Mhe. Waziri hili suala uliangalie na ulichukulie hatua kubwa zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, nikienda kwenye suala jengine ni suala la *vanilla*. Hapa Zanzibar kilimo sasa hivi ni *vanilla*, hiliki na mazao mengine. Lakini leo ukipita humo mitaani hata hiyo *vanilla* haijulikani na *vanilla* nayo ina bei kubwa sana. Kwa hivyo ninamuomba, Mhe. Waziri wa Wizara hii kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Maliasili na Uvuvi hili zao liimarishwe Zanzibar kwa sababu ni zao ambalo lina faida kubwa sana. (*Makofi*)

Pia, vile vile, Mhe. Mwenyekiti, nimuombe Mhe. Waziri kwenye sekta ile ya Jumuiya ya Wafanyabiashara wenye Viwanda na Wakulima. Ninakumbuka kwa sababu mimi ni mwanachama wa jumuiya, ninakumbuka Mhe. Waziri wa Biashara alipita alisema kwamba wafanyabiashara wote wa Zanzibar wawe ni wanachama wa Jumuiya ya Wafanyabiashara, ili kilio chao wakipeleke pale. Lakini hatua hii sijui ilipofikia mpaka hivi sasa. Kwa hivyo, ninamuomba sana Mhe. Waziri aweze kulitafakari hili na ahakikishe kwamba wafanyakazi wote wa Zanzibar wawe ni wanachama wa Jumuiya ile, kwa sababu wanachama wa wafanyabiashara wengi itakuwa pale tayari watakapokuwa na kilio chao, wanakaa na wanakitatua kwa umoja.

Hivyo, Mhe. Mwenyekiti, mimi nilitaka kutia baraka tu kwenye wizara. Sina mengi ya kuchangia isipokuwa ni hilo na ninaunga mkono asilimia mia kwa mia. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Suleiman. Naomba kabla ya Mhe. Salama Aboud Talib, tena bado aendelee Mhe. Waziri Hamad Rashid naye aitumie fursa hii.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. Kwanza nimpongeze sana Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko kwa hotuba nzuri na hasa kazi nzuri iliyofanywa pia na wataalamu wake.

Mhe. Mwenyekiti, kama unavyofahamu mahusiano yaliyo karibu sana ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko na Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, kwa sababu bidhaa nyingi za viwanda vinategemea sana kutoka katika Wizara ninayoiongoza. Kwa hivyo nasema kwanza nimshukuru Mhe. Waziri kwa kusimamia wizara hii katika kipindi kifupi sana na amefanya kazi kubwa sana. Kwanza ya kujua mambo ya msingi yaliyokuwemo ndani ya wizara yake ambayo yanataka kusimamiwa. Ikiwa moja ni kuangalia miundombinu iliyopo katika wizara. Amefanya hiyo kazi kwa ufanisi mkubwa sana. Na mimi ninafikiri katika jambo ambalo Waheshimiwa Wawakilishi kwanza cha kumsaidia Mhe. Waziri ni kumpa muda akatekeleza yale ambayo ameanza nayo.

Mhe. Mwenyekiti, la pili limezungumzwa sana suala zima la mikarafuu. Kwanza nataka tu niseme kwamba lazima tuishukuru sana Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar, ikiongozwa na Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein imekubali kutoa miche ya mikarafuu bure, imetoa miche ya mikarafuu milioni moja kila mwaka bure. Nasema hili ni jambo kubwa sana. Hakuna pahala popote duniani mkulima anapewa kila kitu bure. Zanzibar hapa wakulima wetu wanapata vitu vingi sana bure. Tatizo ambalo lazima tukubali ni kwamba upande mmoja serikali ni kutoa lakini upande wa pili ni yule anayepewa namna anakitunza kile alichopewa. Na hili ndiyo tatizo la msingi ambalo lipo.

Kwa hivyo inawezekana kabisa tusije tukafanya utafiti, lakini yule ambaye amekabidhiwa miche ya mikarafuu, serikali imefanya wajibu wake imemkabidhi miche, wewe uliyekabidhiwa miche ni vizuri ukaitunza wewe mwenyewe miche. Sasa kwa bahati mikarafuu milioni moja hatuna *man power* ya kusema kila pahala tutakwenda kukagua, haiwezekani. Lakini ni vizuri sisi tuhakikishe kama ile milioni moja kweli imetoka milioni moja, na kweli imekwenda kwa watu na watu waliopata kweli wameitunza. Basi hilo ni wajibu ninasema pande zote mbili. Sisi kama serikali tunaotoa lakini upande wa pili vile vile wa wananchi wanaopewa na wao wajitahidi namna ya kutunza.

Kama alivyosema Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum) ambaye ni Mjumbe wa Baraza la Mapinduzi, kwamba nidhamu katika kila jambo ni la msingi sana, bila ya nidhamu katika kilimo, bila ya nidhamu katika kazi, bila ya uadilifu, hakuna kitakachofanikiwa.

Mhe. Mwenyekiti, hilo naomba sana kwa Waheshimiwa Wajumbe kama ni viongozi sote tujitahidi sana katika maeneo yetu kukaa na wakulima wetu kuzungumza nao juu ya suala la taaluma wanayopata na matumizi ya ile taaluma waliyoipata. Hili ni tatizo la msingi ambalo ninaliona lipo.

Kwa hivyo, ninakubaliana na Waheshimiwa hapa kwamba sisi kwa upande wetu tutajitahidi kufuatilia kama kweli kile kiwango tunachokisema kweli kipo na kweli wanachukua, lakini wajibu wa kutunza bado unabaki kwa yule mtu ambaye amepanga mwenyewe. Hilo lilikuwa ni jambo langu la kwanza.

La pili, kuna suala la ukataji wa mikarafuu na minazi. Mhe. Mwenyekiti, hili jambo kwa kweli linaathiri sana. Na kama wanavyosema Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba idadi ya mikarafuu inapungua pamoja na kwamba tunaendelea kupanda, lakini ukipanda unategemea miaka minne, mitano. Na ukipanda mikarafuu milioni moja pengine utabaki mikarafuu laki mbili au tatu ndiyo itabaki hai. Lakini kasi ya kukata mikarafuu na minazi imekuwa kubwa sana. Tulikuwa na minazi kama milioni tano miaka mitano iliyopita. Leo tuna minazi milioni mbili na nusu. Ni kitu cha kusikitisha sana. Minazi imekwenda kabisa kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, watu wanajenga katika maeneo mbali mbali. Kwa hivyo hata tukitaka kuanzisha Kiwanda cha Mafuta ya Nazi sasa kutokana na uzalishaji wa nazi tulizonazo, hicho kiwanda hakiwezi kuwepo kwa sababu hakitakuwa na mali ghafi za kuzalishia. Tutaendelea na *trend* hiyo hiyo kwenye mikarafuu vile vile. Baadae utakuta hata karafuu tunazozalisha ni kidogo sana. Kwa hivyo ninasema na sisi tuna wajibu wa kutunza hizi rasilimali katika maeneo yetu. Maeneo ya mabonde hivi sasa yamevamiwa, maeneo ya mikarafuu inakatwa watu wanajenga majumba. Hivyo, hiyo ni hali ambayo tunayo na mazingira ambayo tunayo. Ni vizuri sote kwa pamoja tukalisimamia vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, suala la bidhaa zilikuwepo baharini ninakubaliana kabisa na Mhe. Mwakilishi aliposema kwamba bidhaa za baharini zina bei kweli. Jana nilikuwa na wataalamu wa kaa, wakaniambia Australia kaa bei yake ni Dola thalathini na tano, hilo moja. Na ukitumia zile *nets* ambazo niliwahi kuzitoa hapa kwa wavuvi unaweza ukapata kilo kumi mpaka kumi na tano kwa siku.

Sasa ukichukua wewe nusu tu ya bei hiyo, tayari umeshauondoa umaskini. Sasa ni vizuri watu wetu wakaelewa hili.

Nafikiri Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko ni vizuri tukajitahidi tukalisimamia hili la masoko, tukawaeleza wenzetu masoko yapo wapi, yanapatikanaje na utaratibu gani masoko hayo yaweze kufikiwa. Hilo ndiyo jambo moja la kufanya.

Lakini la pili ambalo tunalifanya sasa hivi kama jana ambavyo mumefuatilia kwenye vyombo vya habari, tunaanzisha kituo cha kuzalisha vifaranga vya samaki na bidhaa nyengine za baharini, wakiwemo kaa na kadhalika. Badala ya kwenda baharini kuvua, tunataka watu wetu sasa vile vile wafuge. Ninafurahi kusema kwamba wenzetu wa Kisiwa Panza kule wamefuga pweza. Pweza wale wanafika mpaka kilo tano, sasa hivi nimewakuta pamoja na mambo yao mengine waliyonayo na matatizo yao mengine waliyonayo, lakini ninasema ufugaji ule umeleta matunda mazuri sana. Tunataka tuanzishe maeneo mengi zaidi ya ufugaji. Tuna maeneo ya ufugaji kama 152 sasa hivi. Tunataka watu hawa wapate vifaranga vizuri ili waweze kupata mazao mazuri. Kama alivyosema Mhe. Mwakilishi ukijua soko lako vizuri na ukajua aina ya bidhaa inayotakiwa bei yake inakuwa kubwa sana.

Sasa mimi ninasema hili tunalifanyia kazi ili kukuza hii sekta ya uvuvi ili watu waweze kufaidika zaidi. Lakini ninasema jambo la msingi vile vile watu wetu lazima nao waweke na uaminifu ndani yake. Unaweza ukaweka maeneo ya ufugaji, wakaja watu wakavamia, wakapiga mabomu wengine wakachukua mazao wakaondoka. Sasa na uaminifu nao umekuwa ni tatizo la msingi sana. Tunahitaji kujenga uadilifu na uaminifu. *Industry* hii inaweza ikakua vizuri, ikafanya vizuri na tukapata mazao makubwa sana. Kwa hivyo ninasema ninakubaliana naye kabisa kwamba yapo mazao mengi sana baharini yana bei kubwa sana, kuna uvuvi mmoja unaitwa *fish caging*.

Kama kuna mtu anakwambia mimi ninataka samaki aliye na rangi fulani tu na avuliwe namna fulani. Anaweza kununua mpaka Dola hamsini kwa kilo. Sasa anasema kuna aina nyingi hizi zikitengenezwa vizuri, hizi ajira tunazozipigia kelele zitaweza kupatikana. Lakini na vijana wetu lazima wakubali kwenda kujituma kufanya hizi kazi. Suala la kukaa ukazungumza haiwezekani. Kilimo kina nidhamu zake, ufugaji una nidhamu zake, biashara ina nidhamu, viwanda vina nidhamu zake. Hizo nidhamu lazima tuzikubali ndiyo tunaweza tukapiga hatua.

Mhe. Mwenyekiti, nimesikia habari ya *vanilla* na kadhalika. Ninakubaliana nao kabisa lakini kama nchi ni vizuri tukaamua zao gani litatupatia mapato kiasi fulani, kwa sababu ardhi yenyewe tuliyonayo ni ndogo sana. Ardhi yenyewe hiyo hiyo tunaiharibu sasa hivi. Tunajenga ovyo ovyo, tunaharibu maeneo ya vianzio vya maji. Kwa hivyo tunahitaji kujua zao hili tukilipanda tunahitaji tupate *tons* ngapi na tupate lini. Huwezi kupanda kila kitu kwa vile ardhi yenyewe ni ndogo sana. Kwa hivyo ninakubaliana na wewe tutafanya utafiti tuone kwamba je, tupande *vanilla* au tupande kitu gani ambacho kitaleta *impact* katika uchumi. Hatuwezi tukapanda kila kitu.

Mhe. Mwenyekiti, lakini ninasema ninakubaliana na ushauri wake kwamba tuangalie bidhaa mbali mbali ambazo zitasaidia kufanya hiyo kazi. Lakini ninasema kubwa kwa upande wetu tunashirikiana sana na Waziri, yeye atatwambia ana mipango gani, kwa mfano kafanya kazi nzuri sana ya kupata kiwanda kidogo cha kuanza kuzalisha mwani, ku-*process* mwani.

Ninamshukuru sana na tutashirikiana na *UNIDO*, tunaifanyia kazi hiyo na jana bahati nzuri na mimi nimepata fursa tena ya kupata kiwanda chengine *FAO* watatusaidia hapa Zanzibar cha mwani huo huo. Kwa hivyo ninasema tutapiga hatua katika maeneo haya ya kukuza hii *industry*, lakini ninasema taaluma ni suala la msingi sana. Vijana wetu ni lazima wajitahidi kutafuta taaluma.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Waziri kwa mchango wako. Sasa ni zamu ya Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi naomba nichangie katika hotuba hii ya bajeti ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumpongeza tu Mhe. Waziri, kwa hotuba yake nzuri iliyojaa vielelezo lakini iliyotupa matumaini katika kuendeleza mpango wake, mwelekeo wake wa mwaka huu 2016/2017.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii pia kuwashukuru sana watendaji na ninasema hili ninawashukuru sana watendaji, maana yake ninataka kuzungumzia *issue* ya wajasiriamali wakiwa wengi wao ni wanawake. Ninawashukuru sana watendaji kwa sababu wamefanya kazi kubwa na ninaomba niliseme hili, kwa sababu watendaji wa wizara hii wakishirikiana na *ILO* wamechukua jukumu kubwa la kuwafundisha wanawake hasa katika suala

zima la kufanya kazi ya kupata elimu, kwa maana ya uzalishaji. Nimeona mara nyingi mafunzo mengi yametokea nikiwa mdau wa wanawake katika mambo ya *food processing*, mambo ya *packaging* lakini mambo *backpack making* na mambo mengine mengi mengi. Mhe. Mwenyekiti, hivyo utakuta wafanyabiashara wetu wengi sasa hivi wana elimu ya kutosha kupitia wizara hii. Kwa hivyo ninawapongeza sana.

Vile vile, Mhe. Mwenyekiti, wanawake hao wameweza kupata fursa mbali mbali na kwenda kwenye maeneo mbali mbali ndani na nje ya nchi, kwa sababu ya kupitia wizara hii lakini na mafunzo waliyopewa ni kile ambacho wanakizalisha. Pamoja na kwamba wanazalisha kwa kiwango kidogo lakini wanazalisha kitu ambacho kinaeleweka na chenye tija kwa nchi na kwa wenzetu. Hivyo tu niiombe wizara tuendelee kushirikiana pamoja na wizara yangu ili tuweze kuhakikisha kwamba wanawake hawa ambao wengi ni wajasiriamali tunawapatia eneo linalokidhi haja ili waweze kuwa na kituo cha uzalishaji cha kudumu, ili pia waweze kusimamiwa vizuri na tuweze kupata bidhaa zilizo bora zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa naomba nichangie kidogo kuhusu mchango ambao alizungumza Mhe. Hamza Hassan Juma, kupitia Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko, kwa suala zima la uwekezaji ambalo alilizungumzia sana katika kutoa *lease*. Naomba nimshukuru sana Mhe. Hamza kwa kazi kubwa anayoifanya, lakini pia naomba nishukuru kupitia Baraza lako hili wawekezaji wengi wanaokuja hapa nchini kwa nia ya kuwekeza hapa nchini kwetu.

Lakini tu naomba nitoe elimu kidogo Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu ya maendeleo ya nchi hii tunawapenda sana wawekezaji. Lakini kabla hatujawapa *lease* zile tunachukua tahadhari ya kutosha, ikiwemo kulinda maslahi ya nchi lakini na maslahi ya watu wetu, lakini pia kuangalia faida na hasara za ile *concept* ambayo wanakuja nayo. Ndiyo maana wanapofika lazima tufanye *impact assessment*, siyo kila mtu anayekuja na *concept* na uwezo wake kwamba tutampa *lease*, hapana.

Aidha, uangalifu mkubwa tunauchukua Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa watu wengi wanaokuja na hawa wawekezaji ambao wanakuwa kama kidogo kama madalali, wanakuja kwa sababu ya faida zao. Na hatimaye wakati mwengine unaweza ukatoa *lease* ukaona watu wameingia mitini, lakini *lease* pale ipo, eneo limekaa bila ya uzalishaji wowote wala serikali yenyewe haifaidiki chochote. Ndiyo maana tahadhari kubwa tunaichukua.

Lakini tunafanya kazi hii pia kwa sababu tunakuwa na tahadhari kubwa, kwa sababu ya kuondoa kila siku migogoro ambayo siyo ya lazima na isiyokuwa na tija kwa taifa letu na migogoro ambayo inayoepukika. Kwa hivyo naomba tu niwajuulishe Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako hili Tukufu kwamba hizi *lease* hazitolewi tu kama tunavyotoa tunapokwenda kununua buku au tunavyokwenda kununua karatasi dukani, tunazitoa tukiangalia vigezo, tukiangalia utaratibu lakini na sheria za nchi ambazo zipo. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, mwisho kabisa naomba kuunga mkono hotuba hii ya makadirio ya bajeti kwa asilimia mia juu ya mia.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Waziri. Niwashukuru Wajumbe wote ambao wamechangia kwa siku ya leo na niwashukuru kwa utulivu wenu, lakini kwa sababu katika *order paper* zimemaliza shughuli za leo na hakuna tena wachangiaji, naomba niliahirishe Baraza hili hadi kesho mnamo saa 3.00 asubuhi.

(Saa 8.16 mchana Baraza liliahirishwa hadi
tarehe 24/06/2016 saa 3.00 asubuhi)